# Kielelekezi cha Ushiriki wa Mtoto



**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**
**Tanzania**
**2012**

# Kielelekezi cha Ushiriki wa Mtoto



Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Tanzania
2012

# Dibaji

Haki ya kushiriki katika kufanya maamuzi ya mambo yanayowahusu na haki ya ustawi wa mtoto ni kanuni muhimu ya kimsingi ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Mtoto na Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto. Kadhalika, Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009 inasisitiza na kuboresha haki za mtoto na kuweka masharti maalum kwa ajili ya kulinda haki ya kutoa maoni, kusikilizwa na kushiriki katika maamuzi mbalimbali yanayohusu Maendeleo na ustawi wake. Watoto wana haki ya kusikilizwa na kutiliwa maanani katika mambo yote yanayowahusu kulingana na umri na kadiri uwezo wao unavyoruhusu kuelewa mambo mbalimbali. Ushiriki wa mtoto unahusu watoto wote ambao wameshafikia uwezo wa kuwa na maoni bila kujali umri. Ushiriki huo pia lazima uwe mahala pote ( nyumbani, shuleni, kwenye jamii, kwenye mahakama), na mahala pengine popote ambapo ustawi na maslahi ya watoto yanazungumziwa. Ushiriki wa mtoto ni hali inayomuwezesha mtoto katika hatua mbalimbali za ukuaji wake, kuwa na nafasi ya kushiriki kikamilifu katika kutoa mawazo na kushiriki katika maamuzi ya masuala yanayohusu Maendeleo yake na yale yanayopaswa kutekelezwa na jamii husika.

Misingi ya ushiriki wa watoto ipo katika kanuni za binadamu, licha ya kuwepo kwenye mikataba ya kimataifa ya haki za watoto, Katiba ya Nchi, Sheria na Kanuni mbalimbali. Katika kusimamia utekelezaji wa haki ya ushiriki wa watoto, Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Jinsia naWatoto kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa masuala ya watoto imeandaa Kielekezi cha Ushiriki wa Mtoto  (Child ParticipalionToolkit) ambacho pamoja na masuala mengine kimechambua kwa kina dhana ya ushiriki wa watoto katika masuala mbalimbali. Ni matumaini yangu kuwa kielekezi hiki kitasaidia sana kutoa mwongozo wa ushiriki wa watoto katika masuala mbalimbali yanayolingana na uwezo,umri, na mahali walipo.



Tukae Njiku
Mkurugenzi wa Maendeleo ya Watoto

# Shukurani


Kielelekezi hiki kimetolewa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa msaada wa kitaalamu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa kushauriana na wadau mbalimbali wanaojishughulisha na masuala ya ushiriki wa watoto nchini Tanzania. Utayarishaji wake ulihusisha mashauriano yaliyofanyika katika wilaya 4 ambayo yalichangia kwa kiasi kikubwa katika rasimu ya kwanza ya kielekezi hiki na orodha ya mambo muhimu ya kuzingatiwa, mahojiano na watafitiwa kutoka vyama vya kiraia, pamoja na warsha ya wadau wakiwemo wawakilishi wa serikali na wa vyama vya kiraia ambayo ilipitia na kuchangia maoni zaidi katika rasimu ya kwanza. Watu waliojitolea muda wao na kuchangia uzoefu wao, maoni na mitazamo yao walikuwa ni pamoja na:

- Wilaya ya Bagamoyo , Wajumbe wa Baraza la Watoto la Kata za Kiromo na Magomeni
- Wajumbe wa baraza la watoto la Jiji la Mwanza
- Wajumbe wa baraza la watoto la kata ya Magu mjini
- Wajumbe wa baraza la watoto la Wilaya ya Temeke
- Maafisa wa Serikali ya Mtaa pamoja na wawakilishi wa ASIZE wa Wilaya ya Bagamoyo
- Maafisa wa Serikali za Mitaa, wakuu wa shule, viongozi wa dini, wawakilishi wa AZISE, wajumbe wa Kamati za watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi na wajumbe wa Kamati ya Mazingira ya Wilaya ya Temeke.
- Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Timu ya Uongozi wa Halmashauri, na maafisa wa serikali za mitaa, wawakilishi wa Asasi Zisizo za Serikali (AZISE), viongozi wa dini katika wilaya na Magu
- Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka Wilaya za Temeke, Hai, Siha, Bagamoyo, Manispaa ya Dodoma, Wilaya za Magu, Ngara, Kibondo, Kasulu, Manispaa ya Arusha, Wilaya za Mtwara, na Kigoma
- Wawakilishi kutoka World Vision Tanzania, ANCPANN, AFRICARE-Tunajali, REPSSI, PLAN International, REPOA, Dogodogo Centre, Children's Dignity Forum, NNOC, Twaweza, GNRC, and Save the Children.

Ni vigumu kwetu kutaja kila mtu kwa jina lake, hata hivyo tungependa kutoa shukrani zetu za dhati kwa kila mmoja aliyechangia katika kufanikisha shughuli hii. Aidha tunaishukuru Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Programu ya UNICEF Tanzania ya Ulinzi na Ushiriki wa Mtoto, kwa msaada waliotupatia wakati wa mchakato wa mashauriano.

# Yaliyomo


**Utangulizi ..... 6**
Ushiriki wa mtoto ni nini? ..... 6
Kwa nini ushiriki wa mtoto ni muhimu? ..... 6
Aina za ushiriki wa mtoto ..... 7
Ushiriki wa mtoto katika Tanzania ..... 7
Namna ya kufanikisha shughuli za ushiriki wa mtoto ..... 8
Vielekezi ..... 9
Vielekezi hivi vimeandaliwa kwa kuwalenga watoto wa miaka 12-18 na baadhi ya vielekezi vinaweza pia kutumika kwa watoto wa umri mdogo zaidi. Baadhi pia vinaweza kutumika kwa ajili ya vijana wa umri wa zaidi ya miaka 18 na/au watu wazima. ..... 10
Namna ya kutumia kitabu hiki ..... 10

**Sura ya 1: Tunawezaje kuunda au kuimarisha kikundi cha watoto? ..... 11**

1.1 Kujadiliana na watoto kuhusu ushiriki wa mtoto ..... 13
1.2 Kukubaliana kuhusu wajibu wa kikundi cha watoto ..... 16
1.3 Kuweka kanuni za kikundi ..... 17
1.4 Mchezo kuhusu uchaguzi huru na wa haki ..... 19
1.5 Mchezo kuhusu uongozi ..... 21
1.6 Kufanya maamuzi kama kikundi ..... 23

**Sura ya 2: Tunawezaje kuongeza kujiamini na kushirikiana kwenye kikundi cha watoto? ..... 25**

2.1 Mti wa maisha yangu ..... 27
2.2 Mti wa kikundi chetu ..... 30
2.3 Vikundi vya majadiliano kuhusu heshima ..... 32
2.4 Mchezo kuhusu ushiriki ..... 33
2.5 Majadiliano kuhusu masuala ya jinsia ..... 35
2.6 Kuelewa migogoro – mitumbwi ziwani ..... 37
2.7 Hatua sita za kutatua tatizo ..... 38
2.8 Michezo ya mawasiliano ..... 40

**Sura ya 3: Tunawezaje kutambua na kuchunguza masuala yanayohusu watoto katika jamii zetu? ..... 42**

3.1 Kutambulisha jamii kwa misingi ya masuala ya watoto ..... 44
3.2 Kitu gani kinachotufurahisha, kitu gani tungependa kibadilike ..... 47
3.3 Kuigiza kuhusu masuala ya watoto ..... 48
3.4 Kukusanya visa vya matukio ..... 49
3.5 Dira ya jamii inayojali maslahi ya mtoto 55
3.6 Kuchanganua matokeo ..... 52
3.7 Kukabiliana na masuala magumu ..... 53

**Sura ya 4: Tunawekaje malengo ya kazi? ..... 55**

4.1 Kuweka na kuchanganua dira ..... 57
4.2 Kuibua mawazo kuweka vipaumbele 59
4.3 Mti wa malengo na matatizo ..... 62

**Sura ya 5: Tunawezaje kupanga shughuli? ..... 65**

5.1 Kuandaa mpango wa shughuli ..... 67
5.2 Upangaji wa shughuli – mwelekeo ..... 69
5.3 Kuandaa bajeti ..... 71
5.4 Upatikanaji wa fedha – kuandika pendekezo la mradi ..... 72

**Sura ya 6: Tunawezaje kufanya shughuli za kikundi? ..... 73**

6.1 Kupata na kushirikiana taarifa katika kikundi ..... 75
6.2 Kujifunza haki za mtoto ..... 77
6.3 Kutoa maoni kuhusu mipango ya mitaa, sheria ndogondogo , na maamuzi mengine ..... 80
6.4 Kuinua kiwango cha ufahamu katika jamii ..... 82
6.5 Mazungumzo na watoa maamuzi ..... 85
6.6 Kutoa elimu rika ..... 88

**Sura ya 7: Tunawezaje kufuatilia na kutathmini shughuli au michakato? . ........................................................ 90**

7.1 Kupima hisia za mwitikio. ...................... 92
7.2 Orodha za Maoni ...................................... 94
7.3 Picha za mabadiliko................................. 96
7.4 Uwezo wa kufuatilia – mti wa kikundi chetu ............................................................ 98

**Sura ya 8: Tunavyoweza kutunza kumbukumbu za michakato na za kazi.................................................100**
8.1 Kuandika ripoti........................................102
8.2 Uhifadhi wa kumbukumbu kwa ajili ya kikundi.......................................................103
8.3 Uhifadhi wa kumbukumbu kwa ajili ya jamii............................................................104

**Sura ya 9: Tunawezaje kuimarisha mchango wa watu wazima katika ushiriki wa mtoto? .......................108**

9.1 Methali kuhusu watoto ........................107
9.2 Kitu gani ni muhimu? Vipaumbele vya watoto na vya watu wazima.............109
9.3 Manufaa na Mapungufu ya ushiriki wa mtoto .........................................................110
9.4 Ushiriki wa watoto siku za nyuma, sasa, na siku zijazo.................................112
9.5 Wajibu na majukumu katika ushiriki wa mtoto ..................................................114
9.6 Kuandaa mpango wa utekelezaji unaohusu ushiriki wa watoto ...........116
9.7 Kujadili na watu wazima kuhusu haki na ulinzi wa watoto ...............................117

**Sura ya 10: Tunawezaje kucheza na kuimarisha nguvu?.......................119**

**Sura ya 11: Orodha ya kukagulia ushiriki wa watoto .................................. 122**
Orodha ya kukagulia kwa ajili ya watoto .123
Orodha ya kukagulia kwa ajili ya watu wazima .......................................................123

**Marejeo .................................................125**

# Utangulizi

Lengo la kielekezi hiki ni kubainisha seti sahili ya maelekezo ya mwongozo wa utekelezaji na mbinu za uwezeshaji katika kuwasiliana na watoto kwa kutumia njia shirikishi. Walengwa wa Kielekezi hiki ni mashirika, asasi na watu binafsi wa Tanzania wenye lengo la kusaidia watoto katika kuyakabili masuala yao ya msingi kupitia, kwa mfano, mambo mbalimbali yanayofanyika shuleni, katika mabaraza, kamati, vyama vya wanafunzi, au katika makundi mengine yasiyo rasmi

Kielekezi hiki kimeandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, jinsia na watoto, kwa msaada wa kiutaalamu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa kushauriana na wadau mbalimbali wanaojishughulisha na masuala ya ushiriki wa watoto nchini Tanzania (soma sehemu ya shukrani). Kielekezi hiki kinajumuisha; utangulizi mfupi kuhusu dhana ya ushiriki wa mtoto; hali ya ushiriki wa mtoto chini Tanzania; seti ya maelekezo sahili kwa ajili ya uwezeshaji wa shughuli zinazoshirikisha mtoto na; vielekezi halisi 48 kwa ajili ya uwezeshaji wa shughuli za ushiriki wa mtoto nchini Tanzania. Ili kupata taarifa zaidi na za kina kuhusu *nadharia* ya ushiriki wa mtoto tafadhali soma vitabu vilivyoorodheshwa katika kurasa za mwisho za kielekezi hiki.

**Ushiriki wa mtoto ni nini?**
Ushiriki wa mtoto unahusu kuwapatia watoto fursa ya kushiriki katika maamuzi pamoja na kutoa mawazo yao kuhusu masuala yanayogusa maisha yao. Ushiriki wa mtoto unatokea katika mazingira ya aina zote - nyumbani, katika jamii yake na katika ngazi za taifa na kimataifa.

Ushiriki wa mtoto hauna maana ya kumpatia mtoto majukumu kamili ya kufanya na kusimamia maamuzi, bali humaanisha kuwapatia watoto nafasi ya kushiriki pamoja na kuwahimiza waweze kuchangia mawazo yao. Jukumu la watu wazima katika ushiriki wa mtoto ni kuwapatia watoto taarifa za masuala yanayohusu maisha yao, kuwawezesha watoto kufikia maamuzi kuhusu masuala hayo, kuwashirikisha watoto katika shughuli na michakato inayowahusu , kusikiliza maoni yao, na ikibidi kuwaongoza.

Kuwaamulia watoto nini wafanye na nini wasifanye bila kuwapatia nafasi ya kufahamu au kujadili sababu za maamuzi hayo sio ushiriki wa mtoto – wala ushiriki wa mtoto sio kwa maneno tu – kwa mfano kuwashirikisha watoto kwenye mikutano bila ya kuwaandaa kuhusu nini cha kufanya na bila kuwapatia nafasi ya kushiriki katika majadiliano.

**Kwa nini ushiriki wa mtoto ni muhimu?**
Ushiriki wa mtoto ni haki ya kila mtoto. Ni moja ya nguzo nne za Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto, na una msingi wake katika mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto. Serikali ya Tanzania imeridhia (mikataba yote miwili) . Aidha, Hapa Tanzania, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 iliyofanyiwa marekebisho, ushiriki wa mtoto umetambuliwa kama haki na umerejelewa katika Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

Pamoja ya kwamba ni haki, ushiriki wa mtoto una manufaa mengine mengi. Hapa chini tumeorodhesha manufaa matatu muhimu miongoni mwa mengine:

- Ushiriki wa mtoto humpatia mtoto nafasi ya kujifunza. Hukuza stadi na uwezo wa watoto pamoja na kuwajengea hali ya kujitambua, maendeleo na kujiamini.

- Ushiriki wa mtoto huchangia katika maendeleo ya familia, jamii na taifa kwa jumla. Mawazo na mitazamo ya watoto hutofautiana na wakati mwingine huwa mizuri kuliko ya watu wazima. Vile vile watoto wanapopewa majukumu huyatekeleza vizuri zaidi , wakaboresha

kwa mfano mahusiano katika familia ,jamii au katika ufanisi wa shule.

- Ushiriki wa mtoto unaunga mkono maendeleo ya demokrasia. Ushiriki huimarisha uwezo wa watoto wa kuelewa demokrasia na haki za binadamu, na kuwatia moyo wa kushiriki katika mchakato wa demokrasia na kuuheshimu.

**Aina za ushiriki wa mtoto**
Ushiriki wa mtoto uko wa aina tofauti. Ili kurahisisha, tutazungumzia aina 3 za ushiriki wa mtoto. Endapo utapenda kujisomea zaidi kuhusu nadharia na aina za ushiriki wa mtoto, tafadhali soma vitabu vilivyoorodheshwa katika marejeo.

Katika *mashauriano yanayoongozwa na mtu mzima*, watoto huhusishwa katika maamuzi, na kupewa nafasi ya kutoa maoni na kueleza hisia zao, hata hivyo uamuzi wa mwisho hutolewa na watu wazima. Njia ya mashauriano ya kuongozwa na mtu mzima ni njia nzuri endapo lengo ni kubaini maoni ya watoto kuhusu maamuzi, ambayo hatimaye yatafanywa na watu wazima – kwa mfano maamuzi yanayofanywa na serikali ya mtaa, bodi za shule n.k.

Katika *ushiriki unaoanzia kwa watu wazima*, watu wazima hubuni kitu cha kufanya lakini watoto hushirikishwa katika upangaji na utekelezaji wake, na maamuzi hufanyika kwa pamoja. Mkabala huu ndio unaotumika katika shughuli nyingi zinazoshirikisha watoto, hususan katika hatua za mwanzo za ushiriki .

Katika *ushiriki unaoanzia kwa watoto*, watoto wenyewe hubainisha jambo la kushughulikiwa na huanzisha na kusimamia shughuli zenyewe. Maamuzi huwashirikisha watu wazima, lakini wao hushiriki kama wawezeshaji tu na wala sio waongozaji. Mkabala huu ni mzuri kwa watoto wakubwa ambao tayari wana uzoefu katika masuala ya ushiriki .

Aina ya ushiriki wa watoto itakayotumika katika mazingira tofautitofauti itategemea: suala linaloshughulikiwa, uwezo wa watoto na mkabala unaotumiwa na watu wazima wanaoshughulikia ushiriki wa watoto.

**Ushiriki wa mtoto katika Tanzania**
Serikali ya Tanzania imeridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto mwaka 1991, na Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto mwaka 2003. Mwaka 1996 Tanzania ilitunga Sera ya Maendeleo ya Mtoto, ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2008. Sera hiyo inasisitiza kuhusu haki za mtoto za kuishi na kukua, kupewa ulinzi na kushirikishwa. Sheria ya Mtoto iliyopitishwa na Bunge la Tanzania Novemba 2009, inaweka msingi wa kitaifa wa ulinzi na upatikanaji wa haki za mtoto. Miongoni mwa haki zilizobainishwa katika sheria hiyo ni ile ya mtoto ya kutoa maoni na kushirikishwa katika maamuzi.

Mwaka 2002, serikali ya Tanzania ilianzisha muundo wa Baraza la watoto ambao lengo lake ni kuwakilisha maoni ya watoto katika ngazi za kimkoa na kitaifa. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto nayo pia imejumuisha mashauriano na watoto kama sifa ya msingi katika mchakato wa kitaifa wa upitiaji na ufuatiliaji wa haki za mtoto.

Pamoja na kwamba sasa hivi kuna sera na sheria kadhaa zinazohimiza ushiriki wa mtoto, bado masuala ya watoto hayajapewa nafasi yanayostahili katika Tanzania. Kwa jumla, kaida za mafunzo na malezi ,katika Tanzania zina mwelekeo wa kiimla, zikitetea mamlaka ya wanaume na ya kimsonge katika familia na jamii. Utafiti wa "Maoni ya Watoto 2007" kuhusu mtazamo wa watoto wa Tanzania kuhusu elimu na wajibu wao katika jamii, ulithibitisha jambo hili, ukibainisha kwamba ujifunzaji mashuleni ni wa kutoka kwa mwalimu kwenda kwa wanafunzi na sio shirikishi, na adhabu ya viboko hutumika sana. Wakati ambapo watoto wengi wanakiri kuwa wanaamini

kwa njia moja au nyingine kwamba wanasikilizwa katika familia, bado kwa kiasi kikubwa hakuna utaratibu unaoeleweka wa ushiriki wa watoto pamoja na usikilizwaji wa maoni yao.

Wadau kadhaa, ikiwa ni pamoja na watumishi wa serikali na wanaharakati wa vyama vya kiraia (kwa mfano Save the Children, REPSSI, GNRC, World Vision, PLAN, Children's Dignity Forum na wengine) wamo katika harakati za kuanzisha ushiriki bora wa mtoto katika mazingira mbalimbali nchini Tanzania (klabu za amani, kamati za watoto, mabaraza ya watoto, mabaraza ya shule n.k.), wakiongozwa na miongozo iliyopo ya kitaifa au kimataifa pamoja na vielekezi mbalimbali vya ushiriki . Licha ya juhudi hizo bado sehemu kubwa ya shughuli za ushiriki wa mtoto hutendeka kama tukio la mara moja la mfano tu. Wakati wa mchakato wa mashauriano ya maandalizi ya kielekezi hiki, wadau waliweka bayana kwamba kumekuwa na tatizo kubwa la kutoeleweka vyema kwa dhana nzima ya ushiriki wa mtoto miongoni mwa watu wazima. Mojawapo ya sababu zilizotajwa inahusiana na hofu ya jumla kwamba pangeweza kutokea mvurugiko wa maadili ya kitamaduni na kijamii, kutokana na watu wengi wazima kuutazama ushiriki wa mtoto kama uigaji wa mambo ya kimagharibi na mawazo ya kigeni. Watu wana hofu kwamba ushiriki wa mtoto utawajengea watoto kiburi na kuwaharibu kabisa kitabia. Hata hivyo hakuna ushahidi wowote kwamba ushiriki wa mtoto husababisha kuharibika kwa tabia.

Changamoto nyingine kubwa iliyobainishwa na wadau ilihusiana na uwezo mdogo miongoni mwa watoto wa kushiriki katika mchakato wa ushiriki kwa vile watoto wengi hawajazoea utamaduni wa kusikilizwa. Uwezo wa watoto wa kushiriki katika mchakato wa ushiriki unatofautiana sana baina ya maeneo katika nchi, hali ya jumla ikionyesha kwamba watoto wa maeneo ya mijini wana uwezo wa kujieleza zaidi na wanajiamini zaidi kuliko watoto wa maeneo ya vijijini ambao hawapati nafasi kubwa ya kusikiliza vyombo vya habari na kusoma magazeti pamoja na kushiriki katika shughuli za maendeleo. Aidha, ubaguzi, unyanyapaa na mila na imani zinazohusishwa na makundi ya watoto, k.m. wasichana, watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi na wanaokabiliwa na upungufu fulani, kwa mfano watoto walioko katika umaskini wa kutupwa, walemavu, wasioko shuleni n.k. ni kikwazo cha kuweko kwa ushiriki unaostahili wa watoto wote.

**Namna ya kufanikisha shughuli za ushiriki wa mtoto**

Vyama na wakala kadhaa wameandaa miongozo kuhusu namna ya kushughulikia suala la ushiriki wa mtoto. Baadhi ya masuala ya msingi katika miongozo hiyo yamefafanuliwa hapa chini. Ili kupata maelezo ya kina soma marejeo yaliyoambatishwa .

<u>Hakikisha kwamba ushiriki wa mtoto sio wa kulazimishwa na unamlinda mtoto.</u>
Ushiriki wa mtoto hauna budi kuwa wa hiari. Watoto waeleweshwe vyema kuhusu mchakato na shughuli zinazohusika na wafahamishwe kuhusu haki pamoja na wajibu wao. Watoto wote wanaohusika katika ushiriki wapewe muda wa kutafakari kuhusu ushiriki wao na waulizwe kama wanaukubali wenyewe bila kulazimishwa. Hakikisha kuwa hatua zimechukuliwa kudhibiti kabisa hatari zozote na kuzuia uonevu.

<u>Fahamu hali na vipaumbele vya watoto</u>
Mwanzo kabisa wa kumhusisha mtoto katika ushiriki kwenye maamuzi ni kubaini uzoefu wa mtoto mwenyewe, hali na vipaumbele vyake. Chukua muda kuwafahamu vizuri watoto husika pamoja na matarajio yao kabla ya kuanza kuwashirikisha kwenye shughuli.

Hakikisha kwamba ushiriki wa mtoto umezingatia uwezo wa mtoto na mazingira yao ya kijamii na kiutamaduni.
Watoto wana uwezo tofautitofauti kulingana na umri na maisha yao ya nyuma. Zingatia jambo hili kila unapotaka kushirikisha watoto kwenye shughuli yeyote. Tafuta uwiano baina ya (a) kuheshimu uwezo wa watoto na kuwahamasisha kujijengea uwezo wa aina hiyo, na (b) kutowakatisha tama ya kushirikishwa kwa kuwaingiza katika shughuli ambazo zinazidi uwezo wao.

Ushiriki wa watoto hauna budi pia kuzingatia kaida za kijamii na kiutamaduni za jamii ya mtoto. Hata hivyo, zingatia kwamba utamaduni ni kitu kinachobadilika wakati wote na kwamba, hakuna utamaduni wa aina moja tu katika jamii. Hivyo basi kuheshimu utamaduni hakumaanishi kusikiliza tu maoni ya watu wazima, bali kuna maana ya kushirikisha makundi mbalimbali kwenye jamii katika michakato na majadiliano kuhusu ushiriki wa mtoto, kusikiliza na kuheshimu maoni ya watu wote.

Pambana na vikwazo dhidi ya ushiriki na hakikisha hakuna ubaguzi katika ushiriki
Unapowezesha shughuli na michakato wa ushiriki wa mtoto; zingatia changamoto na vikwazo dhidi ya ushiriki ambavyo unaweza kupambana navyo, na tafakari namna ya kuviondosha. Watoto wote wana uwezo wa kushirikishwa endapo utakuwa umechagua mkabala sahihi.

Kuwa mwezeshaji mvumilivu, mshaurika, msikizi na mtambuzi
Kuwezesha mchakato wa ushiriki wa watoto (na wa watu wazima) huhitaji mwezeshaji mwenye uelewa mkubwa. Kuwa mvumilivu na tayari kubadilika pale mambo yanapokwenda kinyume na mipango au matarajio yako, hakikisha kwamba unaheshimu maoni ya watoto pamoja na kutambua michango yao ya mawazo, na kamwe usitawale wala kulazimisha majadiliano. Kuwa tayari kusikiliza na kujifunza, na usiogope kukiri kwamba yapo mambo ambayo huyafahamu. Aidha, heshimu mahitaji ya watoto k.m. kuhusiana na wakati wa kufanya vikao, aina ya shughuli za kufanya, umuhimu wa mafunzo n.k.

Hakikisha kuweko kwa mazingira rafiki kwa watoto
Ushiriki wa mtoto huwa wa ufanisi endapo watoto watajisikia huru na furaha. Unaweza kuyafanya mazingira yawe ya kuvutia kwa watoto kwa kuchagua mahali pa kufanyia mkutano ambapo panapendwa na panafikika kwa watoto wote, kutenga muda wa kutosha wa kukutana, kuwapatia watoto taarifa wanazopaswa kuwa nazo kabla na wakati wa utekelezaji wa shughuli, na kuhakikisha kwamba maelezo na maelekezo yanatolewa kwa lugha rahisi itakayoeleweka kwa kila mtoto. Mwisho, sikiliza maoni ya watoto kuhusu mambo ambayo huyafanya mazingira yawe katika hali ya kuwavutia

Tambua kwamba ushiriki wa mtoto ni suala la maisha ya kila siku ya mtoto na wala sio tukio la kutendeka mara moja tu.
Ushiriki wa watoto hauna budi kuwa sehemu ya shughuli zao za kila siku na wala sio kufanyika tu katika matukio maalumu au katika mazingira yasiyooana na maisha yao ya kila siku. Maana yake hapa ni kwamba ushiriki wa mtoto hauna budi kuingizwa katika asasi muhimu zinazosimamia maisha ya mtoto, kwa mfano, shule.

**Vielekezi**
Vielekezi vilivyobainishwa katika kitabu hiki vimeteuliwa kwa kuzingatia mbinu mbalimbali za ushiriki wa mtoto kwa ajili ya ujifunzaji na ukuaji. Mbinu za ushiriki zina lengo la kuhusisha kikamilifu washiriki katika ujifunzaji, utambuzi, uchambuzi, upangaji na ufanyaji tathmini. Zinapotumika vizuri, mbinu hizo husaidia katika kujenga hisia za umiliki miongoni mwa washiriki na imani kwamba mambo yao yanathaminiwa.

Vielekezi hivi vimeandaliwa kwa kuwalenga watoto wa miaka 12-18 na baadhi ya vielekezi vinaweza pia kutumika kwa watoto wa umri mdogo zaidi. Baadhi pia vinaweza kutumika kwa ajili ya vijana wa umri wa zaidi ya miaka 18 na/au watu wazima.

Kielekezi hiki kimeandaliwa kwa kutilia manani kwamba ushiriki wa mtoto unahusu mchakato mzima wa maisha ya mtoto wala hauhusu tukio la siku moja tu. Hivyo vielekezi husika vimeandaliwa katika utaratibu wa Sura zikiashiria ngazi tofautitofauti katika mchakato mzima wa ushiriki wa mtoto – kuanza (sura ya 1), kujenga timu (sura ya 2), kubainisha masuala muhimu yanayowahusu watoto (sura ya 3), kupanga malengo (sura ya 4), kupanga kazi (sura ya 5), kutekeleza kazi (sura ya 6), kazi za ufuatiliaji na tathmini (sura ya 7) na utunzaji kumbukumbu (sura ya 8). Kielekezi hiki pia kina sura kuhusu namna ya kuimarisha mchango wa watu wazima katika ushiriki wa mtoto kwenye jamii (sura ya 9) na baadhi ya maoni kwa ajili ya michezo na viimarishi nguvu (sura ya 10).

Katika mwanzo wa kila sura, utabaini mapendekezo kadhaa ya miongozo ya kuzingatia pale unapokuwa ukiongoza shughuli, na fafanuzi za baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika kwenye zana husika.

Katika sehemu ya mwisho ya Kielekezi hiki utakuta orodha ya mambo muhimu ya kuzingatiwa katika ushiriki wa mtoto ambayo yanaweza kukusaidia kabla ya kuanzisha shughuli za ushiriki wa mtoto, na baadaye ukayatumia katika kujitathmini kwa lengo la kubaini kama kile unachofanya ndicho au la. Tumeweka pia orodha ya mambo muhimu ya kuzingatiwa na watoto. Mwisho kuna orodha ya marejeo ambayo unaweza kujisomea zaidi kuhusu ushiriki wa mtoto.

**Namna ya kutumia kitabu hiki**

Watumiaji wa kitabu hiki wanaweza kuwa:

- Waalimu wa watoto katika shule au katika vilabu vya watoto
- Wafanyakazi wa kudumu na wa kujitolea kutoka AZISE wanaofanya kazi katika vilabu, makundi au kamati za watoto
- Viongozi wa Serikali ya Mtaa au watumishi wa kujitolea wa masuala ya jamii wanaofanya kazi katika mabaraza ya watoto katika ngazi za kata, wilaya au mikoa.
- Mtu yeyote binafsi, kijana au mtu mzima, mwenye mapenzi katika shughuli za watoto katika jamii yake.


Tunapendekeza kwamba:

- Pitia kitabu hiki kwa haraka ili uweze kuufahamu muundo wake.
- Chagua sura ambayo inaendana na kazi yako unayoifanya
- Tumia kielekezi kilichobainishwa katika kitabu hiki kama mwongozo, lakini zingatia mazingira halisi unakofanyia shughuli yako.
- Buni au shirikiana na watoto kubuni vielekezi vyenu wenyewe.

Namna utakavyotumia vielekezi hivi itategemea mazingira unakofanyia shughuli yako, aina ya kundi lako la watoto na mada ya shughuli yako. Hivyo vielekezi vilivyobainishwa humu havina budi kutumiwa kwa kuzingatia hali halisi na ubunifu na kulingana na matarajio, mahitaji na muktadha mahususi wa kundi la watoto – vimekusudiwa vitumike kama mwongozo tu na wala sio kama maneno ya msahafu au biblia.

# Sura ya 1: Tunawezaje kuunda au kuimarisha kikundi cha watoto?






Sura hii inaelezea baadhi ya vielekezi vinavyotumika kusaidia watoto katika kuunda kikundi cha watoto, kwa mfano, klabu, kikundi, baraza au kamati. Vikundi na vyama vingi vya watoto huanzishwa na watu wazima. Changamoto hapa ni kuwamilikisha watoto kwa kiasi kikubwa vikundi hivyo mapema kadiri inavyowezekana.

**Miongozo:**

- Fanya miundo na masharti ya kikundi kuwa mepesi – hakuna sababu ya kupoteza nguvu na mawazo kwa kuwa na urasimu mkubwa.
- Hakikisha kwamba masharti yanatekelezeka – yanatakiwa yawe mepesi ili watoto waweze kukutana mara kwa mara.
- Changia mawazo na rahisisha michakato mbalimbali inayofanyika lakini waachie watoto wenyewe majukumu mengi kadiri inavyowezekana.
- Weka msisitizo katika kuendeleza ujuzi kwa watoto wote na sio tu kwa viongozi wachache, wawezeshe watoto waliokosa fursa.
- Kuwa makini na masuala ya ujumuishi tangu mwanzoni. Hakikisha kwamba mambo yote yanayofanyika yanawafikia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, waliokosa fursa, na wote wanapewa nafasi ya kushiriki kikamilifu na kuchangia mawazo yao. Kama kwenye kikundi kuna watoto wasioona, tumia utaratibu ambao utajumuisha kwa kiasi kikubwa majadiliano kwa njia ya mazungumzo na hakikisha kwamba wanasaidiwa, kwa mfano, wakati wa kupiga kura au kuandika maoni. Na kama kwenye kikundi kuna watoto wenye matatizo ya kusikia, andaa utaratibu wa kupata msaada wa tafsiri ya lugha ya alama au tumia maandishi au michoro.

**Baadhi ya mambo ya kuzingatia kwa ajili ya kuitisha mkutano:**


- Buni utaratibu wako binafsi wa kufungua mkutano (kwa mfano, wimbo maalum au mchezo)
- Panga ratiba ya muda
- Shirikisha watoto katika kuandaa ajenda
- Shirikisha watoto katika kuamua nani atakuwa na jukumu gani wakati wa mkutano
- Hakikisha kwamba kila mmoja anapata nafasi ya kuongea
- Waache watoto wafanye kazi katika makundi madogo madogo ili kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata nafasi ya kusikilizwa
- Fanya michezo midogo midogo na vitendo vingine vitakavyowaongezea nguvu watoto
- Onyesha kupendezwa na mawasilisho na michango wanayotoa watoto, kwa mfano kwa kupiga makofi.

**Kamusi**

*Wajibu*: Vitendo na kazi zitolewazo au zinazotegemewa kufanyika kutoka kwa mtu binafsi au kikundi.

*Ujumuishi*: Hakikisha kila mtoto anashiriki kwenye maamuzi au shughuli za kikundi bila kujali umri, jinsia, rangi, kabila, afya, dini, familia anayotoka, tabaka, ulemavu, ujinsi n.k.

## 1.1 Kujadiliana na watoto kuhusu ushiriki wa mtoto



**Lengo:** Kama kikundi cha watoto kimeundwa kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa mtoto, hatua nzuri ya kuanzia inaweza kuwa kujadili ushiriki wa mtoto katika ufanyaji maamuzi kwenye jamii. Lengo la kitendo hiki ni kuongeza uelewa na fikra za ushiriki wa mtoto miongoni mwa watoto.

**Ukubwa wa kikundi.** Kama kikundi ni kikubwa, kigawe katika vikundi vidogovidogo vya watu 6-8.

**Vifaa.** Vifaa tofauti vya asili vinavyopatikana katika mazingira husika (kwa mfano, vijiti, majani, mawe ya aina tofauti, au vitu vilivyokwisha tumika), karatasi na kalamu

**Muda:** Takribani saa 2

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wa kila kikundi washirikiane kutengeneza angalau mazingira ya aina tatu ambayo ni muhimu kwa maisha ya watoto, kwa kutumia vifaa vya asili vinavyopatikana eneo hilo. Mazingira yanaweza kuwa ya nyumbani, shuleni, serikali ya mtaa, na sehemu watoto wanakofanyia shughuli zao, lakini waache watunge mawazo yao wenyewe.
2) Endesha mjadala mfupi miongoni mwa washiriki wote kuhusu maana ya ushiriki . Tilia mkazo katika ushiriki ukihusianisha ufanyaji maamuzi, na siyo tu kushirikishwa kwenye shughuli mbalimbali. Halafu yaambie makundi yajadili mambo yafuatayo:
   - Ni kwa kiasi gani unafikiri watoto walihusishwa kwenye ufanyaji maamuzi katika mazingira ya aina mbalimbali hapo zamani? Elezea nini maana ya zamani – kwa mfano, wakati wazazi au mababu na mabibi walipokuwa wadogo. Kiwango cha kuhusishwa kwa watoto katika ufanyaji maamuzi kimeonyeshwa kwa kutoa alama kuanzia, kwa mfano, 1 mpaka 5. Hili linaweza kufanyika kwa kuweka mawe madogo madogo au vitu vingine kwenye safu kutokana na aina ya mazingira, jiwe moja likimaanisha kiwango kidogo cha uhusishwaji, mawe matano yakimaanisha kiwango kikubwa zaidi cha uhusishwaji.
   - Ni kwa kiasi gani watoto wanashirikishwa kwenye ufanyaji maamuzi katika mazingira tofauti hivi leo? Tengeneza safu nyingine karibu na ya kwanza na onyesha kiwango cha ushiriki wa watoto kwenye kufanya maamuzi kwa kutumia alama walizopata.
   - Ni kwa kiasi gani unafikiri watoto wanatakiwa wahusishwe katika ufanyaji maamuzi siku zijazo? Onyesha kiwango cha ushiriki wa watoto katika ufanyaji wa maamuzi kwa kutumia alama walizopata kwenye safu ya tatu.

3) Ruhusu vikundi viwasilishe kazi zao.

**Tafakari na majadiliano**

Jadili dondoo zote au baadhi kati ya hizi zifuatazo:

- Kama kuna utofauti kati ya kiwango cha kufanya maamuzi hapo zamani na hivi sasa, Je, ni nini kimesababisha utofauti huu?

- Ni changamoto zipi zinazojitokeza katika ushiriki  wa mtoto kwenye ufanyaji maamuzi katika jumuiya yetu kwa hivi sasa?
- Kwa nini unataka uone kiwango kikubwa au kidogo cha ushiriki  wa mtoto katika mazingira tofauti siku zijazo?
- Nini kinaweza kufanyika ili kuongeza ushiriki  wa mtoto katika kufanya maamuzi?
- Alama zingekuwaje kama ungekuwa unaongelea wasichana tu? Na kama ungekuwa unaongelea wavulana tu? Je kuna tofauti kati ya idadi ya wasichana na wavulana wanaoshrikishwa katika kufanya maamuzi? Kama ni ndiyo, kwa nini? Je ni haki?

Waambie watoto wazungumze na watu wazima kwenye jumuiya, kwa mfano, wazazi na wazee kuhusu suala hili ili kujua zaidi jinsi mambo yalivyobadilika. Taarifa hizi zinaweza kutolewa kwenye mkutano ujao wa kikundi.

**Utofauti:**
Unaweza kuwaambia washiriki wafanye utenganishi wa vikundi tofauti vya watoto, kwa mfano, vikundi vya umri fulani, wavulana na wasichana, masikini na matajiri, walemavu n.k.
Kama kwenye kikundi kuna watoto wasioona , hakikisha wanapewa nafasi ya kushiriki kwenye mijadala.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Nakili mifano na alama kwenye kipande cha karatasi na hifadhi michoro kwenye mafaili ya kikundi. Inaweza kupitiwa kwenye hatua zinazofuata kwa ajili ya watoto kujadili kama wamebadilisha maoni yao kuhusu masuala fulani au inaonekana wanazidi kukaribia zaidi malengo yao ya ushiriki  wa mtoto hapo baadaye.

## 1.2 Kukubaliana kuhusu/shughuli za kikundi cha watoto

**Lengo:** Wakati wa kuunda kikundi rasmi cha watoto watakaoshirikiana kwa kipindi fulani, ni wazo zuri kuanza kwa kuwashirikisha wanachama wote wa kikundi katika kufikiria na kukubaliana kuhusu wajibu wa kikundi.

**Ukubwa wa kikundi:** Watu 8-30

**Vifaa:** Kalamu na karatasi kwa kila mtu. Flipchati na kalamu au ubao na chaki.

**Muda:** Takriban saa 2

**Kazi:**

1) Endesha mjadala mfupi miongoni mwa washiriki kuhusu maana ya "wajibu" (tafsiri moja inaweza kuwa ni vitendo na shughuli walizopewa au kutarajiwa na kikundi).

2) Mwambie kila mtu afikirie kuhusu nini kinapaswa kuwa wajibu wa kikundi cha watoto, halafu aandike mapendekezo matatu. Hili likishafanyika, waambie watoto wakae pamoja wawili wawili, wajadili mapendekezo na kukubaliana kuhusu masuala matatu muhimu kuliko yote. Vikutanishe vikundi viwili kwa pamoja (4 kwa 4) halafu waache wakubaliane tena kuhusu masuala matatu muhimu kuliko yote. Vikutanishe tena pamoja vikundi kwa mara nyingine (8 kwa 8) halafu waache wakubaliane kuhusu masuala matatu. Endelea na mchakato huu mpaka utakapowakutanisha watoto wote na wakakubaliana kuhusu majukumu matatu muhimu kuliko yote ya kikundi cha watoto. Waambie wafanye haya mambo kama wao ndio wahusika wakuu (mfano "kikundi kitafanya kazi kwa kuheshimu haki za watoto katika jumuiya" au "kikundi kitaainisha masuala ya watoto").

3) **Tafakari na majadiliano:**
   Jadili kwa kina zaidi kuhusu majukumu tofauti waliyokubaliana – sentensi hizi zinamaanisha nini hasa.

**Utofauti:**
Kama watoto hawawezi kuandika, waambie waonyeshe majukumu haya kwa mchoro. Kama kuna watoto wasioona kwenye kikundi waruhusu wawasilishe wajibu wao kwa mdomo.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Hifadhi maelezo ya wajibu kwenye mafaili ya kikundi cha mtoto au yabandike ukutani.

# 1.3 Kuweka kanuni za kikundi

**Lengo:** Kwa ujumla vikundi vinapaswa viwe na kanuni za mawasiliano ili ili viweze  kufanya kazi kwa ufanisi. Kanuni za kikundi hufanya kazi vizuri zaidi kama wanachama wote wa kikundi watakuwa wameshiriki katika kuziandaa na kama wataziona kanuni hizo kuwa ni zao.

Lengo la kielekezi hiki ni kukiwezesha kikundi kujiwekea kanuni zake chenyewe kwa ajili ya kazi kinazofanya.

**Ukubwa wa kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa, kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watu 6 – 8.

**Vifaa:** Kalamu na vipande vingi vya karatasi/kadi (kwa mfano, ukubwa wa A5).

**Muda:** Takriban saa 1

**Kazi:**

1) Endesha mjadala mfupi miongoni mwa washiriki kuhusu aina gani ya kanuni zinahitajika katika kuongoza kikundi. Orodhesha. (Mifano inaweza kuwa mifumo ya utawala/uongozi, taratibu za uchaguzi, kanuni za uchaguzi, jinsi ya kuitisha kikao, jinsi ya kufanya mkutano, jinsi ya kufanya maamuzi, ufuataji wa maadili).

| Aina ya uongozi | Upatikanaji wa viongozi | Jinsi ya kufanya maamuzi ya kikundi | Maadili ya wanakikundi | Jinsi ya kufanya mkutano |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

2) Waambie washiriki wa kila kikundi wajadili na kukubaliana kuhusu kanuni zilizopendekezwa. Hamasisha zipatikane kanuni nyepesi lakini zenye ufanisi. Kila kanuni itatakiwa liandikwe kwenye kipande cha karatasi (kanuni moja kwenye kipande kimoja cha karatasi)

3) Wakusanye pamoja washiriki wote kwenye duara na tandaza aridhini kanuni zote zilizoandikwa kwenye karatasi. Waambie washiriki waainishe kanuni kulingana na masuala mbalimbali. Jadili uwezekano mbalimbali katika kila aina ya kanuni, kama kuna ulazima ziunde upya na mkubaliane ipi iwe kanuni  kuu kwa ajili ya kikundi kwa siku zijazo. Andika kanuni zilizokubaliwa kwenye karatasi lingine tofauti.

**Tafakari na majadiliano:**
Jadili kwa nini ni muhimu kuwa na kanuni wakati wa kufanya kazi kwa pamoja kwenye kikundi.
Jadili ikiwa kikundi kinahitaji kanuni ili kuhakikisha kwamba kila mtu anapata fursa ya kushiriki kikamilifu. Hizi zinaweza kuwa ni kanuni kuhusiana na sehemu ya kufanyia mkutano (inayoweza kupatikana kwa urahisi na salama kwa kila mtu), ushiriki wa watoto wenye matatizo ya kusikia, maadili ya kuzingatia kwa ajili ya ushirikiano kati ya wavulana na wasichana, n.k.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:** Hifadhi kanuni zilizokubaliwa kwenye mafaili ya kikundi cha watoto au yabandike ukutani. Amua lini masharti haya yapitiwe upya na kufanyiwa marekebisho.

## 1.4 Mchezo kuhusu  uchaguzi huru na wa haki

**Lengo:** Vikundi vingi vya watoto hufanya chaguzi ili kuchagua mwenyekiti, na pengine makamu wake, katibu na mhazini. Watoto wana mazoea ya kuchagua watoto ambao ni wawazi na wababe kuwa viongozi (mara nyingi vijana wenye umri mkubwa zaidi yao). Mchezo huu huwahamasisha watoto kutafakari kuhusu mahusiano ya uongozi na fursa za michakato ya uchaguzi iliyo ya haki zaidi.

**Kikundi:** Watu 8-30

**Vifaa:** Mawe madogo madogo, pipi au vitu vingine.

**Muda:** Saa 1.

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wote wakae mduara. Weka vitu vidogo vidogo katikati ya mduara huu (idadi vitu hivi inatakiwa iwe takriban theluthi moja ya washiriki au chini ya hapo). Fafanua kwamba vifaa havitatosha kwa kila mtu, kwa hiyo yeyote atakayekuwa wa kwanza kuvipata avichukue. Waambie washiriki wachukue vitu hivi. Hamasisha washiriki kutafakari nani alipata pipi na kwa nini. Je mchakato huu ulikuwa ni wa haki? Kwa nini/kwa nini hapana?

2) Katika mzunguko wa pili waambie washiriki kuwa mtu anayeishi karibu na kituo cha jamii abaki katikati ya duara. Watake washiriki wote ambao wanaishi kwenye maeneo ya jamii ambayo yamejitenga (kwa mfano, mbali na shule, kituo cha afya, n.k) kukaa mbali (nje ya mduara). Kwa mara nyingine tena weka vifaa vidogo vidogo katikati ya duara halafu waambie watoto wavichukue. Waulize watoto kama ugawaji huu ni wa haki. Waulize ikiwa mfano huu unawakilisha ukweli wowote wa uzoefu wao katika jamii. Je, kuna baadhi ya watoto wanaopata fursa kubwa zaidi ya kwenda shule na kupata huduma nyingine za kijamii – kama ndivyo, ni watoto gani na kwa nini?

3) Katika mzunguko wa mwisho waambie kwamba kuna vifaa ‘X’ tu. Eleza kwamba ili mchakato wa uchaguzi uwe wa haki, watoto na vijana wadogo kutoka katika familia na umri tofauti, pamoja na wasichana na wavulana wanatakiwa wapate fursa ya kuwakilisha wenzao. Kwenye kundi la watoto fulani na vijana wadogo kutoka kwenye makundi yanayotengwa zaidi kwenye jamii (pamoja na watoto wenye ulemavu) wanatakiwa wapewe haki sawa ya kuchaguliwa. Hivyo, hamasisha watoto waamue ni vikundi gani vya watoto (kwa mfano, wavulana na wasichana; watoto wadogo na wenye umri mkubwa zaidi; watoto wanaosoma na ‘wasiosoma’ shule; watoto wenye ulemavu) wanatakiwa kuwakilishwa.

**Tafakari na majadiliano:**
Jadili kuhusu uchaguzi na tengeneza mwongozo ili kuhakikisha chaguzi jumuishi na za haki.

**Uhifadhi:**
Andika miongozo iliyokubaliwa, iweke kwenye mafaili ya kikundi na itumie wakati wa kufanya chaguzi.

## 1.5 Mchezo kuhusu uongozi

**Lengo:** Mchezo huu huhamasisha watoto kutafakari aina tofauti za uongozi, faida na hasara zake, na kujadili kuhusu uongozi wa kidemokrasia.

**Ukubwa wa kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa, kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watu 6-8.

**Vifaa:** Vitambaa vya kufunga machoni kwa ajili ya washiriki wote. Kwa njia nyingine, mchezo huu unaweza kufanywa kwa kuwaambia washiriki wafunge macho yao.

**Muda:** Saa 1

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wa kila kikundi wachague kiongozi. Wahamasishe wachague wasichana na wavulana bila ubaguzi. Waambie washiriki wote wafungwe vitambaa machoni au wafunge macho yao. Waite viongozi pembeni na waeleze kwamba inabidi wasaidie vikundi vyao katika kufanya kazi viliyopewa – kwa mfano, kutoka sehemu moja kwenda nyingine (hakikisha kwamba kuna vikwazo kadhaa njiani), kutengeneza sanamu kwa kutumia miili yao, kuchora ardhini kwa pamoja, n.k. Toa muda wa kufanya hiyo kazi (kwa mfano, dakika 10).

**Tafakari na majadiliano:**

1) Kazi inapomalizika, ita washiriki wote (viongozi pamoja na wanachama wa vikundi) ili kuchangia mawazo yao. Ulijisikiaje kuwa mwanachama wa kikundi? Ulijisikiaje kuwa kiongozi? Mambo yapi yalienda vizuri? Na yapi hayakwenda vizuri?

2) Watajie washiriki aina tatu za uongozi:
    - Uongozi wa mabavu – mtu mmoja hutoa amri na wengine kutekeleza
    - Uongozi wa mashauriano – Mtu mmoja hutoa maamuzi lakini husikiliza kwanza maoni ya watu wengine.
    - Uongozi wa kidemokrasia – kila mmoja hushirikishwa katika kufanya maamuzi, kwa mfano, kwa kukubaliana au kupiga kura. Kiongozi ni mhamasishaji na mwongozaji.

3) Jadili:
    - Ni aina zipi za uongozi zilikuwa zikitumika katika mchezo wa funga macho?
    - Ni aina gani ya uongozi tunaotaka itumike kwenye kikundi chetu cha watoto? (pendekeza uongozi wa kidemokrasia)
    - Mbinu za uongozi bora ni zipi? (Orodhesha)we ungependa kuongozwa na mtu mwenye sifa zipi?

- Viongozi wana majukumu gani? Wanachama wana majukumu gani? (Orodhesha)
- Viongozi wanatakiwa kukaa madarakani kwa muda gani?

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Weka orodha ya mbinu za uongozi bora na majukumu yake kwenye mafaili ya kikundi. Tumia kama hatua ya kuanzia mjadala wakati wa uchaguzi au kama kuna migogoro inayohusiana na uongozi kwenye kikundi.

## 1.6 Kufanya maamuzi kama kikundi

**Lengo:** Kwenye vikundi vingi na hasa vikundi vyenye idadi kubwa ya watoto, si kila mtoto hupata nafasi au huwa na ujasiri wa kutosha wa kutoa maoni kwenye mjadala. Vielekezi hivi hutoa mawazo kuhusu namna ya kuwapa washiriki wote nafasi ya kutoa maoni yao. Hali hii huongeza uwezo wa kushiriki katika ufanyaji wa maamuzi.

**Ukubwa kikundi:** watoto 8-30.
**Vifaa:** Kalamu, karatasi, mawe madogo madogo na kadi.

**Kazi:**
**Kupiga kura**
Wakati uamuzi mdogo utakapofanyika, uliza watoto wote kama wanauunga mkono au wanaupinga kwa kunyoosha mikono yao. Pia unaweza kuwaambia waandike kwenye kipande cha karatasi kama wanapinga au wanaunga mkono, kusanya vipande hivyo vya karatasi halafu hesabu kura. Wakati wa uchaguzi waambie wote waandike jina la mtu wanayempigia kura kwenye karatasi.

**Matokeo**
Kama unataka kufahamu ni kwa jinsi gani washiriki wangependa kutoa kipaumbele kati ya mambo kadhaa yanayoweza kufanyika, andika au chora kila jambo kwenye kipande kikubwa cha karatasi au ardhini. Mpe kila mtu idadi kadhaa ya vitu (kwa mfano, mawe 3) na waambie wayaweke kwenye sehemu tatu ambazo wanazipa kipaumbele cha juu zaidi. Andika alama za kila fursa(kila jambo/kipaumbele). Kama kuna ulazima unaweza kufanya mzunguko wa pili na kuwaambia washiriki waonyeshe fursa wanazozipa kipaumbele cha chini zaidi.
Njia ya matokeo pia inaweza kutumika kuuliza maoni ya washiriki katika maelezo tofauti. Andika maelezo tofauti na uwape washiriki vitu vidogo vidogo kulingana na maelezo. Waambie waweke kitu kwenye maelezo ambayo wanakubaliana nayo.

**Kipaumbele**
Kama unataka kujua jinsi washiriki wanavyotoa vipaumbele kwa fursa tofauti, unaweza kuwagawa kwenye vikundi vidogo na kutengeneza kadi yenye michoro au maelezo ya kila fursa. Waambie wajadili na kutoa kipaumbele kwenye kadi kulingana na umuhimu wao (1, 2, 3, 4, n.k.)

**Mijadala katika vikundi vidogo vidogo**

Mijadala katika vikundi vidogo vidogo hutoa nafasi kubwa ya kushiriki kwa washiriki wenye aibu.
Wakati wa mijadala katika vikundi vikubwa unaweza kuwaambia washiriki wachangie maoni yao na mtu aliye karibu yao kwa muda wa dakika 3-5 kabla ya kuruhusu maoni kwenye mjadala wa wote. Kitendo hiki huwafanya watu wawe wajasiri zaidi kutoa maoni yao.


**Fanya mzunguko**

Mwambie kila mtu atoe maoni kuhusu suala lililojadiliwa, mmoja baada ya mwingine. Kumbuka kuwa kitendo hiki kinaweza kuwaogopesha washiriki wenye aibu.

**Maoni au kisanduku cha maswali**

Kama mnajadili masuala magumu, unaweza kuwaambia washiriki watoe maoni yao au maswali kwa kuandika kwenye kipande cha karatasi. Kusanya vipande vyote vya makaratasi kwenye kisanduku au kofia. Vichukue na usome karatasi moja baada ya nyingine kwa sauti halafu waambie washiriki wajadili.

# Sura ya 2: Tunawezaje kuongeza kujiamini na kushirikiana kwenye kikundi cha watoto?




Watoto wengi hawajazoea kusikilizwa mahitaji yao, au kushirikiana kwa pamoja kama kikundi katika kushughulikia masuala yao wenyewe. Vielekezi vya  sura hii vina lengo la kuwafanya watoto wajiamini zaidi, kuimarisha ushirikiano pamoja na mbinu za kufanya kazi kitimu miongoni mwao.

**Miongozo:**

- Hakikisha kila mtoto anajumuishwa. Fahamu hali ya kila mtoto anapoanza kushiriki kwenye kikundi, iwe inahusiana na ulemavu wa aina yoyote ile, hadhi au na kaida za kijamii na kiutamaduni. Hamasisha kila mtoto ashiriki. Kama kuna watoto wasioona kwenye kikundi, anzisha vitendo ambavyo vinajumuisha zaidi majadiliano kwa njia ya mazungumzo na hakikisha wanapata msaada stahili, kwa mfano, wakati wa kupiga kura au kuandika maoni. Ikiwa kuna watoto wenye tatizo la kusikia kwenye kikundi, fanya mpango wa kupata msaada wa lugha ya alama au tumia maandishi na michoro.
- Heshimu haki ya watoto ya kukataa kushiriki. Baadhi ya vitendo vinavyofanyika kwenye kikundi vinaweza kuwaogopesha baadhi ya watoto.


**Kamusi:**

Utambulisho: Utambulisho binafsi ni namna unavyojiona na kujielezea kulingana na tabia yako na kama mwanachama wa vikundi tofauti. Utambulisho wa kikundi ni namna kikundi kinavyojichukulia kulingana na tabia fulani.

*Ujumuishi:* Hakikisha kila mtoto anashiriki kwenye maamuzi au shughuli za kikundi, bila kujali umri, jinsia, kabila/ rangi, afya, dini, familia anayotoka, tabaka, ulemavu, ujinsi, n.k.

*Jinsia:* Humaanisha tofauti za kijamii na kitamaduni kati ya wanaume na wanawake. Utambulisho na majukumu ya kijinsia havitokani na tofauti za kibaiolojia ila hutokana na kaida na mazoea ya kijamii na kiutamaduni.

## 2.1 Mti wa maisha yangu



**Lengo:** Kuelewa na kutafakari utambulisho wa mtu binafsi na wa watu wengine ni msingi muhimu wa kuhakikisha kunakuwepo na ushirikiano. Kielekezi hiki kinalenga kuwahamasisha washiriki wa kikundi kujielezea, kutafakari juu ya maisha yao na utambulisho wao wenyewe, na kuheshimu utambulisho wa wengine.

**Ukubwa wa kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Karatasi, kalamu za rangi au kalamu za kutia alama.

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**

1) Mpatie kila mshiriki karatasi isiyoandikwa chochote na kalamu kadhaa za rangi na waambie wachore mti unaoelezea jinsi walivyo. Wafafanulie vipengele tofauti vinavyoweza kuunda mti huo (kwa mfano, mizizi – wapi ninapotoka, mti wenyewe – utambulisho wangu kwa sasa, matawi na majani kwa juu – ndoto zangu kuhusu maisha yangu ya baadaye).

2) Jadiliana nao kwa lengo la kubainisha aina ya taarifa ambazo washiriki wangependa kushirikishana na wenzao (kwa mfano, mahali ninapoishi, maisha yangu ya kila siku, shule yangu na darasa nililopo (ikiwa ni mwanafunzi), familia yangu, dini yangu, mambo yanayonifurahisha, vitu vinavyonikosesha furaha, mambo niliyobobea, mambo ambayo sina utaalamu nayo, malengo yangu ya baadaye nitakapokuwa mkubwa, kwa nini niliamua kujiunga na kikundi cha watoto, n.k).

3) Waambie watoto waandike taarifa hizi kwenye miti yao. Toa muda kwa watoto kujichunguza na kushirikishana mambo tofauti na wenzao kwa njia isiyo rasmi. Washiriki wote watakapokuwa wamemaliza, waombe watoto wachache wajitolee kuwaambia washiriki wengine kwenye kundi kuhusu mti wa maisha yao. Baada ya mawasilisho kadhaa, waambie washiriki wachanganyikane na kujaribu kutafuta mambo yanayofanana na yanayotofautiana katika miti yao.


*Kwa mfano:*
*Mliyekulia naye sehemu moja – na anayetoka sehemu tofauti.*
*Mnayehuzunishwa na kitu kimoja – na anayehuzunishwa na kitu kingine tofauti kabisa.*
*Aliyebobea kwenye mambo sawa na yako – na aliyebobea kwenye kitu kingine tofauti. (Haya ni mapendekezo tu; kuwa mbunifu na uje na mawazo mapya.)*

**Tafakari na majadiliano:**
Maliza kikao kwa kuendesha mjadala kuhusu mambo yanayofanana na yanayotofautiana na namna ambavyo mambo hayo yanachukua nafasi katika utambulisho wetu. Jadilini umuhimu wa kuheshimu utambulisho na tofauti za kila mmoja.

Mwache kila mtoto abaki na mchoro wake.

**Utofauti:**
Kama kwenye kikundi kuna watoto wasioona, unaweza kuwaambia watoto wafanye mawasilisho yao kwa kuzungumza badala ya kutumia michoro.

## 2.2 Mti wa kikundi chetu



**Lengo:** Kuwahamasisha washiriki watafakari kuhusu utambulisho wa kikundi, mambo gani yanakifanya kikundi chao kuwa imara na jinsi ya kukabiliana na mapungufu.

**Kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa, kigawe kwenye vikundi vidogo vidogo vya watoto 6-8.

**Vifaa:** Karatasi, kalamu za rangi au kalamu za kutia alama.

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**

1) Kiambie kila kikundi kuchora mti wenye mizizi, shina, matawi na majani unaoonyesha kundi/chama chao. Jadiliana nao ili ijulikane wazi vipengele tofauti vya mti huo vinawakilisha nini. Kwa mfano, mizizi inaweza kuchukuliwa kama misingi ya kikundi (yaani, watoto wenyewe), shina la mti kama nguvu inayoendesha kikundi, matawi kama shughuli zinazofanywa na kikundi, na majani kama watu wanaoguswa na shughuli hizo. Pembejeo kutoka nje ili kusaidia mti kuwa imara zinaweza kuchukuliwa kama miale ya jua au mvua. Changamoto, mapungufu au vitisho vinaweza kuonekana kama watu wanaokata mizizi au matawi ya mti huo.

2) Viombe vikundi vijadili mambo yanayounda vipengele tofauti katika kila kikundi. Mambo gani yanaupa nguvu mti wa kikundi (Shawishi vikundi hivi kutilia mkazo wajibu wao wenyewe katika kuongeza uimara wa mti huo). Ipi ni misingi ya mti, shughuli zipi zinafanyika, watu gani wanafikiwa na shughuli hizi? Kuna changamoto, mapungufu au vitisho gani?

3) Ruhusu vikundi viwasilishe michoro yao.

**Tafakari na majadiliano**

Tunza michoro kwenye mafaili ya kikundi, au ikiwa kikundi kina chumba, bandika michoro hii kwenye kuta.

## 2.3 Vikundi vya majadiliano kuhusu heshima

**Lengo:** Kuanzisha mjadala kuhusu dhana ya 'heshima', nini maana yake, na namna ambavyo ukosefu wa heshima unaweza kuathiri kikundi na jamii kwa ujumla.

**Kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa, kigawe kwenye makundi madogo ya watoto 6-8.

**Vifaa:** Karatasi na kalamu kwa ajili ya kuchukua maoni.
**Muda:** Saa 1-2.

**Kazi:**
1) Kiombe kila kikundi kijadili maswali yafuatayo:
    - Nini maana ya heshima?
    - Nani anakuheshimu? Nani kwa kawaida huwa hakuheshimu? Unawezaje kufahamu kama watu wanakuheshimu?
    - Ni kwa kiasi gani unaonyesha heshima kwa watu wengine? Ni nani kwa kawaida huwa unamuheshimu siku zote? Ni wakati gani na kwa sababu zipi huonyeshi heshima kwa watu wengine?
    - Ni nani anaheshimiwa zaidi shuleni, kwenye familia na kwenye jamii kwa ujumla? Nani anapata heshima kidogo zaidi? Kwa nini?
    - Hoja zipi hutolewa kutetea kuheshimu kila mtu muda wote?
    - Hoja zipi hutolewa kutetea kuheshimu watu fulani pekee?
    - Hali ya kuheshimiana ikoje ndani ya kikundi cha watoto? Tunawezaje kuhakikisha kuwa kila mtu anaheshimiwa
    - Ni mambo gani unamfanyia mtu kuonyesha kuwa unamheshimu?
    - Je mtu akikufanyia nini au mambo gani utaona kama amekuheshimu?

2) Acha kila kikundi kielezee mahitimisho yake kwa vikundi vingine.

**Tafakari na majadiliano:**
Jadilini tofauti na mifanano ya maoni ya vikundi hivi. Sisitizia kuwa kila mmoja ana haki ya kuheshimiwa na wajibu wa kuwaheshimu wengine, bila kujali umri na nafasi yake kwenye jamii. Fafanua kuwa kuheshimu watu hakuna maana ya kukubali tabia isiyo ya haki au ya udanganyifu.

## 2.4 Mchezo kuhusu ushiriki wa Watoto

**Lengo:** Kuhamasisha kufikiri kuhusu hali mbalimbali za watoto wanapoanza kushiriki kwenye kikundi na utambuzi wa umuhimu wa kushirikishwa.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Flipchati, kadi/vipande vya karatasi na kalamu za kutia alama.

**Muda:** saa 1

**Kazi:**

1) Waombe washiriki wataje makundi mbalimbali ya watoto kwenye jamii na kuyaorodhesha kwenye flipchati (kwa mfano, wavulana, wasichana, watoto wenye ulemavu, walioathirika na VVU, wanaotoka kwenye familia tajiri au masikini sana; yatima, zeruzeru, Waislamu, Wakristo, Wahindu, n.k.). Orodha itakapokuwa tayari, gawa uhusika (ukihusisha jinsia na umri) kwa kila mtu (kwa mfano, msichana Mwislamu wa miaka 12, mvulana yatima wa miaka 16). Ili kuhakikisha kuwa watoto wanakumbuka uhusika wao, unaweza kuandika mambo wanayotakiwa kufanya kwenye kadi au kwenye kipande cha karatasi.

2) Waambie washiriki wasimame kwenye mstari. Eleza kwamba utasoma mifano ya hali mbalimbali za kimaisha, na washiriki watapaswa kusogea hatua mbili mbele kwa kila hali ambayo wanaona inaendana moja kwa moja na uhusika wao, kusogea hatua moja mbele ikiwa hali iliyotajwa 'kuna wakati' inaendana na uhusika wao, na kubaki walipo ikiwa hali iliyotajwa haiendani na uhusika wao. Anzeni kwenye sehemu iliyokubaliwa na kila kikundi na weka mstari wa kumalizia kukatiza sehemu/chumba kinachotumika.

3) Soma hali hizo:
   - Unaweza kwenda shule?
   - Unaweza kutumia usafiri wa umma?
   - Ni salama kwako kwenda nyumbani mwenyewe usiku?
   - Unadhani watoto wengine wanakusikiliza?
   - Unadhani watu wazima wanakusikiliza?
   - Unadhani watu wazima wanakutendea inavyostahili?
   - Je, watu wangekusikiliza kama ungeongea kwenye mkutano wa kijamii?
   - Unaweza kucheza michezo mbalimbali kirahisi?
   - Je, unaweza kushiriki bila shida kwenye shughuli mbalimbali baada ya kutoka shule?

- Je, unahisi kukaribishwa kwenye (sema jina la kikundi/chama husika)?
- Je, unaweza kushiriki bila shida yoyote kwenye shughuli tofauti za (sema jina la kikundi/au chama husika)?

**Tafakari na majadiliano:**
Mara baada ya kumalizika kwa zoezi, acha washiriki wabaki kwenye sehemu walizomalizia na kujadili uzoefu wao. Ulipata hisia gani? Unajisikiaje kuwa mbele kabisa au nyuma? Jadilini wahusika waliopata wakati mgumu kushiriki kwenye shughuli za kikundi na kwa nini hawakuweza, na ruhusu maoni ya nini kifanyike ili kuhakikisha watoto hao wanaweza kushiriki.

**Utofauti:**
Kama kuna watoto wenye ulemavu kwenye kikundi, wanapaswa kusaidiwa kushiriki.

## 2.5 Majadiliano kuhusu masuala ya jinsia

**Lengo:** Wavulana na wasichana wana majukumu tofauti ya kijamii, na mara nyingi mambo wanayopendelea na mahitaji yao huwa tofauti pia. Madhumuni ya kielekezi hiki ni kuhamasisha mjadala kuhusu majukumu ya kila jinsia na historia zake, na kuongeza ushiriki wa watoto wa jinsia zote.

**Kikundi:** watoto 8-30
**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama.

**Muda:** saa 1-2

**Kazi:**

1) Gawa washiriki kwenye vikundi vidogo vidogo (watu 6-8), baadhi vikiwa na wavulana pekee na vingine wasichana pekee.(nadhani kwa mara ya kwanza wavulana wawe pekee na wasichana wawe pekee ili baadae wanaweza kuchanganyika. Lengo ni kutoa uhuru wa kuongea

2) Kila kikundi kichore kwenye flipchati jedwali lenye visanduku nane, halafu kijadiliane na kujaza maneno muhimu au michoro kwenye visanduku hivi.

| | |
|---|---|
| Wasichana hupenda: | Wavulana hupenda: |
| Wasichana hawapendi: | Wavulana hawapendi: |
| Wasichana wanatarajiwa: | Wavulana wanatarajiwa: |
| Wasichana hawaweki wazi maoni yao pale: | Wavulana hawaweki wazi maoni yao pale: |

3) Ruhusu vikundi viwasilishe kazi zao.

4) Zoezi hili pia linaweza kuongezwa na zoezi la wasichana wataje sifa za wavulana hali kadhalika wavulana wataje sifa za wasichana. Kisha sifa hizo zijadiliwe kwa pamoja ili kubaini ni zipi za kijinsi na kijinsia ,zipi zinabagua na zipi zinaunganisha.

**Tafakari na majadiliano:**

Endesha mjadala kuhusu mambo yafuatayo:

- Nini tofauti kati ya maelezo yaliyotolewa kuhusu wavulana na kuhusu wasichana? Kwa nini yanatofautiana? Tofauti zipi zinatokana na maumbile (za kiasili) na zipi zinatokana na mitazamo ya kiutamaduni na kijamii ?

- Unadhani kwamba wazazi wako au mababu na mabibi zako wangejaza visanduku hivyo kwa namna tofauti wakati walipokuwa watoto? Kwa nini/kwa nini hapana?

- Tutawezaje kuhakikisha kuwa shughuli za kikundi zinafurahiwa na wote, wavulana na wasichana? Tutawezaje kuhakikisha kuwa kila mtu anatoa maoni yake?

## 2.6 Kuelewa migogoro – mitumbwi ziwani

**Lengo:** Kuhamasisha tafakari kuhusu migogoro na sababu zake.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Kurasa za magazeti

**Muda:** Saa 1

**Kazi:**

1) Tandaza kurasa za gazeti kwenye sakafu/udongo ukiacha nafasi kati ya ukurasa na ukurasa. Anza na kurasa nyingi za magazeti. Waambie washiriki kwamba kila ukurasa unawakilisha mtumbwi unaoelea kwenye moja ya ziwa au mto hapa Tanzania. Waambie 'waogelee' (watembee) kuzunguka mitumbwi hiyo bila kuikanyaga na kwamba utakaposema kwa sauti "mamba!" wanapaswa kurukia kwenye moja ya mitumbwi (panaweza kuwa na mshiriki zaidi ya mmoja kwenye mtumbwi, ila ikiwa tu wote wamesimama kwenye gazeti). Baada ya hapo watarudi kuendelea kutembea kati ya visiwa.

2) Baada ya kila 'shambulio la mamba', ondoa mtumbwi moja, ili kwamba idadi ya mitumbwi iwe inapungua taratibu. Mwishowe, hakutakuwa na nafasi ya kutosha kwa washiriki wote; wale wasioweza kuingia kwenye mtumbwi watakuwa wametolewa kwenye mchezo. Acha mchezo uendelee mpaka utakapobaki mtumbwi mmoja na wengi wa washiriki watakapokuwa wametolewa.

**Tafakari na majadiliano:**

Jadili zoezi hilo na washiriki, kwa mfano, kwa kutumia maswali yafuatayo:

- Nini kilitokea pale mitumbwi ilipokuwa imebaki michache? Watu walifanya nini?
- Ulijisikiaje uliposhindwa kuingia kwenye mtumbwi na ukatolewa kwenye mchezo?
- Uliwezaje kulinda nafasi yako mwenyewe? Je, ulipambana na wengine? Uliwasaidia wenzako? Je, ungeweza kufanya jitihada zaidi kusaidia wengine?
- Je, mambo kama haya yanatokea kwenye maisha ya kila siku?

Husianisha mchezo huu na hali ya kila siku katika maisha na endesha mjadala pamoja na washiriki kuhusu rasilimali na vyanzo vya migogoro. Waambie washiriki kwamba migogoro ni kitu cha kawaida ila tu inaweza kuambatana na vurugu pale watu wanaposhindwa kugawana, kushirikiana na kuwa na umoja/mshikamano na wengine. Mara nyingi tumezoea kutatua migogoro kwa kujifikiria sisi wenyewe kwanza, lakini je tunafanya jitihada gani za pamoja katika kubadili kabisa mazingira fulani ili pasiwepo na watu wasio fursa?

## 2.7 Hatua sita za kutatua tatizo

**Lengo:** Mgogoro ni kitu cha kawaida katika mahusiano ndani ya kikundi, lakini ni muhimu sana kutafuta njia muafaka za kuitatua. Kielezi hiki kinawafahamisha washiriki kuhusu mbinu rahisi za kutatua migogoro baina yao ambazo zinaweza kutumika ndani ya vikundi na hata katika mahusiano ya aina nyingine.

**Ukubwa wa kikundi:** watoto 8-30
**Vifaa:** Hakuna

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wawili wajitolee kuigiza mgogoro, kama vile mzozo juu ya kitabu au kifaa kingine chochote wakiwa shuleni; utani kuhusu mwonekano au mavazi; kulazimishwa na mtu kutoa fedha; kurudishiwa kitu kikiwa kimechakaa au kuharibika; au kulazimishwa kufanya kitu usichotaka. Washiriki waliojitolea wafanye igizo hilo mbele ya wanakikundi wengine. Itapendeza zaidi kama malumbano yatakuwa makali hadi washindwe kufikia muafaka.

2) Wafahamishe washiriki kuhusu mchakato wa hatua sita za kutatua tatizo:

Hatua ya 1. Tambua mahitaji: "Ni nini hasa unahitaji (au unataka)?"
Muombe kila mtu aliye katika mzozo kujibu bila kumlaumu au kumshutumu mwenzake.

Hatua ya 2. Fafanua tatizo: "Unalionaje tatizo?"
Waambie washiriki wa kikundi wasaidie kupata jibu linalojumuisha mahitaji ya watu wote wawili na ambalo halimtii mmoja wao lawamani. Mtu aliye kwenye mgogoro anapaswa akubaliane na namna tatizo lilivyofafanuliwa.

Hatua ya 3. Endesha mjadala mzito ili kupata ufumbuzi wa aina mbalimbali: "Nani anaweza kufikiria njia ya kutatua tatizo hilo?" Yeyote kwenye kikundi anaweza kutoa jibu. Majibu yote yanapaswa kuandikwa mahali, bila kutoa hukumu, maoni, wala tathmini juu yake. Hatua hii inalenga kupata aina nyingi za ufumbuzi kadiri inavyowezekana.

Hatua ya 4. Fanya tathmini ya ufumbuzi uliopatikana: "Je, ungefurahia ufumbuzi huo?"
Kila upande katika mzozo huu utapitia orodha ya ufumbuzi unaoweza kufaa uliopatikana, huku ukielezea ufumbuzi upi ungekubalika au usingekubalika.

Hatua ya 5. Fanya uamuzi kuhusu ufumbuzi bora zaidi: "Je, wote mnakubaliana na ufumbuzi huo? Je, tatizo limeisha?"
Hakikisha pande zote zinakubali na kutambua juhudi zao katika kutafuta ufumbuzi.

Hatua ya 6. Fuatilia kuona namna ufumbuzi huu unavyofanya kazi: "Hebu tuongee tena baada ya dakika kumi ili kuhakikisha kwamba matatizo yaliyokuwepo yameisha kabisa".

**Tafakari na majadiliano:**
Kuendesha mjadala kuhusu kitu gani kifanyike pale panapokuwa na tofauti kati yetu, na umuhimu wa kutafuta ufumbuzi badala ya kulaumiana. Onyesha umuhimu wa kurudi nyuma na kutazama ufumbuzi uliopatikana baada ya muda fulani ili kuhakikisha kuwa unafanya kazi. Jadili mazingira ambamo njia hii ya kutatua matatizo inaweza kutumika.

## 2.8 Michezo ya mawasiliano

**Lengo:** Mawasiliano na kufanya kazi kitimu ni mambo muhimu sana katika kuboresha ufanisi wa kikundi. Michezo hii inalenga kuzidisha ushirikiano kwa kujenga na kuleta umakini katika mbinu za kuwasiliana.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:**
Kamba na vitambaa vya kufunga machoni kwa ajili ya mchezo wa funga kidoto.
Karatasi na kalamu kwa ajili ya kubadilishana vitu visivyoonekana.
Hakuna vifaa kwa ajili ya michezo mingine.

**Muda:** Takriban dakika 30 hivi kwa kila mchezo.

**Kazi:**

**Mchezo wa kusikiliza**
Waambie washiriki wakae chini katika duara. Mwombe mshiriki mmoja afikirie sentensi fupi na amnong'oneze sikioni jirani yake aliyekaa upande wa kushoto, ambaye naye atapitisha ujumbe huo kwa jirani yake, na kuendelea. Pale ujumbe utakapokuwa umemfikia mtu aliyekaa upande wa kulia wa aliyetoa ujumbe huo, mtu huyo aseme kwa sauti ujumbe huo. Halafu yule aliyetengeneza ujumbe huo mwanzoni naye amwambie kila mtu ujumbe halisi kama ulivyokuwa mwanzoni. Mara nyingi ujumbe halisi huwa umebadilika kwa kiasi kikubwa njiani.

Jadili: Kwa nini ujumbe ulibadilika? Je, hii inaweza kulinganishwa na hali mbalimbali katika maisha ya kila siku? Utahakikishaje kwamba hakuna upotoshaji wa mawasiliano na ujumbe?

**Kubadilishana vitu visivyoonekana**
Mwambie kila mtu afikirie kitu. Pitia washiriki wote na orodhesha vitu hivyo.
Waambie washiriki wabadilishane vitu vyao, wakisema 'nakupatia kitu changu XXXX'. Halafu wabadilishane kitu cha pili na cha tatu na kuendelea mpaka watakapokuwa wamebadilishana vitu sita. Waambie washiriki waseme kwa sauti vitu ambavyo wanavyo kwa sasa. Viorodheshe. Soma orodha hizo mbili za vitu. Mara nyingi baadhi ya vitu vitakuwa vimetoweka, vingine vitakuwa vimeongezeka.

Jadili: Kwa nini vitu hivyo vilibadilika? Je, ungeweza kufanya kitu chochote kuepuka 'kupoteza' au kubadilisha kitu chochote? Je, aina hii ya mawasiliano inaweza kulinganishwa na hali mbalimbali katika maisha ya kila siku?

**Mchezo wa funga kidoto.**
Funga ncha mbili za kamba pamoja. Waambie washiriki wote washike kamba kwa mikono yote miwili na wafunge macho yao au wafungwe kitambaa machoni na msimamizi. Halafu toa maagizo kwa kikundi kutengeneza maumbo tofauti bila kuachia kamba. Mifano ya maumbo inaweza kuwa mraba, pembe tatu, mstatili, nyota, n.k. Waambie washiriki wote wa kikundi washirikiane kitimu ili kufanikisha shughuli hii na pia wapatie muda maalumu wawe wamemaliza. Kila baada ya jaribio moja, watake washiriki kufungua macho yao na kuangalia umbo walilotengeneza.

Jadili: Kwa nini ilikuwa rahisi/ngumu? Kuna 'mikakati' yoyote ilitumika, ipi? Je, mmoja wenu alikuwa kiongozi wa kikundi? Kwa nini? Baada ya majaribio kadhaa, waambie washiriki kuunda umbo, lakini safari hii bila ya kuongea.

Jadili: Mawasiliano kwa njia ya mdomo yana nafasi gani katika ushirikiano?

**Ujumbe wa dakika moja**
Waambie washiriki wakubaliane ujumbe mmoja wa kuufanyia kazi (kwa mfano, watoto wote wanapaswa kwenda shuleni, jamii inapaswa kusikiliza maoni ya watoto, adhabu ya viboko inapaswa kufutwa, n.k). Wagawe washiriki kwenye vikundi vidogo vidogo na toa dakika kumi kwa kila kikundi kuandaa njia ya kuwasilisha ujumbe wao. Uwasilishaji wa ujumbe huo haupaswi kuchukua zaidi ya dakika moja, ila vikundi vinaweza kutumia njia yoyote watakayotaka (mifano inaweza kuwa nyimbo, hotuba, igizo, n.k). Ruhusu vikundi viwasilishe ujumbe wao.

Jadili: Njia zipi za kufikisha ujumbe zilikuwa na ufanisi zaidi? Kwa nini?

# Sura ya 3: Tunawezaje kutambua na kuchunguza masuala yanayohusu watoto katika jamii zetu?



Ushiriki  kwa watoto una maana pale tu wanaposhiriki kwenye masuala ambayo ni muhimu kwao na kwa watoto wenzao kwenye jamii. Katika sura hii, vielekezi vinawasaidia watoto kutambua na kufuatilia masuala yanayowahusu. Kwenye baadhi ya vikundi vya watoto, vielekezi hivi vinaweza kutumiwa ndani ya kikundi chenyewe. Kwenye vikundi vingine (kwa mfano, mabaraza ya watoto), ingefaa zaidi kama watoto hawa wakialika watoto wengine kwa ajili ya kufanya majadiliano.

**Mwongozo:**

- Zingatia na kuwa tayari kukabiliana na masuala magumu. Katika mchakato wa kutafiti masuala ya watoto, kuna uwezekano mkubwa wa kukutana na watoto waishio katika mazingira magumu ambao wako katika uhitaji mkubwa wa msaada. Tafuta nani ambaye unaweza kuwapeleka watoto kwake (tazama sehemu ya 3.7).

- Fikiria kama ushiriki wa watoto katika kutambua masuala yanayowahusu unaweza kuwaweka katika hatari kwenye familia au jamii zao. Hakikisha unawapa taarifa wazazi na wadau wengine (kwa mfano, walimu na viongozi wa jamii) na kuwahusisha kwenye mchakato ili kuhakikisha kwamba wanaelewa na kuunga mkono malengo na shughuli zao.

- Kama kujua kusoma na kuandika ni tatizo kwa watoto, fanya mawasilisho kwa tumia michoro na mazungumzo badala ya maandishi.


- Kama kwenye kikundi kuna watoto, anzisha vitendo ambavyo vinajumuisha zaidi majadiliano kwa njia ya mazungumzo na hakikisha wanasaidiwa, kwa mfano, katika kuandika maoni. Kama kuna watoto wenye matatizo ya kusikia kwenye kikundi, andaa utaratibu wa ukalimani wa lugha ya alama au tumia maandishi na michoro.

**Kamusi:**

Dira: Taswira ya siku zijazo. Dira inaonyesha wapi unataka kwenda kwa ujumla hatua kwa hatua.

Kisa: hapa kisa kinamaanisha maelezo ya kina ya hali au mchakato alioupitia mtoto katika jamii (kikisimuliwa bila muhusika kujitambulisha).

## 3.1 Kutambulisha jamii kwa misingi ya masuala ya watoto



**Lengo:** Kutafiti/kufuatilia/kuchunguza masuala ya yanayowahusu watoto katika jamii, kubainisha matatizo na mapendekezo kwa ajili ya mabadiliko.

**Ukubwa wa kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa, kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watoto 6-8.

**Vifaa:** Vifaa tofauti vya asili vinavyopatikana mahali husika (kwa mfano, vijiti, majani, mawe ya aina tofauti, vifaa vilivyotumika (vilivyo safi), karatasi, kalamu.

**Muda:** Takriban saa 2

**Kazi:**

1) Waambie washiriki watengeneze ramani ya jamii ardhini kwa kutumia vifaa vya asili vinavyopatikana. Mifano ya alama zinazoweza kutumika ni kama mashamba, shule, nyumba za familia, majengo tofauti ya kwenye jamii, sehemu za kazi, ofisi za serikali, viwanja vya michezo, n.k.

2) Waambie washiriki wajadili kama watoto wana furaha au la katika mazingira tofauti yaliyopo kwenye ramani, na kuweka alama kwenye ramani kuonyesha mtoto mwenye furaha na mtoto asiye na furaha (Hizi zinaweza kuwa nyuso ndogo za furaha na zisizo za furaha). Waambie washiriki wajadili sababu ya kufanya maamuzi haya.

3) Waambie washiriki wabainishe na kuandika vitu 3 ambavyo wangependa kuvibadilisha katika jamii ili kuboresha hali katika jamii.

4) Ruhusu kila kikundi kiwasilishe kazi yake kwa kikundi kingine.

**Tafakari na majadiliano:**

Jadili:

- Kitu gani kinafanya mazingira fulani yawe mazuri au mabaya kwa watoto?
- Je, kuna tofauti kati ya ramani za vikundi tofauti? Je kuna mambo yanayofanana?
- Je, unaweza kukubaliana na vitu 3 muhimu kuliko vyote ambavyo ungependa kubadilisha kwenye jamii? Kwa nini vitu hivyo?
- Je, kuna tofauti kati ya maoni ya wavulana na wasichana? Kama ndiyo, Kwa nini?
- Je, kuna tofauti kati ya vikundi tofauti vya watoto katika jamii? Kama ndio, Kwa nini?

**Utofauti:**
Unaweza kuwaambia washiriki kutengeneza ramani kuhusu aina za vikundi tofauti vya watoto, kwa mfano, kikundi cha umri fulani, wavulana na wasichana, masikini na matajiri, walemavu n.k. Kama kuna watoto wasioona kwenye kikundi, hakikisha wanapewa nafasi ya kushiriki kwenye mijadala.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Orodhesha sehemu mbaya na nzuri zilizotajwa na watoto na sababu za kufikia maamuzi hayo. Orodhesha pia mambo ambayo watoto wanataka yabadilishwe. Tunza orodha hizo kwenye mafaili ya kikundi.

## 3.2 Kitu gani kinachotufurahisha, kitu gani tungependa kibadilike

**Lengo:** Shughuli hii ni rahisi zaidi ikilinganishwa na zoezi la kugawa makundi mbalimbali kwenye jamii, ikilenga hasa kuchunguza masuala ya watoto na kubainisha changamoto zinazowakabili katika jamii.

**Ukubwa wa kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Karatasi na kalamu.

**Muda:** Saa 1

**Kazi:**

1) Mwambie kila mshiriki aandike vitu 3 anavyovifurahia katika maisha yake na vitu ambavyo angependa vibadilike.

2) Wakusanye washiriki katika vikundi vya watu 5-8 na waambie wachangie na kujadili mawazo yao, na kuyaorodhesha pamoja kwenye kipande cha karatasi.

3) Ruhusu vikundi viwasilishe tafiti zao.

**Tafakari na majadiliano:**

Endesha mjadala kuhusu mambo yafuatayo:

- Je, kuna mambo yanayofanana kati ya vitu vinavyotufurahisha? Kwa nini vinatufurahisha?
- Je, kuna mambo yanayofanana kati ya vitu vinavyotuudhi? Kwa nini vinatuudhi? Tufanye nini ili kubadilisha mambo haya?
- Je, kuna tofauti kati ya maoni ya wavulana na wasichana? Kama ni ndiyo, kwa nini?
- Je, kuna tofauti kati ya vikundi tofauti vya watoto katika jamii? Kama ndio, Kwa nini?

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**

Andika kwa ufupi matokeo ya utafiti huu na kuyatunza kwenye mafaili ya kikundi.

## 3.3 Kuigiza kuhusu masuala ya watoto

**Lengo:** Kuigiza kunaweza kutusaidia kuelewa na kupata picha ya hali ya watoto wengine. Shughuli hii inalenga kutafiti masuala ya watoto na kubainisha changamoto za vikundi tofauti vya watoto.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** karatasi na kalamu kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu kwa maandishi.

**Muda:** Saa 2

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wajadili na kuorodhesha vikundi tofauti vya watoto vilivyopo kwenye jamii (kwa mfano, wasichana, wavulana, walemavu, masikini, matajiri, yatima, watoto waishio katika mazingira magumu, watoto wanaofanya kazi n.k.)

2) Gawa washiriki katika vikundi vidogo vidogo (watu 4-6) na gawa watoto tofautitofauti kati ya vikundi. Waambie washiriki wa kila kikundi waigize kuhusu siku ya kawaida katika maisha ya mtoto wa aina hiyo.

3) Ruhusu kila kikundi kiwasilishe igizo lake. Baada ya hapo jadili na orodhesha changamoto zilizomkabili mtoto aliyeigizwa. Wakaribishe washiriki wengine kuongeza changamoto ambazo hazikuonyeshwa kwenye igizo.

**Tafakari na majadiliano:**
Wakati vikundi vyote vitakapokuwa vimeshawasilisha michezo yao ya kuigiza, jadili changamoto zipi zinafanana kwenye vikundi vingi vya watoto, na zipi ni za kipekee kwenye kikundi pekee cha watoto. Jadili nini kinaweza kufanyika ili kukabiliana na hizo changamoto.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Tunza orodha ya za changamoto.

## 3.4 Kukusanya visa vya matukio

**Lengo:** Visa vya matukio hufanya matatizo ya watoto kufahamika katika jamii. Shughuli hii inalenga kuchunguza masuala ya watoto na kubainisha changamoto zinazowakabili watoto.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Karatasi, kalamu

**Muda:** Mkutano wa kwanza: Dakika 30 kwa ajili ya maandalizi, mkutano unaofuata: saa 1-2 kujadili visa, kutegemeana na idadi.

**Kazi:**

Maandalizi:

1) Wafahamishe washiriki kuhusu wazo la kukusanya visa vya matukio yanayohusu hali za watoto katika jamii. Eleza kwamba kisa ni tukio la kweli lakini kutoka kwa mtoto asiyejitambulisha, kikilezea kuhusu hali ambayo inaweza kuwatokea watoto wengine pia.

Mpangilio wa kisa unaweza kuwa:

- Mchoro wa tukio
- Maelezo (maandishi au masimulizi): Nini kilitokea? Mtoto alijisikiaje kwenye tukio hilo? Watu wengine walifanya nini dhidi ya tukio hilo? Nini kilitokea baadaye?

2) Jadili na watoto kama wanafikiri itakuwa ni rahisi kwao kukusanya matukio ya visa kutoka kwa watoto wenzao katika jamii– au kuelezea baadhi ya visa ambavyo vimewatokea wao binafsi. Kama wanakubali, waambie waje na hivyo visa wakati ujao mtakapokutana.

Mjadala wa visa:

1) Wakati ujao, waache watoto wasimulie visa ambavyo wamekusanya. Pitia moja baada ya kingine.

2) Baada ya kila kisa, endesha mjadala unaohusu mambo yafuatayo:

- Je hali hii ni ya kawaida katika jamii yetu? Kwa nini / Kwa nini siyo?
- Kama kisa kinaelezea hali ngumu, nini kingeweza kufanyika ili kutatua hilo tatizo?

**Tafakari na majadiliano:**
Jadili na washiriki kama walipata ugumu kukusanya visa vya matukio na kwa nini /Kwa nini hapana?
Kama utakutana na visa vya kusikitisha vya udhalilishaji wa watoto fanya jitihada kutatua hilo tatizo na jaribu kuripoti katika mamlaka husika kama vile vyombo vya usalama au taasisi yoyote inyoweza kusaidia( kwa mfano. polisi, afisa ustawi wa jamii, afisa maendeleo yaa jamii nk.). Jadili na watoto namna ya kukabiliana na visa hivyo vya kusikitisha (tazama sehemu ya 3.7) na wape moyo wa kuwajulisha watoto wenzao.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Tunza visa vya matukio. Kama sio vya kudhalilisha sana, vinaweza kutumiwa baadaye kama sehemu ya maonyesho au kampeni.

## 3.5 Dira ya jamii inayojali maslahi ya mtoto

**Lengo:** Tafiti mitazamo ya watoto na bainisha mawazo ya kuleta mabadiliko.

**Kikundi:** Kama kikundi ni kubwa, kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watoto 6-8.

**Vifaa:** Karatasi, gundi, kamba, kalamu za kutia alama, mabaki ya vifaa (vifaa vilivyotumika, magazeti, majani, vijiti n.k..

**Muda:** Saa 2

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wa kila kikundi watengeneze mji wao binafsi au jamii kwa kutumia mabaki ya vifaa. Jamii inatakiwa iwe moja ambamo watoto wanaishi kwa furaha. (mji wa kufikirika) weka vitu vinavyofanya watoto wafurahie. Kikundi kinatakiwa kujadiliana zaidi na kuamua kuhusu baadhi ya/au mambo yote yafuatayo:
    - Jina la mji na kwa nini walichagua jina hili.
    - Sheria za huo mji.
    - Hali ya uchumi ya jamii (watu wanafanya kazi za aina gani na ubora wa maisha ukoje).
    - Huduma za shule, afya, dini, mfumo wa sheria, ukusanyaji wa takataka na shughuli zingine zinaendeshwaje.
    - Nafasi ya watoto katika jamii.

Vikundi vinaweza pia kutengeneza nembo ya mji wao na kujadili maana ya alama zilizotumika.

2) Waambie washiriki wa vikundi kuwasilisha miji au jumuiya zao ili kuwafundisha wengine.

**Tafakari na Majadiliano:**
Jadili mawazo gani yamejitokeza ambayo yanaonekana kuwa na manufaa na ya kupendeza. Je jamii hizi za kubuni zimetofautiana vipi na jamii halisi, tunamoishi? Bainisha na orodhesha mawazo yanayofanana yanayohusu kitu kinachofanya jamii kuwa sehemu nzuri kwa watoto.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Kama inawezekana, tunza hiyo mifano au kwa namna nyingine ipige picha.

## 3.6 Kuchanganua matokeo

**Lengo:** Baada ya kukusanya taarifa zinazohusu mitazamo ya watoto kuhusu masuala yao, unatakiwa kuchambua taarifa hii ili kuelewa mwelekeo wa jumla wa masuala hayo. Vielekezi vilivyoelezewa hapa vinatoa njia rahisi (na ambavyo si vya kisayansi) kwa ajili ya kufanyia uchanganuzi.

**Kikundi:** watoto 8-20

**Vifaa:** Flipchati, vipande vya karatasi / Kadi nyingi, kalamu za kutia alama

**Muda:** Saa 1

**Kazi:**

1) Kwa kushirikiana na washiriki fanya tena mapitio ya tafiti za kazi zozote zilizofanywa kwa lengo la kuchunguza masuala ya watoto katika jamii.

2) Chora jedwali kama lifuatalo hapa chini na orodhesha mambo ambayo yamejitokeza. Jadili na watoto kama, kutokana na matokeo ya tafiti zao pamoja uzoefu wao binafsi kwenye jamii, suala hilo ni la kawaida kwa watoto wengi, wa wastani au wachache.

| Suala | wachahe | Wastani | wengi |
|---|---|---|---|
| *Mifano:*<br>*Watoto wasiosoma shule* | | | |
| *Watoto wasiotaka kusoma shule* | | | |
| *Watoto wanaofanya kazi kwa muda wote* | | | |
| *Watoto wasiokuwa na wazazi* | | | |
| *Watoto wanaonyanyaswa* | | | |

3) Pitia tafiti au jadili kazi zilizofanywa ili kuchunguza maoni ya watoto katika jamii na orodhesha mawazo yoyote ya mabadiliko ambayo yamejitokeza. Andika kila wazo kwenye kipande cha karatasi (wazo moja kwenye kadi moja). Waambie watoto wapange kadi katika makundi. Jadili mapendekezo gani ya mabadiliko yamejumuishwa katika kila kundi.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Tunza jedwali na orodha ya mapendekezo ya mabadiliko yaliyopangwa katika vikundi kwa ajili ya kutumika kama marejeo ya baadaye.

## 3.7 Kukabiliana na masuala magumu

**Lengo:** Kuhakikisha kwamba mwezeshaji pamoja na kikundi wako tayari kwa ajili ya kukabiliana na masuala magumu yaliyowakabili au kubanishwa wakati wa kazi za kikundi.

**Kikundi:** kama kikundi ni kikubwa kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watoto 6-8.

**Vifaa:** Kadi/vipande vya karatasi, flipchati na kalamu za kutia alama, wino.

**Muda:** Saa 1

**Kazi:**

1) Waambie watoto katika kila kikundi watengeneze michoro kwenye kadi inayoonyesha sehemu ambazo watoto hawaishi kwa furaha. Kama, kuna ulazima, ongeza mwenyewe baadhi ya kadi ili kuhakikisha kuwa sehemu zote zinaonyeshwa.

2) Mifano:
   - Watoto ambao wanafanyiwa vitendo vya unyanyasaji uliokithiri kwenye familia zao au sehemu nyingine.
   - Watoto wanaoumwa sana.
   - Watoto wanaodhalilishwa.
   - Watoto wanaozuiwa kwenda shule.
   - Wasichana wanaoolewa katika umri mdogo.
   - Watoto wanaoishi katika mila hatarishi.

3) Waambie watoto wapange kadi katika vikundi kutokana na nani wanataka kuongea naye kama hali hiyo itaonyeshwa kwenye kadi.


4) Ruhusu vikundi viwasilishe kazi zao.


5) Andika orodha ya asasi au watu katika jamii ambao unaweza kuwafuata kwa ajili ya msaada kama unahitajika na jadili nani ataweza kutatua matatizo yapi.

6) *Mifano:*
   - Asasi zisizo za kiserikali
   - Viongozi wa kidini
   - Ofisi za ustawi wa jamii (ofisi ya wilaya)
   - Kituo cha msaada wa kisheria (haki, masuala ya kisheria)
   - Polisi
   - Madaktari, wauguzi, hospitali, kliniki
   - Viongozi wa kijiji/Jumuiya
   - Marafiki watu wazima na watu wengine wanaoweza kusaidia
   - marafiki

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Tunza orodha.

# Sura ya 4: Tunawekaje malengo ya kazi?






Malengo ni shabaha zinazoongoza kazi yako na hutumika kama mahali pa kuanzia katika shughuli za uwekaji wa mipango. Sura hii inatoa mapendekezo kwa shughuli za aina 3 tofauti ambazo zinaweza kutumika katika uwekaji wa malengo ya kazi ya kikundi cha watoto. Si lazima uzitumie zote tatu; chagua shughuli unayoona inakuvutia na itakifaa kikundi cha watoto unachofanya nacho kazi.

**Mwongozo:**


- Rekebisha vielekezi hivi kulingana na uwezo wa watoto. Ikiwa shughuli hizi zitaonekana kuwa ngumu, jaribu kurahisisha au kuchagua baadhi ya vipengele vyake.
- Tenga muda wa kutosha kwa ajili ya shughuli hizi, ikibidi tumia zaidi ya mkutano mmoja kwa kazi hii.
- Endapo kuna watoto wasioona kwenye kikundi, hakikisha kila kitu kinajadiliwa kwa njia ya mazungumzo na kwamba watoto hawa wanapewa msaada unaostahili, kwa mfano katika kuandika maoni yanayotolewa. Na endapo kuna watoto wenye tatizo la kusikia kwenye kikundi, fanya mpango wa kupata msaada wa tafsiri kwa lugha ya alama au tumia maandishi na michoro.
- Kama unashughulika na watoto wasiojua kusoma na kuandika, waambie wachore badala ya kuandika.

**Kamusi:**

*Dira:* Taswira ya siku za mbeleni. Lengo la dira ni kutoa maelezo ya jumla kuhusu mahali unakotaka kufika.

*Malengo:* Maelezo ya shabaha dhahiri za kazi inayofanyika.

## 4.1 Kuweka na kuchanganua dira



**Lengo:** Kuweka dira na malengo kwa ajili ya mradi/shughuli mbalimbali kwenye kikundi. Mtazamo huu wa uwekaji malengo unategemea mawazo chanya waliyonayo watoto.

**Kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa, kigawe kwenye makundi madogo madogo ya watoto 6-8.

**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama.

**Muda:** Saa 2

**Kazi:**

1) Ikiwa kikundi cha watoto kimeshughulikia uchunguzi na uchambuzi wa masuala yanayohusu watoto kwenye jamii, pitia upya matokeo waliyopata, hususan matokeo yenye uhusiano na mawazo ya kuleta mabadiliko katika jamii.


2) Kiombe kila kikundi kitengeneze mchoro wa puto la hewa ya joto (tazama kielelezo).
   Jadili:
   - Dira yako kwa watoto kwenye jamii ni ipi? Andika au chora dira yako juu ya puto. Mfano wa dira: Kwenye jamii yetu haki za watoto zinaheshimiwa na kila mtu.
   - Ni vitu vipi au mazingira gani lazima yawepo ili kuhakikisha kuwa dira hii itatimia? Haya ni malengo. Yaandike kama hewa ndani au pembeni mwa puto na kulisaidia puto kupaa. Mfano wa malengo:
   - Watoto wawe wanafahamu haki zao..
   - Wazazi/watu wazima wawe wanafahamu kuhusu haki za mtoto.
   - Maafisa wa serikali wawe wanawaelekeza watu kwenye jamii kuheshimu haki za mtoto.
   - Ni watu gani lazima washirikishwe ili kufanya uzingatiaji wa dira hii uwe wa mafanikio? Wachore au waandike kama wasafiri kwenye kikapu chini ya puto.
   - Mambo yapi yanaweza kuchelewesha au kuzuia utimizwaji wa dira hii? Hivi ni vikwazo. Yaandike chini ya nyaya zinazoshikilia puto.

3) Ruhusu vikundi viwasilishe dira zao.

**Tafakari na majadiliano:**
Jadilini dira tofauti na mkubaliane ipi muendelee kuifanyia kazi. Hili linaweza kufanyika kwa kufanya mjadala na kufikia muafaka au kwa kupiga kura. Mara baada ya washiriki wote kukubaliana dira ya kufanyia kazi, endesha mjadala kuhusu malengo yapi ya kufanyia kazi na namna ya kukabiliana na vikwazo.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Weka kumbukumbu ya dira zote na andika dira zipi na malengo yapi yataendelea kufanyiwa kazi na kikundi.

## 4.2 Kuibua mawazo kuweka vipaumbele



**Lengo:** Kuibua na kuchanganua mawazo kwa lengo la kupata uwezo wa kukabiliana na changamoto na matatizo mbalimbali.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Flipchati, kalamu, mawe madodo madogo

**Muda** : Saa 2

**Kazi:**

1) Kama kikundi cha watoto kilifanya uchunguzi na uchanganuzi wa masuala yanayohusu watoto kwenye jamii, pitia upya matokeo yaliyopatikana. Jadili namna ambavyo matatizo/changamoto mbalimbali zilizobainishwa zinahusiana. Tengeneza taswira ya matatizo haya kwa kutumia maneno au michoro – tazama kielelezo kwa mfano.

2) Waombe washiriki wapange changamoto wanazotaka kuzifanyia kazi kama kikundi kulingana na uzito wake. Hili linaweza kufanyika kwa kumtaka kila mshiriki aweke kura zake kwenye masuala matatu yaliyo juu ya taswira ya matatizo ambayo wanaona ni ya muhimu zaidi. Ikiwa taswira hii iko chini kwenye udongo, kura zinaweza kuwa mawe madogo madogo, na kama iko ukutani, kura zinaweza kupigwa kwa kuchora alama ndogo ndogo au nyota pembeni mwa changamoto. Kwa kuzingatia upigaji kura, waambie washiriki wakubaliane kuhusu changamoto moja, au kundi la changamoto kwa ajili ya kutilia mkazo.

3) Wagawe washiriki kwenye makundi madogo ya watu 6-8, na wapatie flipchati au kipande cha karatasi.
Gawa karatasi hii katika visanduku vinne:

| Mawazo ya kupatia ufumbuzi Nini? | Maswali | Maoni | Mawazo mapya |
|---|---|---|---|
| Namna gani? | | | |

Kila kundi lijadili kwa kina kuhusu mawazo ya kupatia ufumbuzi/njia za kukabili changamoto na kuandika mawazo hayo/njia hizi kwenye sanduku la kwanza. Mawazo/njia hizi zinapaswa kueleza nini kifanyike (kwa mfano, kusambaza taarifa kuhusu suala fulani) na toa mawazo ya namna ya kufanikisha jambo hilo (kwa mfano, kubandika matangazo, kuzungumza na watu, n.k). Halafu karatasi itolewe kwa kundi lingine, ambalo litapitia ufumbuzi uliopendekezwa, na kuandika maswali kadhaa, kutoa maoni yao na mawazo mapya. Baada ya hapo karatasi itolewe kwa kundi lingine tena.

4) Baada ya karatasi kuzunguka mara 3 au 4, itarudishwa kwa kundi la kwanza ilipoanzia, na washiriki wa kundi hilo wapitie upya mawazo yao kwa kuzingatia maswali yaliyoandikwa, na maoni na mawazo mapya yaliyotolewa.


5) Ruhusu kila kundi liwasilishe kwa ufupi mawazo yao waliyopitia.

   Napendekeza pia kwa mwezeshaji kuruhusu pongezi kwa kila kikundi kinapomaliza uwasilishaji wa kazi au taarifa. Pia washiriki wote kupongezana wanapomaliza hatua fulani ya majadiliano.


**Tafakari na majadiliano:**
Jadilini mawazo tofauti na mkubaliane mawazo yapi yatasaidia kuleta ufumbuzi muendelee kuyafanyia kazi. Hii inaweza kufanyika kwa njia ya majadiliano, kuafikiana au kupiga kura. Maelezo ya nini kifanyike ni malengo ya kazi ya kikundi.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Andika malengo yaliyokubaliwa. Hifadhi mawazo yote yaliyopatikana kwenye mjadala wa kina, hata yale msiyotarajia kuyafanyia kazi, yanaweza kusaidia kwenye kazi za baadaye.

# 4.3 Mti wa malengo na matatizo




Mti wa Matatizo




Mti wa Malengo

**Lengo:** Kuchanganua vyanzo na athari za matatizo, kutambua matatizo makuu, kuweka malengo.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Muda:** 2-3

**Vifaa:** Flipchati, kalamu za kutia alama, utepe wa kufunikia, kadi/vipande vya karatasi

**Kazi:**

1) Unda swali la jumla ili kuongoza mijadala, kwa mfano, "Hali ya watoto kwenye jamii yetu ikoje?" au "hali ya watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi kwenye jamii yetu ikoje?"

2) Endapo kikundi kimefanya uchunguzi na uchanganuzi wa masuala yanayohusu watoto kwenye jamii, pitia upya matokeo yaliyopatikana.

3) Gawa washiriki katika vikundi vya watu 4-6. Kiombe kila kikundi kuandika matatizo yote wanayoweza kufikiria kuhusiana na swali mojawapo la jumla (kwa msaada wa matokeo yaliyopatikana katika kipindi cha uchunguzi pamoja na mawazo yao wenyewe). Kila tatizo liandikwe kwenye kipande cha karatasi (tatizo moja kwa kila kipande cha karatasi).


4) Chora mti mkubwa kwenye kipande kikubwa cha karatasi (tumia flipchati mbili), au chini kwenye udongo.
Vilete vikundi pamoja na waambie washiriki kutoka kila kikundi kuangalia matatizo yote yaliyoandikwa na kutafuta moja ambalo linaonekana kuwa na uzito zaidi. Tatizo hili liwekwe juu ya shina la mti. Waambie washiriki waweke matatizo mengine kwenye matawi juu ya tatizo kuu endapo matatizo hayo ni matokeo ya tatizo kuu; au kwenye mzizi wa mti endapo ni chanzo cha tatizo hilo. Baada ya hapo endesha mjadala kuhusu uhusiano kati ya matatizo haya na yaweke kwenye mnyororo wa chanzo na athari. Kama itahitajika, tengeneza kadi za ziada (tazama kielelezo).badala ya kuchora wanaweza wakatumia karatasi kuwa umbo la mti....

5) Mara mti wa matatizo utakapokamilika, waambie washiriki wasaidie kuandika kadi mpya kuelezea hali ambayo ni kinyume ya ile iliyoelezwa katika kila kadi ya tatizo na kuziweka pamoja kama mti wa malengo. Mti huu unaonyesha hali chanya, ambayo inatakiwa kutamaniwa.

**Tafakari na majadiliano:**
Jadili mti wa malengo na malengo yapi mngependa kuyafanyia kazi.

**Uhifadhi:**
Nakili miti yote miwili (ya matatizo na malengo) kwenye kipande kidogo zaidi cha karatasi na kihifadhi kwenye mafaili ya kikundi.

# Sura ya 5: Tunawezaje kupanga shughuli?




Sura hii inatoa mawazo kwa ajili ya vielekezi rahisi vya kutumia wakati wa kupanga na kuandaa bajeti kwa ajili ya shughuli za kikundi. Kabla ya kuanza kupanga, kikundi kinatakiwa kiwe kimeshajiwekea malengo kwa ajili ya kazi yao, kwa mfano kwa kutumia moja ya vielekezi vilivyobainishwa kwenye sura ya 4.

**Miongozo:**

- Hamasisha watoto kubuni shughuli ambazo zinaweza kutekelezeka kwa kutumia fedha kidogo au zisizotumia fedha kabisa. Usiache shughuli zote za kikundi ziwe tegemezi kwa wawezeshaji wa nje.

- Kazi ya kupanga na kuandaa bajeti inaweza ikawa ya kuchosha kidogo. Hakikisha unaeleza vizuri kwa nini ni muhimu kupanga bajeti, na fanya vitu vya kufurahisha zaidi kabla, baada au wakati wa zoezi la kupanga na kuandaa bajeti.

- Kama unafanya kazi na watoto wasiojua kusoma na kuandika tumia michoro na alama badala ya maandishi.

- Kama kuna watoto wasioona kwenye kikundi, hakikisha kwamba shughuli zote zinazofanywa kwa njia ya maandishi zinaelezewa vizuri. Kama kuna watoto wenye matatizo ya kusikia kwenye hicho kikundi, andaa utaratibu wa ukalimani wa lugha ya alama au tumia maandishi na michoro.

**Kamusi**

*Bajeti:* Kadirio la kiasi gani cha fedha kitahitajika katika kugharamia utekelezaji wa kitu fulani, kwa mfano, utekelezaji wa mojawapo ya shughuli za kikundi.

*Andiko la mradi:* Maelezo yaliyopangiliwa vizuri ya mradi au shughuli fulani yanayotumika wakati wa kuomba msaada.

## 5.1 Kuandaa mpango wa shughuli

**Lengo:** Kushirikisha watoto katika kuandaa mpango kwa ajili ya kutekelezea shughuli za kikundi ndani ya muda uliopangwa.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama /ubao mweusi na chaki

**Muda:** Saa 1-2, kulingana na idadi ya shughuli zinazotarajiwa kupangwa.

**Kazi:**

1) Wafahamishe washiriki kuhusu dhana ya upangaji. Jadili: Nini maana ya upangaji na kwa nini tunahitaji kupanga? (Kwa mfano, kupanga ni kuamua kuhusu shughuli zipi zifanyike na kwa wakati gani. Huwa tunapanga ili kuhakikisha kwamba tunajua nini cha kufanya, na wakati gani wa kufanya kitu hicho, tunahitaji vitu gani kwa ajili ya kufanya kitu hicho na ni nani atahusika.)

2) Pitia malengo yaliyofafanuliwa na kikundi (tazama sura ya 4). Acha washiriki wakubaliane juu ya lengo moja ili kupanga shughuli kwa ajili ya kulitekeleza. Weka muda wa kutekeleza lengo hilo (kwa mfano, mwezi 1, miezi 6, mwaka 1).

3) Chora jedwali kama inavyoonyeshwa hapo chini kwenye flipchati au kwenye ubao. Andika lengo kwenye kisanduku cha kwanza.

| Kwa nini?<br>Lengo | Nini?<br>Shughuli | Jinsi gani?<br>Maandalizi (kwa mfano, vifaa) | Wapi? | Lini? | Nani anawajibika? | Nani anahusika? | Viashiria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *Mfano: Kupanua ufahamu kuhusu haki ya watoto ya kupata elimu.* | *Kuonyesha igizo kwa wazazi kuhusu watoto wasiosoma* | *Maandalizi ya mchezo wa kuigiza Kuwaalika watu kwa kuwaambia tu kwa mdomo* | *Kwenye ukumbi wa jumuiya* | *Tarehe 10 Oktoba 2010* | *Kiongozi wa kikundi cha tamthiliya* | *Kikundi cha tamthiliya* | *Washiriki wote wa kikundi kukaribisha wazazi na majirani.* |


4) Wagawe washiriki katika vikundi vidogo vidogo. Waambie wafikirie kwa makini kuhusu shughuli ambazo wangependa kuzifanya. Kwa kila shughuli, wajadili uwezekano wa kufanyika kwa shughuli hiyo – Je inawezekana kufanyika shughuli hiyo: Je tuna muda wa kutosha kufanya shughuli hiyo? Je tunayo maarifa ya kuifanya shughuli hiyo au tunaweza kuyapata maarifa haya mahali pengine? Je tuna rasilimali zinazohitajika?

5) Ruhusu vikundi viwasilishe shughuli zao ambazo zimefuzu jaribio la 'uwezekano wa kufanyika'. Andika au chora kila shughuli kwenye jedwali.

6) Acha washiriki waamue shughuli zipi wazifanyie kazi, ama kwa njia ya majadiliano na kufikia muafaka au kwa kutoa kipaumbele kwa mambo ya muhimu kwanza (tazama sura ya 1). Kwa shughuli iliyochaguliwa, jadili na jaza kila kisanduku kwenye jedwali. Mwambie kila mshiriki aandike majukumu yake.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:** Tunza mpango huu na hakikisha unafanya ufuatiliaji.

## 5.2 Upangaji wa shughuli – mwelekeo



**Lengo:** Kuwashirikisha watoto katika kupanga shughuli moja moja na kuwahamasisha kupitia mchakato wa shughuli fulani na kutazamia changamoto zinazoweza kujitokeza.

**Kikundi:** Ni vizuri wasizidi watu 10. Kama kikundi ni kikubwa zaidi ya watu 10, kigawe kwenye vikundi vidogo vidogo na kitake kila kikundi kipange shughuli moja.

**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama /ubao na chaki.

**Muda:** Saa 1-2.

**Kazi:**

1) Kwenye flipchati, chora mchoro katikati ya karatasi ukionyesha kazi unazotaka kuzifanya. Kwa upande wa kushoto, chora barabara inayoelekea kwenye kazi, kwa upande wa kulia chora barabara inayotoka kwenye kazi.

   Jadili:

   - Tunatakiwa tufanye nini kabla ya kazi? Inatakiwa ifanywe kwa muda gani na ni nani atakayeifanya? Andika au chora hili kwenye barabara upande wa kushoto wa kazi.

   - Tunahitaji vitu gani vingine tofauti ili kuweza kufanya shughuli yenyewe? Nani ataifanya? Andika au chora hili juu ya mchoro wa shughuli yenyewe.

   - Tunatakiwa kufanya nini baada ya shughuli hii? Nani atafanya na ni wakati gani inatakiwa kufanyika? Andika au chora hili kwenye barabara iliyo upande wa kulia wa shughuli.

   - Je, tunaweza kukabiliana na changamoto zozote wakati wa kutekeleza hili? Tufanye nini ili kuzikabili? Andika hili chini ya mchoro wa shughuli.

**Tafakari na majadiliano:**
Jadilini mapango wenu hakikisheni kuwa kila kitu kimejadiliwa. Waambie washiriki waandike majukumu yao.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Itunze ramani ya shughuli na fanya ufuatiliaji

## 5.3 Kuandaa bajeti

**Lengo:** Kuwashirikisha watoto kwenye kuandaa bajeti ya shughuli na kuwapa hamasa ya kufikiria kuhusu njia tofauti za kukusanya rasilimali.

**Kikundi:** Wasizidi watoto 10 kwenye kila kikundi

**Vifaa:** Flipchati na kalamu.

**Muda:** Saa1.

**Kazi:**

1) Wafahamishe washiriki kuhusu wazo la bajeti – nini maana yake na kwa nini inaandaliwa? (Kwa mfano, bajeti ni kadirio la gharama za kufanya kitu fulani, kama vile, shughuli ya kikundi).

2) Waambie washiriki wachore jedwali kama hili lifuatalo. Kwenye safu ya kwanza orodhesha vitu vinavyohitajika kwa ajili ya kufanyia kazi mnayopanga. Kwa kila kitu jadilini ikiwa mtahitajika kukinunua au kama mnaweza kukiazima au kutolewa bure na mtu. Kama mtahitajika kukinunua, kadiria gharama yake. Kama hufahamu gharama yake, fuatilia na malizia kuandaa bajeti hiyo kwenye mkutano ujao.

| Jina la shughuli (kwa mfano: mkutano wa wazazi) | | | |
|---|---|---|---|
| Maelezo ya vitu vinavyohitajika | Gharama | Aina ya kitu | Mtoaji (kwa mfano mtu yeyote kwenye jamii, serikali ya mtaa au shirika) |
| Mfano chai na biskuti (watu 40) | Shilingi 40,000 | | Asasi zisizo za kiserikali zilizopo katika eneo hilo |
| Viti | | Viti | Shule |
| Chumba cha mkutano | | Chumba cha darasa | Shule |

**Tafakari na majadiliano:**
Kama gharama ya bajeti iliyoandaliwa ni kubwa zaidi kuliko rasilimali zinazopatikana, usikate tamaa, ila jadili njia mbadala za kumalizia shughuli hiyo.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Itunze bajeti kwa ajili ya kufanya marejeo baadaye.

## 5.4 Upatikanaji wa fedha – kuandika pendekezo la mradi

**Lengo:** Kuwawezesha watoto kuandika miradi rahisi au pendekezo la shughuli kwa ajili ya kupatia fedha.

**Kikundi:** Wasizidi watoto 10 katika kila kikundi

**Vifaa:** Karatasi, kalamu

**Muda:** Muda utakaotumika kwa ajili ya shughuli hii utategemeana na kikundi chenyewe na kiasi gani wazo la shughuli hiyo litakuwa limechambuliwa vizuri. Watoto wanaweza kuhitajika kutumia muda mfupi kabla mikutano haijaisha ili kutafuta taarifa.

**Kazi:**

1) Wafahamishe washiriki kuhusu wazo la pendekezo la mradi (maelezo ya muundo mzima wa mradi au shughuli inayofanyika wakati wa kuomba msaada kwa mtu)


2) Waambie washiriki washirikiane kwa pamoja kuandika au kukupa vitu vinavyohitajika katika kuandika pendekezo la mradi kwa ajili ya shughuli:
    - Kwa nini? Nini lengo la shughuli au mradi?
    - Jinsi gani? Shughuli gani zitajumuishwa?
    - Lini? Shughuli au mradi huo utafanyika kwa muda gani?
    - Nani? Nani atakuwa na jukumu gani?
    - Itagharimu shilingi ngapi? Ambatanisha bajeti.
    - Utatathmini vipi kama kazi au mradi ulifanyika vizuri au la?

| lengo la shughuli | Jinsi gani shughuli itafanywa | Lini na kwa muda gani shughuli itafanywa | Nani atakuwa na majukumu gani | utathmini /kiwango cha utekelezaji wa shughuli |
|---|---|---|---|---|
| • | • | • | • | • |
| • | • | • | • | • |
| • | • | • | • | • |

3) Jadilini nani atakuwa tayari kufadhili mradi uliopendekezwa. Amua nani atapeleka au kuleta pendekezo la mradi.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Wakati wote tuma nakala za pendekezo la mradi kwa watu wanaoweza kutoa misaada.

# Sura ya 6: Tunawezaje kufanya shughuli za kikundi?




Sura hii ya kielekezi hiki inatoa mwangaza kuhusu njia ambazo zinaweza kutumika pale watoto wanapotaka kufanya jambo fulani ili kutimiza mahitaji yao. Lakini bado kuna mawazo mengi ambayo hayajazungumziwa hapa, na mara nyingi watoto wenyewe watakuja na mawazo yao wenyewe.

Mada za shughuli zinazofanywa na vikundi vya watoto ni pana, na hivyo vielekezi vinavyotolewa kwenye sura hii ni mawazo ya jumla tu.

**Miongozo:**

- Epuka vitendo vya kishari au kisiasa ambavyo vinaweza kuhatarisha usalama wa watoto.
- Hakikisha kwamba watoto wanasaidiwa na kufuatiliwa wakati wakitekeleza shughuli zao.
- Tazamia na uwe tayari kukabiliana na masuala magumu. Katika mchakato wa kutekeleza shughuli mbalimbali za kikundi, unaweza kukutana na watoto ambao wako katika mazingira magumu sana na wanahitaji msaada mkubwa. Tafuta mtu unayeweza kuwaelekeza kwake (tazama sehemu ya 3.7).
- Fikiria ikiwa kuwashirikisha watoto katika kutatua masuala yao wenyewe kunaweza kuhatarisha usalama wao kwenye familia au jamii zao. Hakikisha kwamba wazazi na wadau wengine (kwa mfano, walimu na viongozi wa kijamii) wanapewa taarifa na kushirikishwa kwenye michakato mbalimbali ili kuhakikisha wanaelewa na kuunga mkono azma na shughuli za kikundi.

**Kamusi:**

Mtoa maamuzi: Mtu, taasisi au kikundi kinachohusika katika ufanyaji maamuzi yanayoathiri maisha ya watu wengine – kuanzia ngazi ya chini kabisa, mpaka ya kitaifa au kimataifa. Watu hawa wanaweza kuwa wazazi, viongozi, maafisa wa kiserikali, wanasiasa, n.k.

*Ufahamu:* Kutambua na kuwa na taarifa kuhusu jambo fulani.

*Utetezi:* Kujaribu kushawishi michakato na maamuzi mbalimbali ili kuleta mabadiliko fulani.

*Elimu rika:* Shughuli za kuelimisha rika – watoto wenye umri unaolingana au unaotofautiana kidogo au watoto walio kwenye mazingira yanayofanana.

## 6.1 Kupata na kushirikiana taarifa katika kikundi

**Lengo:** Kuhamasisha watoto kutafuta taarifa mbalimbali na kuwashirikisha wenzao katika taarifa hizo.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Hakuna

**Muda:** Saa 1 kwa ajili ya kupanga na kufuatilia kwenye vikao vinavyofuata.

**Kazi:**

1) Amua aina gani ya taarifa kikundi kinapendelea. Hii inaweza kuwa taarifa kuhusu haki za mtoto, taarifa kuhusu hali ya watoto kwenye jamii, taarifa kuhusu mambo mapya yanayotokea kwenye jamii (yanayohusu watoto), taarifa kuhusu mada dhahiri (kwa mfano, vurugu, udhalilishaji au afya) n.k.

2) Jadilini, kama kikundi, kuhusu njia zitakazowawezesha kupata taarifa.
   Mifano:

   - Kufanya mazungumzo ya kawaida na watoto wa rika moja na watu wengine kwenye jamii.

   - Kusoma taarifa mbalimbali kwenye mbao za matangazo zilizopo shuleni au sehemu mbalimbali kwenye jamii. Kama hakuna mbao za matangazo au ikiwa taarifa zinazobandikwa hazibadilishwi kila mara ili kwenda na wakati, waombe wakuu wa shule na ofisi za serikali kuweka mbao za matangazo na kuweka taarifa zinazokwenda na wakati.

   - Kutana na watu wanaoweza kutoa msaada. Tengenezeni orodha ya watu wanaohusika wanaoweza kutoa msaada walioko kwenye jamii (kwa mfano, wazee na viongozi wa jamii, wataalamu, watu kutoka Taasisi zisizo za kiserikali, maafisa wa serikali,polisi, watu kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali, wajumbe wa baraza la usuluhishi na mabaraza ya kata,) ambao wanaweza kualikwa kuja kutoa taarifa ambazo kikundi cha watoto kinapaswa kufahamu. Jadilini namna ambavyo mialiko inapaswa kuandaliwa.

- Kushiriki kwenye mikutano ya kijamii. Endesha mjadala kuhusu nini kinaweza kufanyika ili kuhakikisha kwamba baadhi ya wawakilishi wa kikundi wanaweza kuhudhuria kwenye mikutano ya kijamii inayowahusu watoto. Jadilini namna ambavyo taarifa itafikishwa kwa wanachama wengine wa kikundi baada ya mikutano hiyo.

- Kusoma magazeti. Baadhi ya washiriki wanaweza kupata magazeti na hivyo wanaweza kukata au kunakili kurasa za magazeti zenye taarifa muhimu kwa ajili ya kuwashirikisha wengine kwenye kikundi.

- Kusikiliza redio au kutazama runinga. Wanachama wa kikundi ambao wanaweza kupata habari kutoka vyombo hivi vya habari wanaweza kuandika mahali masuala muhimu yanayojitokeza na kuwataarifu wengine kwenye mikutano itakayofanyika.

- Kutafuta kwenye mtandao. Baadhi ya wanachama wanaweza kupata bahati ya kutumia mtandao na wanaweza kutafuta taarifa zinazofaa, na kuzichapa au kuziandika mahali na kuwapatia wenzao taarifa hizo baadaye.

3) Gawa majukumu kwa wanakikundi wote.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Kama inawezekana, hifadhi taarifa zote zilizokusanywa, kwa mfano, kwenye mafaili ya kikundi au kwenye mabango au kwenye vijarida.

## 6.2 Kujifunza haki za mtoto

**Lengo:** Kujifunza kuhusu haki za mtoto ni njia muhimu ya kuwawezesha watoto. Lengo la kielekezi hiki ni kuhamasisha watoto kujifunza haki zao.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Nakala za Mikataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto, kwa mfano, toleo rahisi la Mkataba huo kwa ajili ya watoto linalopatikana kwenye tovuti ya Umoja wa Mataifa (weka kielezo).

**Muda:** Inategemeana na shughuli yenyewe.

**Kazi:**

1) Kuufahamu Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa haki za mtoto.

- Wajulishe watoto kuhusu dhana ya haki za mtoto na mkataba kuhusu haki za mtoto, kwa kutumia toleo rahisi la mkataba huo lililoandikwa kwa ajili ya watoto (tazama uk. wa 89).
- Mwambie kila mshiriki achague haki tatu anazoona ni za muhimu sana. Halafu waambie washiriki wajiunge kwenye vikundi vya watu wanne wanne na kujadili haki ambazo kila mtu amezichagua kuwa za muhimu zaidi. Kubalianeni juu ya haki 3 kwa pamoja kama kikundi.
- Ruhusu kila kikundi kiwasilishe kazi yao.
- Jadilini: Je, ilikuwa vigumu kukubaliana kuhusu haki hizo tatu? Kwa nini, kwa nini hapana? Nini maana ya 'haki'? Majukumu gani yanaambatana na haki?

2) Kufahamu sheria zinazohusu masuala ya watoto nchini Tanzania

- Wafahamishe washiriki kuhusu Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ukitumia toleo la sheria hiyo lililoandikwa kwa lugha nyepesi (tazama uk. wa 90).
- Gawa washiriki kwenye makundi na endesha mjadala na wasaidie kutambua mambo 3 yaliyo kwenye sheria hiyo wanayoona ni muhimu zaidi.
- Ruhusu kila kikundi kiwasilishe kazi yake.
- Jadilini: Hali kwenye jamii yetu ikoje ikilinganishwa na sheria hii inavyosema? Nini kinaweza kufanyika ikiwa watu wanavunja sheria hii?

3) Kujadili kuhusu umri na haki

- Gawa washiriki katika vikundi vya watoto 4-6.
- Kitake kila kikundi kujadili umri gani mtu anapaswa kuwa nao ili aweze kufanya shughuli zifuatazo:
- Kwenda shule
- Kuamua nini cha kujifunza
- Kuamua mahali pa kuishi
- Kufanyia kazi nyumbani
- Kufanya kazi mbali na nyumbani
- Kuchagua dini ya kuabudu
- Kuwa na marafiki
- Kuoa au kuolewa
- Kwenda vitani
- Kupiga kura
- Kutoa maoni yake kuhusu maamuzi ndani ya jamii
- Kutoa maoni yake kuhusu maamuzi yanayohusu nchi kwa ujumla
- Kusikilizwa na watu wazima
- Mengineyo (washiriki wanapaswa kufikiria maswali yao wenyewe)
- Acha kila kikundi kiwasilishe kazi yao.
- Jadilini: Je, kuna tofauti kubwa sana kati ya vikundi hivi? Unadhani kwamba watu wazima wangejibu maswali haya kwa namna tofauti? Je, unadhani kwamba watoto waishio kwenye jamii au nchi nyingine wangejibu kwa namna tofauti pia? Je, Mkataba wa Haki za Mtoto unasema chochote kuhusu masuala hayo, unasemaje?

4) Kujadili haki za mtoto kwenye jamii zetu.

- Gawa washiriki kwenye vikundi vya watu 4-6.
- Kiambie kila kikundi kipitie toleo la mkataba wa haki za mtoto lilioandikwa kwa lugha nyepesi.
- Jadilini: Ni haki zipi ambazo siku zote huwa zinaheshimiwa kwenye jamii yetu? Ni zipi ambazo mara nyingine haziheshimiwi? Na ni zipi huwa zinaheshimiwa kwa nadra sana?
- Acha vikundi viwasilishe kazi zao.
- Jadilini: kwa nini baadhi ya haki haziheshimiwi siku zote? Nini kifanyike kuhusu suala hilo?

5) Jifunze kutoka kwenye mtandao.
   Kama kikundi kinaweza kupata na kutumia mtandao, kitembelee tovuti ya vijana ya UNICEF kuhusu haki za mtoto: http://www.unicef.org/rightsite/433.htm.

**Tofauti:**

Vitendo hivi vinaweza pia kufanywa na vijana au watu wazima ili kuleta ufahamu kuhusu haki za mtoto.
Endapo unafanya kazi na vikundi visivyojua kusoma na kuandika, wasilisha Mkataba wa Haki za Mtoto kwa kuzungumza na chora vielezo vya haki hizo.

## 6.3 Kutoa maoni kuhusu mipango ya mitaa, sheria ndogondogo , na maamuzi mengine

**Lengo:** Mipango ya mitaa, sheria ndogondogo, na maamuzi mengine ya kisiasa au kiutawala mara nyingi huathiri maisha ya watoto. Lengo la kielekezi hiki ni kuwawezesha watoto kuchanganua na kutoa maoni kuhusu maamuzi yanayowaathiri.

**Ukubwa wa kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa, kigawe katika vikundi vidogo vya watoto 6-8.

**Muda:** Saa 2

**Vifaa:** Flipchati, karatasi, kalamu za kutia alama na za kawaida.

**Kazi:**

1) Wasaidie washiriki katika kutambua maamuzi ya muhimu kwenye jamii (kwa mfano, kwa kupitia taarifa zinazobandikwa kwenye mbao za matangazo za jamii, taarifa zinazotolewa na ofisi za serikali za mitaa, nk). Andika kwenye flipchati au ubao maamuzi ambayo mngependa kuyajadili.

2) Waambie washiriki wa kila kikundi wafanye mjadala kuhusu yapi yatakuwa matokeo ya maamuzi hayo kwenye jamii zao na jaza jedwali lililopo hapo chini. Jadilini vyote – faida na madhara, na mwishoni kubalianeni kuhusu wazo moja (kwa mfano, Tunaunga mkono wazo hili, hatuungi mkono wazo hili, tunaunga mkono wazo hili lakini mambo fulani fulani yanapaswa kutazamwa upya)

| Uamuzi | Faida kwa watoto | Madhara kwa watoto | Wazo letu kuhusu maamuzi hayo |
|---|---|---|---|
| *Kwa mfano:*<br>*Kuanzisha kituo cha maji/kisima katikati ya vijiji viwili* | *Upatikanaji wa maji safi*<br>*Upatikanaji wa maji kwa mwaka mzima* | *Umbali mrefu wa kutembea kufuata maji*<br>*Usalama mdogo wakati wa kuchota maji* | *Vituo vya maji havina budi kujengwa kwenye kila kijiji* |

3) Acha kila kikundi kiwasilishe kazi yake.

4) Jadilini mawazo tofauti na mkubaliane kuhusu mawazo ya kuwapelekea watoa maamuzi. Jadilini namna ya kuwasilisha mawazo yenu (kwa maandishi, kupitia vikao, kwa njia ya igizo, kwa njia ya wimbo, n.k). Kama mtaamua kuwasilisha wazo lenu kwa njia ya maandishi, hakikisheni mnajumuisha:
   - Utambulisho wenu kama kikundi (jina la kikundi, idadi ya wanachama, umri wao, jinsi n.k.)
   - Wazo lenu kama kikundi
   - Hoja zenu
   - Mapendekezo yenu ya nini kifanyike kuondokana na hali hiyo

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Hifadhi majedwali au yanakili kwenye mafaili.

## 6.4 Kuinua kiwango cha ufahamu katika jamii

**Lengo:** Kupanga na kutekeleza shughuli za kuleta au kuongeza ufahamu.

**Ukubwa wa kikundi:** watoto 8-30
Muda: Inategemeana na shughuli itakayochaguliwa. Huchukua muda kuandaa kwa usahihi shughuli za kuleta ufahamu, hivyo huna budi kutenga vikao kadhaa vya kikundi kwa ajili ya maandalizi.

**Vifaa:** Vifaa vya kutumia vitategemeana na aina ya shughuli inayofanyika.

**Kazi:**

1) Endesha mjadala mfupi kuhusu dhana ya ufahamu (kwa mfano, ufahamu ni utambuzi na uelewa wa taarifa kuhusiana na jambo fulani). Jadilini na kubalianeni kuhusu mada mnayotaka kuongeza ufahamu juu yake na ujumbe mkuu wa shughuli zinazofanyika kwa ajili ya kutoa ufahamu.

2) Jadilini kwa kina kuhusu kanuni zitakazotumika kwa ajili ya kuleta ufanisi katika kuongeza ufahamu.
   *Mifano:*
   Tambulisha kundi la kijamii mnalolilenga – hii itafanya utungaji wa ujumbe kuwa rahisi zaidi.
   Fanya ujumbe wenu kuwa mfupi na rahisi kueleweka.
   Tumia maelezo na mifano hai.
   Pendekeza ufumbuzi

3) Jadilini kwa kina kuhusu njia tofauti za kuongeza ufahamu.
   *Mifano:*
   - Hadithi. Andikeni au tungeni hadithi inayoendana na mada iliyochaguliwa au tumieni hadithi ya kitamaduni yenye ujumbe unaohusiana na mada mnayotaka kuongeza ufahamu juu yake. Alikeni watu (kwa mfano, watu wa rika moja) waje kusikiliza hadithi kwenye sehemu nzuri ya kusimulia hadithi, kwa mfano chini ya mti. Utakapomaliza kusimulia hadithi, karibisha maoni kutoka kwa wasikilizaji – wameionaje hadithi yako? Je, wanaweza kutambua baadhi ya mambo yaliyotajwa kwenye hadithi hiyo na kuyahusisha na maisha yao wenyewe? Je, wahusika wa kwenye hadithi wangeweza kuchukua nafasi nyingine tofauti na zile walizochukua kwenye hadithi hiyo?

- Igizo. Andaeni onyesho au igizo kuhusu mada iliyochaguliwa. Igizo linaweza kuonyesha tatizo na kutoa pendekezo la namna ya kulipatia ufumbuzi tatizo hilo. Igizo litakapokuwa limemalizika, karibisheni maoni kutoka kwa hadhira kuhusu ufumbuzi uliopendekezwa. Je, ufumbuzi huo utafanya kazi? Je, kuna ufumbuzi wa aina nyingine wa tatizo hilo? Njia nyingine mbadala ni kuigiza halafu kulisimamisha igizo ghafla, na kuitaka hadhira kutoa ufumbuzi wa tatizo linalozungumziwa.

- Nyimbo na ngoma. Andaeni ngoma na tungeni nyimbo zenu wenyewe zikilenga mada iliyochaguliwa. Ziwasilishe kwenye mikutano ya kijamii, mikusanyiko mbalimbali kwenye shule au matamasha mengine.

- Picha. Tengenezeni kazi ya sanaa, michoro, katuni au mabango – vyote vikilenga mada iliyochaguliwa na kutoa ujumbe wenu. Pia mnaweza kubandika picha hizi sehemu tofauti kwenye jamii (kwa mfano, kwenye mbao za matangazo) au mnaweza kuandaa tamasha la maonyesho na kualika watu kuja kuangalia picha na kazi hizo za sanaa.

- Vyombo vya habari. Jaribuni kupeleka kampeni yenu ya kuongeza ufahamu kwenye vyombo vya habari, kwa mfano, kwenye vituo vya redio, runinga au magazeti. Hili linaweza kufanyika kwa kuandika makala wenyewe au kwa kuwasiliana na waandishi wa habari.

- Video na picha. Kama mnaweza kupata kamera ya video au ya kawaida, mnaweza kutengeneza filamu zenu wenyewe au mfululizo wa picha zinazolenga mada iliyochaguliwa. Onyesheni kazi hizi kwenye mkutano wa kijamii au mkutano shuleni au andaa onyesho la picha. Hamasisha kufanyika kwa mjadala.

- Vipindi vya filamu. Kama mnaweza kupata filamu za kuelimisha, mnaweza kufanya mpango na kuandaa muda maalumu wa kuonyesha filamu kwenye mkutano wa kijamii au shuleni, ikifuatiwa na majadiliano.

- Gazeti au jarida. Kama kuna fedha za kutosha kutolea nakala, mnaweza kutengeneza gazeti au jarida lenu wenyewe, mkijumuisha makala, picha na matangazo yenu wenyewe. Kazi hii inaweza kutengenezwa kwenye kompyuta au kuandikwa kwa mkono.

- Midahalo ya umma. Andaeni mdahalo wa umma, kwa mfano kwa ajili ya wazazi kuhusu mada iliyochaguliwa. Alikeni wazungumzaji wa kuwasilisha mada au fanyeni mawasilisho wenyewe. Karibisheni washiriki watoe maoni yao.

4) Amueni shughuli za kufanya, andaeni mipango ya shughuli hizo (tazama sura ya 5 kuhusu upangaji) na muitekeleze.

**Tafakari na majadiliano:**

*Jadilini:* Tutawezaje kujua ikiwa kiwango cha ufahamu wa watu kimeongezeka baada ya kila shughuli za kuongeza ufahamu?
Fanya tathmini ya shughuli hiyo baada ya kuimaliza. Je, watu walikusikiliza? Kwa nini/kwa nini hapana? Mambo gani yalienda vizuri na yapi yanaweza kuboreshwa zaidi wakati ujao?

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**

Weka kumbukumbu ya shughuli za kuinua kiwango cha ufahamu kadiri inavyowezekana, kwa mfano kwa kuhifadhi picha, kukusanya mawazo waliyotoa watu, nk.
Hifadhi maelezo yaliyopatikana wakati wa kufanya tathmini.

## 6.5 Mazungumzo na watoa maamuzi

**Lengo:** Kuwawezesha watoto kutetea wenyewe masuala ambayo ni muhimu kwao na kuwashawishi watoa maamuzi.

**Muda:** Saa 2-3 kwa ajili ya kupanga. Muda wa utekelezaji utategemeana na shughuli zinazofanyika.

**Vifaa:** Kalamu na karatasi.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Kazi:**

1) Endesha mjadala kuhusu dhana ya mtoa maamuzi (kwa mfano, mtu, taasisi au kikundi kinachohusika katika utoaji wa maamuzi yanayoathiri maisha ya watu wengine). Jadilini kujua watoa maamuzi ni kina nani, kwa mfano kwenye familia, mashuleni, kwenye jamii na taifa kwa ujumla.

2) Jadilini malengo yenu kwa kufanya mazungumzo na watoa maamuzi – ni mambo gani ungependa wayafahamu au kuwataka wayafanye?

3) Tambueni watoa maamuzi ambao malengo yenu yanawahusu na jadilini wajibu wao na majukumu yao.
   Mfano wa watoa maamuzi:
   - Wazazi
   - Walimu wakuu
   - Viongozi wa kijamii (kwa mfano, viongozi wa dini, viongozi wa jamii, nk.)
   - Mabaraza ya mitaa/vijiji, kamati za maamuzi za mitaa/vijiji
   - Kamati za maendeleo za kata
   - Halmashauri za wilaya/manispaa
   - Madiwani
   - Wabunge
   - afisa ustawi wa jamii
   - polisi

4) Gawa washiriki kwenye vikundi vidogo na kiambie kila kikundi kifanye uchambuzi mdogo wa mmoja wa watoa maamuzi (Vigawie vikundi watoa maamuzi):

| Mada: | Mtoa maamuzi | Wajibu kuhusiana na mada | Ushawishi(Mdogo, wa kati au mkubwa) | Msimamo (Wanatetea, au wanakataa hoja) |
|---|---|---|---|---|
| *Mfano: Kukomesha mimba kwa watoto* | *Wazazi* | *Wanatoa uamuzi wa kumuoza mtoto* | *Mkubwa* | *Baadhi wanatetea, wengine wanapinga* |
| | *Walimu* | *Wanaweza kushawishi wazazi* | *Wa kati* | *Wanatetea* |
| | *Wabunge* | *Kutunga sheria* | *Mkubwa* | *Baadhi wanatetea, wengine wanapinga* |

5) Ruhusu kila kikundi kiwasilishe uchambuzi wake. Jadilini aina ya watoa maamuzi watakaozungumziwa – wale wanaotetea au wanaokataa hoja? Wale wenye ushawishi mdogo au mkubwa?

6) Pangeni shughuli ili kujua namna ya kuwaendea watoa maamuzi.

Mifano:

- Kusanyeni na toeni taarifa kwa wengine. Kama mnataka kufanya tatizo fulani kwenye jamii lifahamike kwa watoa maamuzi, ni wazo zuri kuhakikisha kuwa mnapata taarifa zinazokwenda na wakati kuhusu tatizo mnaloshughulikia. Jaribuni kuchunguza ni kwa kiasi gani tatizo hilo limesambaa, kwa kukadiria tu ni watu/watoto wangapi wameathiriwa na tatizo hilo, na baadhi ya athari ni zipi. Mpatieni mtoa maamuzi taarifa hiyo ama kwa maandishi au kupitia kikao.

- Fanyeni kikao. Pelekeni ombi kwa maandishi la kufanya kikao, mkimkaribisha mtu huyo kutembelea kikundi au kuomba kufanya naye kikao ofisini kwake. Hakikisheni mnaandaa kikao vizuri: Ni ujumbe upi mngependa kumpatia mtu huyo? Mifano yenu au hoja zenu ni zipi? Mnapendekeza ufumbuzi upi? Ni nani atazungumza naye?

- Andikeni barua. Kama ni vigumu kufanya kikao pamoja na mtoa maamuzi, mnaweza badala yake mkamwandikia barua, mkieleza hoja na nia yenu. Hakikisheni kuwa mnaeleza vizuri tatizo ni nini, sababu za tatizo hilo, mifano kadhaa, na mapendekezo yenu ya namna ya kutatua tatizo hilo.

- Tamko. Andaeni tamko linalowasilisha nia na mawazo yenu na acheni watoto wote wa kikundi watie saini tamko hilo. Mnaweza pia kuwaomba watoto wengine kwenye jamii watie saini zao kama watakubali. Tumeni tamko hilo kwa mtoa maamuzi au liwasilisheni kwenye mkutano.

- Shirikianeni na mashirika mengine. Endapo tatizo mnalojaribu kushughulikia ni kubwa au ni vigumu kumshawishi mtoa maamuzi aingie kwenye majadiliano nanyi, fikirieni namna mnavyoweza kushirikiana na mashirika mengine. Inaweza kuwa rahisi zaidi kupata nafasi ya kukaa kikao na mtu muhimu kama ataalikwa na kikundi zaidi ya kimoja.

**Tafakari na majadiliano:**
Fanya tathmini ya shughuli mliyoikamilisha. Je, mtoa maamuzi aliwasikiliza? Kwa nini/kwa nini hapana? Mambo gani yalienda vizuri na yapi yanaweza kuboreshwa zaidi wakati ujao?

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Hifadhi maelezo yaliyopatikana wakati wa kufanya tathmini.

## 6.6 Kutoa elimu rika

**Lengo:** Elimu rika ni shughuli inayohusisha watoto au vijana kuwaelimisha wenzao wa rika moja. Lengo la kielekezi hiki ni kuwawezesha watoto kupanga na kuandaa shughuli za uelimishaji rika. Angalia kama kuna uwezekano wa kupata mafunzo ikiwa kikundi kinataka kuitumia mbinu hii kwa kiasi kikubwa.

**Kikundi:** watoto 8-20

**Vifaa:** Inategemeana na shughuli zinazofanyika.

**Muda:** Inategemeana na shughuli iliyokubaliwa kufanyika, uhitaji wa kufanya mafunzo, nk.

**Kazi:**

1) Endesha mjadala kuhusu elimu rika – nini maana ya elimu rika? (kwa mfano, shughuli za kielimu pamoja na watu wa rika moja – watoto wenye umri mdogo kidogo au unaolingana na wetu)

2) Endesha mjadala ili kutambua mada ambazo kikundi kingependelea kutolea elimu rika.


3) Jadilini ikiwa mnahitaji ujuzi na taarifa zaidi kuhusu mada mliyochagua na jadilini kuhusu uwezekano wa kupata mafunzo.

4) Panga namna ya kutekeleza shughuli.
   - Nani? Bainisheni kikundi cha rika mnachotaka kuzungumza nacho na kujadili mahitaji yao.
   - Wapi? Chagueni eneo la kufanyia shughuli (kwa mfano, shuleni, sokoni, kanisani/msikitini/hekaluni, vyamani).
   - Namna gani? Mtawezaje kuhakikisha kwamba watoto wa rika lenu wanapatikana na shughuli zipi mtazifanya? Mifano ya shughuli ni:
   - Kusimulia hadithi
   - Vipindi vya maigizo na tamthiliya
   - Majadiliano ya kikundi yaliyoanzishwa kwa njia ya, kwa mfano, maswali, visa, mafumbo au chemsha bongo, Tamthiliya au mkusanyiko wa picha.
   - Mazungumzo yasiyo rasmi
   - Mtawezaje kupata majibu ya utekelezaji wa maazimio yenu kutoka kwa wenzenu wa rika moja?

**Tafakari na majadiliano:**
Fanyeni tathmini ya shughuli mliyofanya. Je, wanarika wenzenu walifurahia na waliwasikiliza? Kwa nini/kwa nini hapana? Mambo gani yalienda vizuri na yapi yanaweza kuboreshwa zaidi wakati ujao?

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**
Hifadhi maelezo yaliyopatikana wakati wa kufanya tathmini.

# Sura ya 7: Tunawezaje kufuatilia na kutathmini shughuli au michakato?




Sura hii inabainisha vielekezi vinavyotumika katika kufuatilia na kutathmini shughuli na michakato kwa kushirikiana na watoto.

Kazi ya kufuatilia na kutathmini hufanywa kwa malengo tofauti. Kwanza, inaweza kutusaidia kudhibiti na kufanya mambo yaende kulingana na mipangilio na matarajio yetu. Pili, inapofanywa kwa njia shirikishi husaidia washiriki kujifunza kutokana na uzoefu wanaopata. Tatu, shughuli za ufuatiliaji na ufanyaji tathmini zinazofanywa kwa njia shirikishi huweza kuwa motisha kwa ushiriki endelevu.

**Mwongozo:**

- Fanya tathmini ndogo ya kila shughuli baada ya kuimaliza ili kupata majibu kutoka kwa washiriki (kwa mfano, tathmini hali ya mwitikio wa watoto katika utekelezaji wa shughuli fulani au tathmini maoni yaliyoandikwa)

- Baada ya muda fulani unaweza kuhitaji kufanya ufuatiliaji wa kina zaidi ili kujua kama kazi yako inatoa matokeo uliyoyatarajia na kama uwezo wa kikundi unaendeleza kazi (kwa mfano kwa kutazama hali ya mabadiliko au kutumia shughuli ya mti wa kikundi).

- Kama kujua kusoma na kuandika ni tatizo kubwa kwa watoto, tumia michoro na fanya mawasilisho kwa njia ya mazungumzo badala ya maandishi.

- Kama kuna watoto wasioona kwenye kikundi, badili shughuli na jumuisha zaidi mijadala ya mazungumzo na hakikisha wanasaidiwa, kwa mfano katika kuandika maoni. Kama kuna watoto wenye matatizo ya kusikia kwenye kikundi, andaa utaratibu wa kutafsiri kwa lugha ya alama au tumia maandishi na michoro.

**Kamusi:**

Ufuatiliaji: Kufuatilia maendeleo ya shughuli au mchakato wakati ikiendelea kutekelezwa.

Tathmini: Uchanganuzi wa kina na wa hatua kwa hatua ili kubaini uimara na udhaifu wa shughuli au mchakato, mara nyingi hufanyika baada ya shughuli kumalizika.

Matokeo: Mabadiliko ya muda mrefu au makubwa yaliyotokana na shughuli au michakato.

# 7.1 Kupima hisia za watoto juu shughuli wanazofanya

**Lengo:** Lengo la kielekezi hiki ni kukusanya maoni ya washiriki kuhusu namna walivyochukulia shughuli wanazofanya. Kielekezi hiki kinaweza kutumika kila baada mkutano au shughuli.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama au chupa tupu/vyombo na mawe mengi kulingana na idadi ya washiriki.

**Muda:** Dakika 10 mwishoni mwa kila mkutano wa kikundi.

**Kazi:**
Tengeneza kipimo cha hali ya mwitikio – kipimo cha kupima maoni ya washiriki kuhusu shughuli tofauti zilizofanywa. Kipimo chenyewe kinaweza kutengenezwa kama jedwali kwenye flipchati au kwa kutumia makopo matupu.

**Kipimo cha Flipchati**

1) Chora jedwali kama lifuatalo na andika kila shughuli iliyofanywa wakati wa mkutano kwenye safu ya kushoto.

| Kazi | :-) | :-I | :-( | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| Mifano: | | | | |
| Michezo ya mawasiliano | x | | | |
| Kukutana na viongozi wa kijiji | | x | | |
| Kuandaa sherehe ya siku ya mtoto wa Kiafrika | x | | | |

2) Baada ya kila kazi ya kikundi, waambie washiriki waweke alama ya “x” kwenye kipimo kilichotengenezwa kama waliipenda shughuli sana, kwa wastani au hawakuipenda kabisa.

3) Washiriki wote wanapokuwa wameshaweka alama zao, fanya mjadala na washiriki wote unaohusu maamuzi yaliyofikiwa: Kwa nini unafikiri kwamba washiriki walipenda/hawakupenda hii shughuli? Andika maoni muhimu kwenye safu ya maoni.

**Kipimo cha chupa/kopo:**

1) Kwenye chupa mojawapo chora alama ya sura ya furaha, kwenye chupa ya pili chora sura isiyokuwa na huzuni wala furaha na kwenye chupa ya mwisho chora sura yenye huzuni.

2) Baada ya kila shughuli, mpe kila mshiriki jiwe moja dogo (au kifaa kingine kidogo) na waambie kila mmoja aweke kwenye chupa moja kulingana na jinsi alivyoipenda kazi hiyo: sana, kwa wastani au hakuipenda kabisa.

3) Washiriki wote wanapomaliza kuweka mawe yao kwenye hizo chupa, fanya mjadala wa pamoja kuhusu maamuzi yaliyofikiwa: Kwa nini unadhani kwamba washiriki wengi walipenda/hawakupenda hiyo shughuli?

4) Andika maamuzi na maoni yoyote muhimu.

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**

Tunza jedwali hili au maandishi haya.

## 7.2 Orodha ya shughuli zilizofanywa

**Lengo:** Orodha za shughuli zilizofanywa zinaweza kutengenezwa na mtu binafsi, au kikundi kinaweza kuwa na orodha yake iliyojazwa. Orodha ya maoni ijazwe na kikundi baada ya kila kazi kufanyika. Njia hii huwapa hamasa watoto kutafakari na kuandika ubora wa shughuli zinazofanyika na kutoa taarifa kwa undani zaidi kuliko ile ya kutumia kipimo cha hali ya mwitikio.

**Ukubwa wa kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Madaftari, kalamu.

**Muda:** Maandalizi ya saa 1, halafu baada ya hapo dakika 10 baada ya kila shughuli.

**Kazi: Maandalizi:**

1) Mwambie mshiriki mmoja atengeneze orodha ya viashiria (vigezo) vya shughuli nzuri. Kubalianeni viashiria visivyozidi 6, ama kwa kujadiliana na kufikia muafaka au kwa kupiga kura.

   *Mifano:*
   - *Inafurahisha.*
   - *Tunajifunza kitu.*
   - *Watu wazima hutusikiliza.*
   - *Kila mtu anashirikishwa.*

2) Tumia orodha hii kutengeneza muundo wenye maswali kwa ajili ya maoni. Kwa mfano, Muundo unaweza ukawa na mwonekano huu:

| |
|---|
| Jina la shughuli |
| Tarehe ya kufanya shughuli |
| 1) Je, tulifurahi? Kwa nini/Kwa nini hapana? |
| 2) Tulijifunza nini? |
| 3) Je, watu wazima walitusikiliza? |
| 4) Je, kila mtu alishirikishwa? Kwa nini/Kwa nini hapana? |
| 5) Maoni |

5) Tenga dakika 10 mwishoni mwa kila mkutano au shughuli kwa ajili ya watoto kujaza orodha ya maoni. Kama kujua kusoma na kuandika ni kikwazo kwao, basi wanaweza kuchora badala ya kuandika.

**Tafakari na majadiliano:**
Fuatilia orodha ya maoni kila wakati, kwa mfano kila baada ya miezi mitatu. Jadili: Ni shughuli zipi tulizifurahia sana, na zipi tulifurahia kidogo? Kwa nini? Tumejifunza nini kipindi kilichopita? Je, tuliitumiaje orodha ya maoni? n.k.

## 7.3 Picha za mabadiliko



**Lengo:** Kazi hii ingeweza kufanywa na kikundi cha watoto baada ya kufanya kazi nyingi kwa muda wa kipindi fulani. Hata hivyo inaweza isiwafae sana watoto wa umri mdogo lakini ikawanufaisha sana wale wa umri mkubwa. Lengo ni kuhamasisha watoto katika kutafakari kuhusu mabadiliko yanayoletwa na kazi wanazofanya na kuwafanya kuwa waangalifu na matokeo ya kazi hizo.

- ikiwa kikundi hakijafanya kazi nyingi sana zoezi hili laweza kutumika kuwasaidia wafikirie ni mabdiliko gaani wange penda kuyaona hapo baadae katika jamii yao kuhusu jambo wanalolishughulikia

**Kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watoto 6-8

**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama.

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wa kikundi wachore michoro ya shughuli zilizofanywa wakati wa kipindi cha (kwa mfano miezi 3 au sita) kwenye upande wa kushoto wa flipchati au kipande cha karatasi.

2) Waambie washiriki wa vikundi wajadili kama kazi hiyo ilileta mabadiliko yoyote kwao (mabadiliko chanya au hasi) kama watu binafsi, kwenye familia au jamii zao. Waambie wafikirie mifano hai. Kama mabadiliko yameonekana, inabidi wachore picha ili kufafanua hilo kwenye upande wa kulia wa karatasi karibu na mchoro wa shughuli.

3) Ruhusu vikundi viwasilishe kazi zao.

**Tafakari na majadiliano:**


Jadili:

- Je, shughuli zipi zilileta mabadiliko chanya? Kwa nini?
- Je, shughuli zipi zilileta mabadiliko hasi? Kwa nini?
- Tunawezaje kuhakikisha tunakuwa na mabadiliko chanya kwa siku zijazo?

**Uhifadhi wa kumbukumbu:**

Andika masuala muhimu. Hakikisha unafuatilia kama shughuli zimeleta mabadiliko hasi yasiyotarajiwa (kwa mfano, kama watoto wanapata matatizo kwenye familia zao baada ya kupata elimu kuhusu haki za mtoto na ushiriki ).

## 7.4 Uwezo wa kufuatilia – mti wa kikundi chetu



**Lengo:** Shughuli hii inaweza kufanywa na kikundi cha watoto baada ya kufanya shughuli nyingi kwa kipindi cha muda fulani, kwa mfano miezi 3-6. Lengo ni kufuatilia jinsi washiriki wanavyotathmini uwezo wa vikundi vyao wa kufanya maamuzi.

**Kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watoto 6-8.

**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama.

**Muda:** Saa 2. Shughuli inaweza kufanywa, kwa mfano, kila miezi sita ili kufuatilia maendeleo ya uwezo kwenye kikundi.

**Kazi:**

1) Endesha mjadala miongoni mwa washiriki kuhusu mambo yafuatayo: Zipi ni baadhi ya sifa za baraza la watoto linalofanya kazi kwa ufanisi. Orodhesha sifa 4 – 8 na jadilini mambo ambayo sifa hizi zinajumuisha. (Kwa mfano: Washiriki waliohamasika. Hamasa kubwa inaweza kumaanisha kuwa watu huudhuria mikutano, hushiriki na kujitolea kufanya kazi kati ya mikutano. Kuhamasika kwa kiwango kidogo kunamaanisha kwamba kiwango cha mahudhurio na ushiriki ni kidogo. Mifano mingine ya sifa inaweza kuwa kiwango cha watu wazima kuunga mkono masuala ya watoto, idadi ya shughuli zinazofanywa, idadi ya kesi zinazofikishwa mbele ya serikali ya mtaa, uongozi, utaratibu, ushirikiano ndani ya kikundi n.k.)


2) Waambie washiriki wa kila kikundi wachore mti wenye matawi makubwa 4-8 kulingana na idadi ya ubora waliyokubaliana nayo. Waambie washiriki wa vikundi vyote wajadili hali ya sasa ya kundi la watoto na kutoa alama kwa kiwango cha kuanzia 1-5. Kama kiwango kipo chini, wachore jani 1 kwenye tawi, kama kiwango kipo juu, wachore majani 5.

3) Ruhusu vikundi viwasilishe kazi zao.

**Tafakari na majadiliano:**

Jadili kikundi kingependa kuwa wapi, kwa mfano, baada ya miezi 6 kulingana na kila ubora na nini kinaweza kufanyika kufikia kiwango hiki. Andika tarehe hii kwenye michoro na ihifadhi miti hiyo ili kuipitia tena baada ya muda fulani (kwa mfano miezi 3 au 6). Jadili: Je, hali imebadilika? Unaweza kuviambia vikundi vijadili tena na kuchora majani ya ziada kwa kutumia rangi tofauti.

# Sura ya 8: Tunavyoweza kutunza kumbukumbu za michakato na za kazi



Uhifadhi wa kumbukumbu za kazi ni muhimu kwa ajili ya kujikumbusha masomo yaliyofundishwa wakati wa shughuli na kusherehekea mafanikio yako, kuchangia uzoefu wako na watu wengine katika jumuiya au vikundi vingine vya watoto, na kuelezea kitu gani ulichofanya katika kuonyesha shukrani kwa watu au taasisi iliyokusaidia.

**Mwongozo:**

- Usitumie muda mwingi sana katika kutunza kumbukumbu. Teua vile vitu ambavyo ni  muhimu kuliko vyote.

- Shirikisha watoto katika shughuli za uhifadhi wa kumbukumbu.

**Kamusi:**

Ripoti maelezo: Hii ni ni ripoti inayoelezea shughuli ulizozifanya kwa muda wa kipindi fulani.

Ripoti ya matumizi ya fedha: Ripoti ya matumizi ya fedha ni ripoti inayoelezea jinsi ulivyotumia fedha (na rasilimali nyingine) katika muda wa kipindi fulani.

## 8.1 Kuandika ripoti

**Lengo:** Kuhifadhi maelezo ya shughuli zote na matokeo yake na kupeleka kwa watu waliosaidia kikundi cha watoto (kwa mfano, wawezeshaji)

**Ukubwa wa kikundi:** Kikundi kidogo cha watoto wenye umri mkubwa.

**Vifaa:** karatasi na kalamu au kompyuta na mashine ya kupiga chapa.

**Kazi:**

**Ripoti Maelezo**

Ripoti Maelezo ni ripoti inayoelezea shughuli zote ambazo umezifanyika kwa muda wa kipindi fulani. Ripoti hii inaweza kuandaliwa kwa muundo huu:

- Taarifa za kweli (kwa mfano jina la kikundi cha watoto, jina la shughuli zinazofanywa, ripoti ya kila baada ya kipindi fulani)
- Shughuli. Eleza shughuli zinazofanywa katika kipindi fulani.
- Matokeo. Eleza shughuli hizo zilitoa matokeo gani na yalipokelewaje na watoto pamoja na watu wengine.
- Masomo yaliyofundishwa. Eleza ulijifunza nini kutoka kwenye hizo shughuli.
- Changamoto. Eleza changamoto ulizokabiliana nazo, kama zipo.
- Mwelekeo. Kwa ufupi elezea mwelekeo wako utakuwaje katika kipindi kijacho.

Waambie watoto watoe maoni kwa kila hoja na teua kikundi kidogo zaidi cha watoto kiandike ripoti binafsi.

**Ripoti ya matumizi ya fedha**

Kama umepokea fedha kutoka kwa mtu fulani kwa ajili ya kufanyia shughuli zako, unatakiwa kuandaa ripoti ya matumizi ya fedha. Ripoti hii ya matumizi ya fedha inatakiwa iakisi bajeti yako (tazama sehemu ya 5.3)

| Jina la kazi | | | |
|---|---|---|---|
| Vifaa | Gharama zilizokadiriwa | Gharama halisi | Maoni |
| | | | |

## 8.2 Uhifadhi wa kumbukumbu kwa ajili ya kikundi

**Lengo:** Kudumisha hamasa miongoni mwa wanachama wa kikundi kwa kuhifadhi kumbukumbu  na kukumbuka shughuli zilizofanyika.

**Ukubwa wa kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watoto 6-8

**Vifaa:** Flipchati, kalamu za kutia alama, picha za shughuli kama zitapatikana, masalio (kwa mfano, magazeti, takataka, uchafu mwingine wa asili), utepe wa kufunikia au gundi.

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wa kila kikundi watengeneze bango linaloelezea shughuli au mchakato uliofanywa na kikundi kwa kutumia vifaa vinavyopatikana. Wahamasishe washiriki waelezee shughuli hizo wenyewe kwa hisia zao kama washiriki na hisia za watu wengine.

2) Ruhusu kila kikundi kiwasilishe kazi yake. Kama inawezekana, bandika mabango ukutani.

## 8.3 Uhifadhi wa kumbukumbu kwa ajili ya jamii

**Lengo:** Kufikisha taarifa zinazohusu kazi za vikundi kwa watu wengine kwenye jamii.

**Ukubwa wa kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watoto 6-8

**Vifaa:** Kulingana na shughuli inayofanywa

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**


1) Endesha mjadala, miongoni mwa washiriki kuhusu mambo yafutayo:
   - Tungependa kuwashirikisha watu wengine katika uzoefu gani?
   - Ni watu gani tungependa kuwalenga? (Kwa mfano, watoto wengine au jamii kwa ujumla)
   - Tunapaswa tutumie njia gani?

   Mifano ya njia za kutumia:
   - Mikutano. Alika wanajamii stahiki kwa ajili ya mkutano wa kutoa taarifa na waeleze kuhusu shughuli zako, mafundisho watakayopata, changamoto na mipango ya baadaye. Karibisha maoni.

   - Magazeti ya ukutani. Tengeneza gazeti la kubandika ukutani lenye makala zinazohusu kazi, picha, na kalenda ya shughuli zako na libandike kwenye ubao wa matangazo wa jumuiya au wa shule au sehemu nyingine kwenye jamii ambapo watu wataweza kuliona.

   - Majarida. Tengeneza jarida lenye makala yanayohusu shughuli zenu, picha na kalenda yenu ya shughuli mnazofanya na sambaza kwa walengwa katika jamii.

# Sura ya 9: Tunawezaje kuimarisha mchango wa watu wazima katika ushiriki wa mtoto?



Kikwazo kikubwa katika ushiriki wa mtoto ni wasiwasi miongoni mwa watu wengi wazima dhidi ya dhana hiyo. Mara nyingi watu wazima hufikiri kwamba watoto wana maarifa kidogo au uzoefu mdogo sana wa kuwawezesha kushiriki, au ushiriki wa mtoto unaenda kinyume na mila na desturi za jamii.

Sura hii inatoa baadhi ya vielekezi vya namna ya kuongeza uelewa kuhusu ushiriki wa mtoto miongoni mwa, kwa mfano, maafisa wa serikali, viongozi wa kijamii, viongozi wa kidini, walimu na wazazi. Vielekezi hivi vinaweza kutumika wakati wa mikutano au warsha mbali mbali. Chagua vielekezi ambavyo unaona vinafaa.

**Miongozo:**

- Teua watu ambao watakuwa 'mabalozi' katika jamii wanaounga mkono ushiriki wa mtoto na ambao wako tayari kujaribu kushawishi wengine.

- Omba ridhaa ya wazazi ya ushiriki wa watoto wao kwenye kikundi cha watoto.

- Hakikisha kwamba unawapa taarifa wazazi kuhusu kinachoendelea kwenye kikundi cha watoto, na wahusishe wazazi kwenye mijadala.

- Wataarifu pia watu wazima wengine muhimu (kwa mfano, walimu na viongozi wa kijamii) kuhusu kazi zinazofanyika kwenye kikundi cha watoto, maendeleo yenu pamoja na changamoto zinazowakabili.

- Jadili na watoto ni jinsi gani wataweza kuwashawishi watu wazima kuondokana na wasiwasi juu ya ushiriki wao kwa njia inayokubalika kitamaduni.

- Kama unafanya kazi na vikundi vya watu wazima wasiojua kusoma wala kuandika, tumia njia ya majadiliano na michoro kuliko maandishi.

- Kama kuna wasioona miongoni mwao, tumia njia ambazo zitajumuisha mazungumzo zaidi na hakikisha kuwa wanasaidiwa, kwa mfano, wakati wa kupiga kura au kuandika maoni. Kama kuna watu wazima wenye matatizo ya kusikia kwenye kikundi, andaa utaratibu wa ukalimani wa lugha ya alama au tumia maandishi na michoro.

**Kamusi:**

Ushiriki wa mtoto: Ushiriki wa mtoto ni tendo la kuwahusisha watoto katika kufanya maamuzi na kuwapa nafasi ya kutoa maoni kwenye mambo yanayoathiri maisha yao.

Msaada wa watu wazima: Maana ya msaada wa watu wazima katika ushiriki wa mtoto ni kwamba watu wazima wanaelewa nini maana ya ushiriki wa watoto na kuwasaidia watoto wanapotoa maoni yao kwa kuwasikiliza.

Mpango wa utekelezaji: Panga vitu gani vya kufanya na lini.

## 9.1 Methali kuhusu watoto

**Lengo:** Shughuli hii inaweza kufanywa na watu wazima pekee au na watu wazima waliochanganyika na watoto. Lengo ni kuchochea tafakari na mjadala kuhusu mitazamo ya kijamii na kitamaduni dhidi ya watoto na umuhimu wa mitazamo hii kwa sasa.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Kadi nyingi/vipande vya karatasi na kalamu za kutia alama.

**Muda:** Saa 1

**Kazi:**

1) Anzisha wazo la kutumia methali kama njia ya kuanzia mjadala wa masuala yanayohusu watoto na utoto.

2) Gawa washiriki katika vikundi vidogo vidogo vya watu 4-8 na waambie waainishe methali au misemo mingi ya Kitanzania kadiri wawezavyo inayohusu watoto. Wanaweza kuandika au kuchora kwenye kadi. Waambie washiriki wa vikundi wajadili misemo inasema nini kuhusu watoto, na kuzipanga kadi kulingana na methali zinazoendana na ambazo haziendani.
*Mifano ya methali:*
   - Asiye funzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
   - Samaki mkunje angalia mbichi
   - Mtoto akililia wembe mpe
   - Haba na haba hujaza kibaba
   - Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
   - Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe
   - Ukiona vyaelea ujue vimeundwa
   - Mtoto umleavyo ndiyo akuavyo
   - Isiyo kungwe haivushi
   - Uchungu wa mwana aujuae mzazi

3) Waambie washiriki wa vikundi waandike methali ambazo bado ni muhimu na zinafaa mpaka leo na kama zinaunga mkono au zinakatisha tamaa ushiriki wa mtoto katika kufanya maamuzi kwenye familia na jumuiya.

4) Ruhusu vikundi viwasilishe maainisho yao na kuelezea kwa nini.

**Tafakari na majadiliano:**

Jadili: Nyanja zipi za asili za tamaduni na mila ni chanya na zinatakiwa kuendelezwa, na zipi zinatakiwa zifanyiwe mabadiliko ili kuhakikisha kunakuwa na hali nzuri kwa watoto?

## 9.2 Kitu gani ni muhimu? Vipaumbele vya watoto na vya watu wazima

**Lengo:** Shughuli hii ingeweza kufanywa na watu wazima pekee au na mchanganyiko wa watu wazima na watoto. Lengo ni kuchochea tafakari kuhusu vipaumbele tofauti vya watu wazima na watoto ili kuongeza uelewa wa hali ya watoto.

**Kikundi:** watoto 8-30

**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama.

**Muda:** Saa 1

**Kazi:**

1) Wagawe washiriki katika vikundi vidogo vidogo vya watu 4-8. Waambie washiriki wa kila kikundi watoe mifano ya vipaumbele vya watoto na vya watu wazima vinavyotolewa nyumbani, shuleni na kwenye jamii na orodhesha baadhi ya maneno muhimu (au alama/michoro kama tatizo ni kujua kusoma na kuandika).

| **Nyumbani** | |
|---|---|
| Kitu gani ni muhimu kwa watoto? | Kitu gani ni muhimu kwa watu wazima? |
| **Shuleni** | |
| Kitu gani ni muhimu kwa watoto? | Kitu gani ni muhimu kwa watu wazima? |
| **Kwenye Jumuiya** | |
| Kitu gani ni muhimu kwa watoto? | Kitu gani ni muhimu kwa watu wazima? |

2) Ruhusu vikundi viwasilishe kazi zao.

**Tafakari na majadiliano:**

Jadili:

- Je, watu wazima na watoto wote wana vipaumbele vinavyofanana? Kwa nini/Kwa nini hapana?
- Je, vipaumbele vya watu wazima (wakati wote) huwa muhimu zaidi kuliko vya watoto? Kwa nini/Kwa nini hapana?
- Je, inawezekana kuhakikisha kwamba vipaumbele vyote vya watoto na watu wazima vinazingatiwa?

## 9.3 Manufaa na Mapungufu ya ushiriki  wa mtoto

**Lengo:** Shughuli hii ingeweza kufanywa na watu wazima pekee au na mchanganyiko wa watu wazima na watoto. Lengo ni kuchochea  tafakari kuhusu ushiriki  wa mtoto

**Ukubwa wa kikundi:** watu 8-30

**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**

1) Wafahamishe washiriki kuhusu dhana ya ushiriki  wa mtoto na jadili nini maana ya ushiriki  wa mtoto. (Kwa mfano, kuwapa watoto fursa ya kuhusishwa katika kufanya maamuzi na kutoa maoni kuhusu masuala yanayoathiri maisha yao). Waambie washiriki waainishe orodha ya wadau (watu binafsi, vikundi au taasisi) ambao wanaunga mkono ushiriki  wa watoto.
   Mifano:
   - Watoto
   - Wazazi
   - Shule
   - Wanajamii
   - Serikali

2) Gawa washiriki katika vikundi vidogo vidogo vya watu 4-8. Waambie washiriki wa kila kikundi waandae flipchati na kuchora jedwali kama lifuatalo, na kujadili kama kila mdau atanufaika au atapungukiwa na nini  pale watoto watakapohusishwa katika ufanyaji maamuzi.

| Mdau | Manufaa ushiriki  wa mtoto | Mapungufu ya ushiriki  wa mtoto |
|---|---|---|
| Mfano:<br>Wazazi | Watoto kuwa na majukumu mengi zaidi<br>Watoto kuwa na furaha<br>Familia kuwa na  amani zaidi | Watoto wanaweza kupoteza utii au heshimu kwa maamuzi ya wazazi |
| | | |

Kama kuna tatizo la kutojua kusoma na kuandika, fanya zoezi hili kwa njia ya mazungumzo na washiriki wote.

3) Ruhusu vikundi viwasilishe kazi zao.

**Tafakari na majadiliano:**

Jadili:

- Kwa ujumla kulikuwa na manufaa au mapungufu mengi zaidi?
- Tutawezaje kuhakikisha kwamba mapungufu yanayotokana na ushiriki wa watoto yanarekebishwa?

## 9.4 Ushiriki wa watoto siku za nyuma, sasa, na siku zijazo

**Lengo:** Shughuli hii iligusiwa katika Sura ya Kwanza, hata hivyo inaweza kufanyiwa na watu wazima kwa kujadili ushiriki wa watoto na kutafakari jinsi jamii inavyobadilika. Lengo ni kuongeza uelewa na tafakari kuhusu ushiriki wa mtoto miongoni mwa watoto.

**Ukubwa wa kikundi:** Kama kikundi ni kikubwa kigawe kwenye vikundi vidogo vidogo vya watu 6-8.

**Vifaa:** Vifaa tofauti vinavyopatikana kwenye mazingira ya kawaida (kwa mfano vijiti, majani, mawe ya aina tofauti, na vifaa chakavu). Kalamu na karatasi.

**Muda:** Takriban saa 2

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wa kila kikundi washirikiane katika kutengeneza angalau mazingira ya aina 3 ambayo ni muhimu kwa maisha ya watoto, kwa kutumia vifaa vya asili. Mazingira yanaweza kuwa ya nyumbani, shuleni, serikali ya mtaa au sehemu ambayo watoto hufanyia shughuli zao, lakini waache watoto wenyewe watoe mawazo yao.

2) Endesha mjadala mfupi miongoni mwa washiriki wote kuhusu maana ya ushiriki . Tilia mkazo kwenye ushiriki ukihusisha na ufanyaji maamuzi, na sio ushiriki katika shughuli tu. Halafu waambie washiriki wa vikundi kujadili mambo yafuatayo:

- Unafikiri ni kwa kiasi gani watoto walihusishwa kwenye ufanyaji maamuzi katika mazingira tofauti hapo zamani? Eleza nini maana ya zamani – kwa mfano wakati wazazi au mabibi na mababu walipokuwa wadogo. Kiwango cha ufanyaji maamuzi kionyeshwe kwa kutoa alama kuanzia kwa mfano 1-5. Hili linaweza kufanyika kwa kuweka mawe madogo madogo au vifaa vingine kwenye safu juu ya mchoro, jiwe 1 linamaanisha uhusishwaji wa kiwango cha chini, mawe 5 yanamaanisha uhusishwaji wa kiwango cha juu.

- Ni kwa kiwango gani watoto wanahusishwa katika ufanyaji maamuzi kwenye mazingira tofauti kwa hivi sasa? Tengeneza safu nyingine karibu na ya kwanza na onyesha kwa alama kiwango cha ufanyaji maamuzi.

- Unafikiri ni kwa kiwango gani watoto wanatakiwa wahusishwe katika kufanya maamuzi siku zijazo? Onyesha kiwango cha ufanyaji maamuzi kwa alama kwenye safu ya tatu.


3) Ruhusu vikundi viwasilishe kazi zao.

**Tafakari na majadiliano:**

Jadili:

- Kama kuna tofauti yoyote kati ya kiwango cha zamani na cha sasa cha ufanyaji maamuzi, ni kitu gani kilicholeta mabadiliko hayo?
- Zipi ni baadhi ya changamoto za ushiriki wa mtoto kwenye ufanyaji maamuzi katika jamii yetu kwa sasa?
- Kwa nini unataka uone ushiriki wa watoto unaongezeka /unapungua zaidi katika mazingira tofauti kwenye siku zinazokuja?
- Nini kinaweza kufanyika kuongeza ushiriki wa watoto?
- Je, alama zingekuwaje kama ungekuwa unaongelea kuhusu wasichana tu? Na kama ungekuwa unaongelea kuhusu wavulana tu?

## 9.5 Mambo anayotakiwa kuyafanya mtoto na mtu mzima katika ushiriki wa mtoto



**Lengo:** Kuondoa hofu kwa watu wazima kuhusu ushiriki wa watoto kwa kukubaliana kuhusu wajibu na majukumu. Kimsingi, shughuli hii inatakiwa ifanywe na watoto kwa kushirikiana na watu wazima, lakini pia inaweza kufanywa na watu wazima wenyewe.

**Ukubwa wa kikundi:**. Kama kikundi ni kikubwa, kigawe katika vikundi vidogo vya watu 6-8. Kama watu wazima wako tayari kutoa nafasi ya ushiriki kwa watoto, unaweza kuwachanganya watu wazima na watoto kwenye vikundi, au la wagawe katika vikundi tofauti.

**Vifaa:** Flipchati na kalamu za kutia alama.

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**

1) Waambie washiriki wa kila kikundi wachore angalau mazingira ya aina tatu kuonyesha maisha ya watoto (kwa mfano, shuleni na kwenye jamii). Chini ya kila picha ya hayo mazingira, wanatakiwa wachore picha ya mtu mzima na ya mtoto.

2) Waambie washiriki wa vikundi wajadili wajibu na majukumu ya watoto na watu wazima wakihusisha ushiriki wa watoto katika mazingira tofauti na kuandika maneno au kuweka alama muhimu pembeni mwa picha ya mtoto na mtu mzima.

3) Ruhusu kila kikundi kiwasilishe kazi zake.

**Tafakari na majadiliano:**

Jadili:

- Je, kuna mawazo tofauti na yanayofanana kati ya vikundi? Je unakubaliana na baadhi ya mawazo kwa ujumla?
- Je, Utahakikishaje kwamba watoto wote na watu wazima wanafahamu wajibu na majukumu yao?

## 9.6 Kuandaa mpango wa utekelezaji unaohusu ushiriki wa watoto

**Lengo:** Kuwahusisha watu wazima katika kuandaa mpango wa utekelezaji wa ushiriki wa watoto katika jamii, ili kuwafanya wajisikie kuwa ndio waanzilishi wa wazo hilo. Shughuli hii inatakiwa ifanywe na watoto kwa kushirikiana na watu wazima.

**Ukubwa wa kikundi:**
Kama kikundi ni kikubwa, kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watu 6-8. Kama watu wazima wako tayari kutoa nafasi ya ushiriki wa watoto, unaweza kuwachanganya watoto na watu wazima kwenye vikundi, la sivyo wagawe katika vikundi tofauti.

**Vifaa:** Kadi nyingi/vipande vya karatasi, flipchati na kalamu ya kutia alama.

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**

1) Kiambie kila kikundi kitoe malengo 3 rahisi kwa ajili ya kuongeza ushiriki wa watoto kwenye jamii ya kawaida na kuandika au kuyachora kwenye hizo kadi.

2) Wakusanye washiriki wa vikundi vyote pamoja na jadili malengo waliyotoa. Kubalianeni kuhusu malengo yapi yafanyiwe kazi. Mfano wa lengo: kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu wanasikiliza maoni ya (kwa mfano, wanapo tambua watoto wenye mahitaji ya matunzo na ulinzi katika jamii wanamoishi)

3) Waambie washiriki wa kila kikundi wabuni angalau shughuli tatu rahisi ambazo zinaweza kufanywa na washiriki ili kufikia malengo yao. Mfano wa shughuli: kila mshiriki mtu mzima atafanya mijadala isiyokuwa rasmi na mtu aliye karibu yake kuhusu ushiriki wa watoto katika kamati ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu ndani ya wiki nne zijazo.

4) Ruhusu vikundi viwasilishe kazi zao. Zipe shughuli uzito kwa kutoa alama (mpe kila mshiriki kwa mfano mawe 3 na waache waainishe shughuli wanazoziona kuwa ni muhimu kuliko zote. Kubalianeni kuhusu nani atafanya shughuli zilizopewa kipaumbele. kikubwa zaidi na zitafanyika lini.

## 9.7 Kujadili na watu wazima kuhusu haki na ulinzi wa watoto

**Lengo:** Kuhusisha watu wazima katika kujadili haki na ulinzi wa watoto, ili kuwahamasisha wachukue hatua dhidi ya ukiukwaji wa haki za mtoto. Ulinzi wa watoto unamaanisha kuzuia na kuitikia pale inapotokea vurugu,unyonyaji na udhalilishaji dhidi ya watoto – hii ikiwa ni pamoja na unyonyaji unofanywa kwa watoto katika bishara ya ngono,ajira za watoto, kusafirisha watoto kutoka mjumbani kwao kwenda kufanyishwa kazi mijini, na vitendo vya kimila ambazo ni hatari kwa afya ya mtoto kama vile ukeketaji/tohara kwa watoto wa kike na ndoa za utotoni.
Ukubwa wa kikundi: kama kikundi ni kikubwa, kigawe katika vikundi vidogo vidogo vya watu 6-8.

**Vifaa:** Kadi/vipande vya karatasi, flipchati na kalamu za kutia alama.

**Muda:** Saa 1-2

**Kazi:**

1) Wasilisha kwa washiriki wazo la haki za mtoto na makubaliano ya haki za mtoto, kwa kutumia tafsiri ya lugha rahisi ya makubaliano hayo (tazama tafsiri iliyoambatishwa uk 128). Kama watu wazima hawajui kusoma na kuandika, basi wasilisha hoja hizo kwa michoro au alama.

2) Mwambie kila mshiriki abainishe haki 3 ambazo anaziona ni muhimu kuliko zote. Halafu waambie washiriki waunde vikundi vya watu 4 na kujadili vipaumbele vyao. Kubalianeni kuhusu haki 3 katika kikundi.


3) Ruhusu kila kikundi kiwasilishe kazi zake.
Jadili: Je, ilikuwa ni vigumu kukubaliana kuhusu haki tatu? Kwa nini, Kwa nini hapana? Majukumu yapi yanahusiana na haki hizo? Je, Haki kuu za mtoto zinaendana au kupingana na mila katika jamii? Je, kuna haki yoyote ya mtoto inayokiukwa katika jamii? Toa mifano.

5) Waambie washiriki wa vikundi wajadili nini kingeweza kufanyika kama haki za mtoto zinakiukwa katika jamii. Jadili mifano ya ukiukwaji wa haki za mtoto na orodhesha asasi au watu binafsi katika jamii ambao unaweza kuwafuata kwa ajili ya msaada kama unawafahamu watoto wanaokabiliwa na matatizo haya. Jadili asasi zipi au watu gani wanaweza kusaidia masuala yapi.

   Mifano:
   - kamati ya ulinzi wa mtoto ya wilaya
   - Ofisi ya ustawi wa jamii (ofisi ya wilaya)
   - Kituo cha msaada wa sheria (haki, masuala ya kisheria)
   - Asasi zisizo za kiserikali
   - Polisi
   - Madaktari wauguzi ,hospitali, kliniki
   - Viongozi wa kijiji/kijamii

Tazama sehemu ya 6.2 kwa ajili ya ufafanuzi unaohusu kujadili masuala ya haki za mtoto.

# Sura ya 10: Tunawezaje kucheza na kuimarisha nguvu?



Michezo na vitendo vingine vya kuimarisha nguvu hufanya mikutano na shughuli nyingine za kikundi kuvutia zaidi, na husaidia kuwafanya washiriki kuwa wachangamfu na wenye umoja. Tumia michezo iliyozoeleka kwenye jamii husika au inayoendana na mawazo yalitajwa kwenye kielezi hiki.

**Mwongozo**

- Mchezo ni kitu cha hiari. Tambua na heshimu utayari wa kila mtoto wa kushiriki kwenye mchezo. Kuna michezo inayoweza kuwaogopesha baadhi ya watoto.
- Chagua michezo jumuishi, na hakikisha kila mtoto kwenye kikundi, wakiwemo wenye ulemavu, anashiriki.
- Wewe mwenyewe hakikisha unashiriki.

**Simba-mamba**
Chora mistari miwili sambamba sakafuni ili kutengeneza 'mto'. Waambie washiriki wasimame kwenye pande zote mbili za mto. Waambie kwamba utakaposema 'simba', wanatakiwa kurukia mtoni ili wasije wakaliwa. Utakaposema 'mamba', wanapaswa kutoka mtoni upesi ili wasije wakaliwa na mamba. Kama mshiriki atafanya kosa, atakuwa ametolewa kwenye mchezo.

**Haramu**
Waambie washiriki wasimame kwenye mduara na kuhesabu (kila mtu akisema namba moja). Eleza kwamba namba 7 (au namba nyingine yoyote ile) ni haramu, hivyo kama kati ya namba zako kuna 7, badala ya kusema namba hiyo, unatakiwa kupiga makofi.

**Doni doni pangarara**
Waambie washiriki waguse upande wa juu wa viganja vya washiriki wenzao, kiganja kimoja juu ya mkono wa mtu mwingine. Kila mtu atumie mikono yote miwili, lakini hakikisha hakuna mtu anayegusa mkono wake mwenyewe. Imba au sema 'doni, doni' kwa kama dakika mbili, halafu sema 'pangarara' (mtandao umevunjika). Washiriki wanapaswa kuwa wasikivu na haraka waachanishe mikono yao.

**Lingu lingu akalingulila**
Waambie washiriki watengeneze duara. Mpe kila mshiriki namba, 1 au 2, kwa kuhesabu. Acha washiriki waimbe au waseme 'lingu lingu, lingu lingu, akalingulila' huku wakipiga makofi, huku wakiwa wameinamia kwa mbele. Watakaposema 'akalingulila', wote wenye namba 1 wasogee mbele na kuangaliana, huku wale wote wenye namba 2 wakirudi nyuma na kuangaliana.


**Nyama nyama**
Waambie washiriki wasimame kwenye duara wakiwa wameshikana mikono, wakiipeleka mbele na kuirudisha nyuma kwa mwendo wa taratibu. Sema 'nyama, nyama'. Washiriki wanapaswa kujibu 'nyama'. Halafu sema aina mojawapo ya nyama, kwa mfano, 'nyama ya kuku', 'nyama ya ngombe', 'nyama ya simba', nk. Pale utakaposema aina ya nyama zinazoliwa kwenye jamii hiyo, jibu kutoka kwa washirki linatakiwa kuwa 'nyama', ila kama aina hiyo ya nyama hailiwi, wanatakiwa wabaki kimya. Kama mshiriki atafanya kosa, atakuwa ametolewa kwenye mchezo.

**Kusogea**
Waambie washiriki wasimame kwenye mduara. Sema 'wote wasogee ambao…. (sema sifa bainifu fulani)'. Washiriki wote wenye sifa hii wahame kutoka kwenye nafasi zao. Mifano inaweza kuwa 'Wote wasogee ambao – wamevaa nguo ya bluu, wamechota maji asubuhi hii (au wiki hii), wanapenda maembe, walisikiliza redio jana' nk.

**Umbeya wa kujenga**
Gawa washiriki kwenye makundi ya watu 3. Mwambie mshiriki mmoja akae chini akiwa amewapa mgongo washiriki wengine, huku nao wakiwa wanapiga umbeya kuhusu yeye kwa muda fulani mtakaopanga. Umbeya wote utakaosemwa unatakiwa uwe wa kujenga. Badilishaneni siti. Baada ya hapo jadilini namna washiriki walivyojisikia.

**Daladala**
Waambie washiriki kutengeneza daladala (vibasi) kulingana na sifa zao bainifu zinazofanana. Sema kwa sauti sifa hizo na waambie washiriki waunde daladala upesi. Sifa bainifu zinaweza kuwa rangi ya nguo, muda waliotumia kuja mkutanoni, wanavyojisikia, nk.)

# 11. Orodha za kukagulia ushiriki wa mtoto



Lengo la orodha hizi ni kufanya ushughulikiaji wa ushiriki wa mtoto uwe wa dhati na halisi.

Orodha hii kwa ajili ya ukaguzi wa ushiriki wa watoto ni orodha fupi ya maswali kwa ajili ya kuwauliza watoto baada ya kuwa wameshiriki kwenye shughuli za ushiriki wa watoto kwa kipindi fulani. Endapo watoto wote watajibu ndiyo kwa maswali haya, hii inakupa ishara kwamba kazi yako inaenda vizuri. Unaweza kuwataka watoto wajibu maswali haya mmoja mmoja na baada ya hapo mkajadili kama kikundi ili kuelewa sababu hasa zilizowafanya watoto watoe majibu hayo.

Orodha ya kukagulia ambayo ni maalumu kwa watu wazima inauliza maswali kadhaa, ambayo unatakiwa uweze kuyajibu 'ndiyo', endapo shughuli zako za kuwashirikisha watoto ni za dhati. Unaweza kuipitia orodha kabla ya kuanza kazi ili kuhamasika, na baadaye kuitumia kuangalia kama shughuli zako zinaenda kama ilivyopangwa. Kama utaweza kusema ndiyo kwa idadi kubwa ya maswali haya, basi haina shaka kuwa mambo yanaenda sawa. Ikiwa utapata 'hapana' nyingi, tafakari kuhusu uwezekano wa kubadilisha mbinu yako unayotumia.

**Orodha ya kukagulia kwa ajili ya watoto**

- Je, kikundi kinakutana mara kwa mara?
- Je, unapata taarifa za kutosha kuhusu shughuli zinazoendelea kwenye kikundi?
- Je, hauna tatizo lolote na muda wa kukutana na sehemu za kukutania?
- Je, unashirikishwa katika ufanyaji maamuzi ndani ya kikundi?
- Je, unashirikishwa katika kuamua aina ya shughuli za kufanya?
- Je, uliombwa kutoa mtazamo wako kuhusu shughuli hizi?
- Je, unafurahia shughuli hizi?
- Je, unajiona kuwa huru wakati mikutano na shughuli za kikundi zinapofanyika?
- Je, unadhani unasikilizwa?
- Je, kila mtu anapata fursa ya kushiriki kwenye shughuli za kikundi?
- Je, unadhani mazingira ya kikundi ni mazuri kwako?
- Je, unadhani kuwa shughuli mnazofanya zinaleta mabadiliko?
- Je, una ufahamu kuhusu haki za mtoto?
- Je, unafahamu wajibu wako?
- Je, unajiona kuwa salama wakati wa mikutano na shughuli nyingine za kikundi?
- Je, wazazi au walezi wako wanaunga mkono wewe kuwa sehemu ya kikundi chenu?
- Je, unashiriki katika kufanya maamuzi mbalimbali kwenye familia yako?

**Orodha ya kukagulia kwa ajili ya watu wazima**

**Je, ni halisi?**

- Je, watoto wanakutana mara kwa mara?
- Je, watoto wako huru kuelezea mitazamo yao?
- Je, watoto wanafahamu haki zao?
- Je, watoto wanaelewa wajibu wao na majukumu yao?
- Je, watoto wanapata taarifa husika kwa ajili ya shughuli zao?
- Je, watoto wanashirikishwa katika uwekaji wa malengo ya kikundi?
- Je, watoto wanapanga na kuanzisha shughuli zao wenyewe?
- Je, watoto wanafanya maamuzi?
- Je, watoto wanasimamia wenyewe na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli wanazofanya?

**Je, ni muhimu?**

- Je, watoto wanachukulia kwa umuhimu masuala yanayojadiliwa na shughuli zinazofanywa na kikundi?
- Je, shughuli hizo zinaleta mabadiliko?
- Je, kuna mabadiliko?
- Je, shughuli hizo zinategemea uwezo na uzoefu wa watoto pekee?

**Je, ni ya heshima?**

- Je, watu wazima wanawasikiliza watoto wote na kufanya juhudi kukumbuka majina yao?
- Je, watu wazima wanasikiliza maoni wanayotoa watoto?
- Je, watu wazima wanathamini maoni haya?

- Je, watu wazima wanatenga muda kwa ajili ya kusikiliza maswali, matarajio na maombi ya watoto?
- Je, watu wazima wanatoa maelezo pale wanapokuwa hawafuati ushauri unaotolewa na watoto?

**Je, ni jumuishi?**

- Je, watoto wote wanapata nafasi ya kushiriki bila kujali jinsia, kabila, hali yao kiafya, imani zao, mazingira wanayoishi, maisha yao ya nyuma, n.k.?
- Je wasichana wanashiriki kwa usawa na wavulana? Je, wasichana wanaweza kuweka wazi mambo yote wanayotaka kusema pale wavulana wanapokuwepo (au kinyume chake)? Je, kuna wasichana walio katika nafasi za uongozi?
- Je, kuna utaratibu wowote uliowekwa ili kuhakikisha kuwa watoto walio katika mazingira hatarishi au wale wenye ulemavu wanaweza kushiriki? Je, kuna watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi au wale wenye ulemavu katika nafasi za uongozi?
- Je, watoto wa umri tofauti wanashiriki? Je, watoto wadogo wanapewa nafasi ya kusema maoni yao?
- Je, kuna uzingatiaji wa hali ya watoto na vipaji vyao mbalimbali wakati wa kupanga shughuli za kikundi?

Je, mazingira ni mazuri kwa watoto?

- Watoto wameshawahi kuombwa kutoa maoni yao kuhusu muda na mahali pa kukutania.
- Je, majukumu mengine waliyonayo watoto yanaheshimiwa?
- Je, lugha inayotumika inaeleweka na wote?
- Je, shughuli zinazofanyika zinawajengea watoto uwezo na kuwafanya wajiamini?

**Je, ni ya hiari?**

- Je watoto wanafahamu vya kutosha kuhusu wajibu wao na michakato pamoja na shughuli zinazofanyika?
- Je, watoto wanaweza kusema hapana wanapotakiwa kushiriki?

**Je, ina ulinzi?**

- Je, kuna utaratibu wowote uliowekwa kuwakinga watoto dhidi ya unyanyasaji?
- Je, uko tayari kuwasaidia watoto wanaopata upinzani kutoka kwa familia au watu wengine wazima kwa sababu ya kushiriki?
- Je, watu wazima wanajibu maswali ya watoto, na kushughulikia mahitaji na matatizo yao yote?

**Je, watu wazima wanaunga mkono?**

- Je, wazazi waliridhia watoto wao kushiriki?
- Kumekuwa na majadiliano miongoni mwa watu wazima kuhusu ushiriki wa watoto?
- Je, watu wazima wanawajumuisha watoto kwenye mikutano na mijadala?
- Je, watu wazima wanafahamu kuhusu haki za mtoto?
- Je, watu wazima wanaelewa wajibu wao na majukumu wanayopaswa kutekeleza?

## Marejeo

### Vielekezi

Arigatou Foundation, UNESCO na UNICEF
2008 Learning to Live Together. An Intercultural and Interfaith Programme for Ethics Education
International guidelines and tool-kit for youth leaders and educators. The aim is to strengthen children's commitment to justice, respect for human rights, and to build harmonious relationships between individuals and within societies.

Chambers, Robert
2002 Participatory Workshops. A sourcebook of 21 sets of ideas and activities. Earthscan.
Sourcebook with ideas for doing participatory workshops.

Children's Dignity Forum, OWA, FORWARD
Training Manual for the Sister to Sister Programme. Intervention Programme to end Child Marriages in Tanzania.
Tanzanian training manual for facilitators aiming to form Sister to Sister Clubs. The aim is to motivate girls to work in groups and empower each other through sharing experiences, information and skills.

Christian Children's Fund
2008 We've got something to say. Promoting Child and Youth Agency. A Facilitator's Manual.
International manual for people working with children and youth as partners in development processes. The manual provide guidelines and practical tools for involving children and youth in consultations, planning, implementation, governance and monitoring and evaluation.

Commonwealth Secretariat
2005 Tools for Adolescent and Youth Participation.
International collection of practical participatory tools for working with adolescents and youth.

Dynamix and UNICEF
2006 Toolbox of Participatory Tools. Adapted from the UNICEF Tanzania Workshop on Participatory Approaches for Working with Children and Young People in Programme Planning, Implementation and Studies and Evaluation.
Manual introducing a number of participatory tools for working with children and young people.

Mkombozi Centre for Street Children
2004 Back to Basics. An Approach to Creating Democratic Communities through Child Participation.
A manual for adults working with children focusing on child participation concepts and principles in mainly organizational and institutional settings. It includes a check-list on child-friendly decision-making for organization and institutions.

REPOA, research on Poverty Alleviation. Children's Research Programme.
2008 Training Manual on Researching with Children. Draft
Tanzanian training manual for facilitators or trainers who work to enhance the understanding of adult researchers on how to involve and work with children and young people in research.

**Miongozo**

JCURT, The Junior Council of the United Republic of Tanzania
2004 Guidelines for the formation of Junior Councils. The Guidelines for forming District and Region Councils.
The guidelines give instructions on formation and elections, and some overall guidelines on facilitations of meetings.

REPSSI
2009 Mainstreaming Psychosocial Care and Support through Child Participation
International manual with guidelines and tools for individuals working in or funding programmes working with vulnerable children (staff or donors). The aim is to increase the understanding on how child participation contributes to the psychological well-being of children.

Save the Children
Practice Standards in Child Participation.
International guidelines for working with child participation within Save the Children programs.

IAWGCP, Inter-Agency Working Group on Children's Participation
2007 Children's Participation in Decision Making: Why do it, when to do it, how to do it.
Guidelines for people in public leadership and service. It provides a check-list for assessing the possibilities for child participation in structures related to justice, health, education, community services and information, entry-points for promoting and improving children's participation in public life, and guidelines for ensuring effective participation.

Nadharia na Usuli kuhusu Ushiriki  wa Mtoto
Rajani, Rakesh
2001 The Participation Rights of Adolescents: A Strategic Approach. UNICEF Working Papers Series.
A theoretical introduction to adolescent participation (defined as people from 10-19 years), a set of strategies and entry points for working with participation and suggestions for a number of practical steps for promoting adolescent participation.

Lansdown, Gerison
2001 Promoting Children's Participation in Democratic Decision-Making. UNICEF
The publication presents implications and rationales of the right to participation, some fundamental principles/guidelines for participation, provides a number of examples of child participation around the world and, lastly, and discusses how to involve children in conferences in meaningful ways.

UNFPA & The African Child Policy Forum
Youth Participation. Concepts, Models and Experiences.
The publication discusses the roles of youth in the society, barriers to effective youth participation and possible ways of overcoming them, and provides a set of general suggestions on how to promote youth participation.

**Ushiriki  wa watoto katika Tanzania**

ACPF, Jukwaa la Afrika la Sera ya Mtoto na UNICEF
2006 What Children and Youth Think. Tanzania. A Statistical Presentation of Opinions and Perceptions of Children and Youth in Tanzani, 2006.

**Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mkukuta**

2007 Tanzanian Children's Perceptions of Education and Their Role in Society. Views of the Children 2007.

**Sheria na Mikataba**

OAU
1990 Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto
OAU Doc. CAB/LEG/24.9/49 (1990), yalianza kutumika  Nov. 29, 1999.
UN CRC
1989 Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto
Ulipitishwa na kuwekwa wazi kwa ajili ya kusainiwa, kuridhiwa na kuridhiwa na kupewa nyongeza na  Azimio la Baraza Kuu la

Umoja wa Mataifa 44/25 la 20 Novemba 1989. Ulianza kutumika Septemba 2 1990, kulingana na kifungu cha 49

JMT, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
2008a Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania (Sera ya Maendeleo ya mtoto iliyopitiwa upya).

JMT, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
2009 Sheria ya Mtoto

**Azimio la haki za mtoto katika lugha rahisi**
kutoka: http://www.un.org/cyberschoolbus/

1. **Kila mtoto ana haki katika mambo haya yafuatayo bila kujali mbari yake, rangi, jinsi, lugha, dini, msimamo au mawazo ya kisiasa, au mahali alikozaliwa au wazazi wake. Haki ya:**
2. **Kukua kimwili na kiroho katika mazingira yanayojali afya, uhuru na utu wake.**
3. **Kupewa jina na kuwa na nchi.**
4. **Kujaliwa, kulindwa, kupata chakula kinachofaa, makazi na huduma za afya.**
5. **Kupewa huduma maalum iwapo ana kilema chochote.**
6. **Kupendwa na kutambulika, hasusani na wazazi na familia yake, lakini pia na serikali pale ambapo hapati vitu hivyo kutoka kwa wazazi na familia yake.**
7. **Kupatiwa elimu bure, kucheza, kupewa fursa sawa ya kujiendeleza na kujifunza namna ya kuwajibika na kutumikia jamii. Wazazi wa mtoto wanalo jukumu la kumpatia elimu na miongozo mingine ya maisha.**
8. **Kuwa wa kwanza kuhudumiwa wakati wote.**
9. **Kulindwa dhidi ya vitendo vya kikatili au vya kiunyonyaji, kwa mfano, kutolazimishwa kufanya kazi hatarishi kwa ukuaji wake kimwili na kiakili.**
   **Mtoto haruhusiwi kufanya kazi kabla ya kufikia umri unaokubalika kisheria na hapaswi kabisa kufanya kazi itakayomdhuru kiafya, kimaadili na kimwili.**
10. **Kufundishwa amani, utangamano, uvumilivu na mahusiano mema ya watu.**

# Sheria ya Mtoto

***Kila mwenye umri ulio chini ya miaka 18 ni mtoto.***

***Watoto wote nchini Tanzania wanalindwa na Sheria hii ya Mtoto.***

*Watoto wana haki ya kupewa jina na utaifa na kusajiliwa mara baada ya kuzaliwa. Ni kinyume cha sheria kwa mtu yeyote kumnyanyasa mtoto eti kwa sababu ni msichana au mvulana, au kwa sababu ya umri wake au dini au asili yake au kwa sababu yeye ni masikini.*

*Watoto wana haki ya kutoa maoni yao juu ya uamuzi unaofanywa kuhusu maisha yao, na ni wajibu wa watu wazima kuzingatia maoni ya watoto pale wanapofanya uamuzi huo.*

### *Kinga ya mtoto*
*Hakuna anayeruhusiwa kumdhuru, kumwumiza au kumnyonya mtoto. Yeyote anayejua kwamba kuna mtoto anayeonewa au kutendewa vibaya hana budi kutoa taarifa kuhusu vitendo hivyo.*

*Adhabu kwa mtoto haipaswi kuwa kali au yenye kumdhalilisha.*

### *Maisha ya familia*
*Watoto wana haki ya kuwafahamu wazazi wao na kuishi nao katika mazingira ya kuwajali na yenye amani. Watoto nao wana wajibu wa kuwaheshimu na kusaidia familia zao.*

*Endapo wazazi watatalikiana, Mahakama itaamua mtoto aishi na mzazi yupi. Watoto walio na umri chini ya miaka saba kwa kawaida huishi na mama zao. Mtoto ana haki ya kumtembelea na kuishi na mzazi mwingine, isipokuwa pale tu kama hatua hiyo itaingilia masomo yake.*

*Akina baba hawana budi kuchangia matunzo ya watoto wao hadi pale watakapofikisha umri wa miaka 18.*

*Endapo wazazi wote wawili watafariki, na hakuna ndugu wa kumtunza mtoto huyo, au kama mtoto hatunzwi, anatelekezwa au anatendewa vibaya na wazazi wake, basi Dola haina budi kuwapa watoto wa aina hii mahali salama pa kuishi.*

*Watoto wanaokutwa wakiombaomba au kuishi mitaani wanaweza kurejeshwa kwenye familia zao. Kama watoto hawa hawatakuwa salama mikononi mwa wazazi, mamlaka zinaweza kuweka utaratibu mwingine ili watoto hao waishi na familia itakayowaasili au katika makazi mengine yaliyokubalika.*

*Watoto pia wanaweza kuasiliwa endapo tu wazazi wanaomwasili mtoto wamethibitishwa na kuonekana kwamba wanaweza kumpa mtoto matunzo sahihi.*

### *Chakula, makazi, matunzo ya afya na shule*
*Wazazi na walezi hawana budi kuwalinda watoto dhidi ya madhara yoyote. Vilevile ni lazima wahakikishe kwamba watoto wanapata chakula, mavazi na mahali salama pa kuishi.*

*Wazazi hawana budi kuhakikisha kwamba watoto wanapata kinga dhidi ya magonjwa mbalimbali. Inapotokea watoto kuugua, basi wapelekwe hospitalini.*

*Wazazi hawana budi kuwapeleka watoto shuleni na kuwapa nafasi ya kucheza na kupumzika. Matunzo na huduma maalumu zitolewe kwa watoto wanaoishi na ulemavu ili nao waweze kwenda shule kama watoto wengine.*

### *Kazi na watoto*
*Watoto wana ruhusa ya kufanya kazi baada tu ya kutimiza miaka 14. Kazi haipaswi kumzuia mtoto kuhudhuria masomo au kupata muda wa kujisomea na kupumzika. Watoto wasiajiriwe kufanya kazi nyakati za usiku.*

*Yeyote anayewafanyisha kazi watoto kupita kiasi, au asiyewalipa ujira unaostahili, basi anavunja sheria hii.*

*Ni makosa kuajiri mtoto kama kazi anayopaswa kufanya ni ya hatari. Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi za baharini, kwenye machimbo au eneo la kupasua mawe na kokoto, wala kubeba mizigo mizito au kufanya kazi zinazotumia kemikali au mitambo. Watoto hawaruhusiwi kufanya kazi za hotelini wala vilabu vya pombe.*

### *Utoaji Haki kwa Watoto*
*Mahakama maalumu zinazoitwa Mahakama za Watoto hazina budi kuanzishwa ili zishughulike na watoto tu. Mahakama hizi maalumu hujitahidi kuhakikisha kwamba watoto hawatishiki kwenda Mahakamani.*

*Watoto wanaoshitakiwa kwa jinai na wanaopelekwa kituo cha polisi wanaweza kuachiwa warudi kwa wazazi wao au wanaweza kupelekwa kwenye nyumba maalumu za kuangalizia watoto ili kusubiri kesi zao zilizo mahakamani.*

*Wanapokuwa Mahakamani, watoto wana haki ya kuwakilishwa na wakili. Vilevile ni lazima waruhusiwe kutoa maoni yao na kueleza yale wanayofahamu kuhusu kilichotokea.*

*Watoto wanaoonekana kuwa na hatia kwa makosa ya jinai wanaweza kuachiliwa huru kwa sharti la kuonyesha tabia njema, au wanaweza kupelekwa kwenye shule zilizoteuliwa kwa ajili hiyo. Watoto hawaruhusiwi kuwekwa gerezani.*



unicef
United Nations Children's Funds
Bibi Titi Mohamed/Magore Street P.O. Box 4076, Dar es Salaam
Tanzania

Ministry of Community Development, Gender and Children
Tanzania